# UPOTOFU NDANI YA KITABU CHA MITAALA KWA SHULE ZA SEKONDARI JUU YA UISLAMU

## Usahihi wa Historia Ni Maandiko Si Ukoo


**Kimeandikwa na:**
Muhammad A. Bahsan

**Kimehaririwa na:**
Alhaji Hemedi Lubumba

**Kimepitiwa na:**
Al Haji Ramadhani S. K. Shemahimbo
Na
Mbarak A. Nkanatila

**© Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
**Al-Itrah Foundation**

**ISBN No:** 978 - 9987 - 17 - 065 - 4

**Kimeandikwa na:**
Muhammad A. Bahsan

**Kimehaririwa na:**
Alhaji Hemedi Lubumba Selemani

**Kimepitiwa na:**
Al Haji Ramadhani S. K. Shemahimbo
Na
Mbarak A. Nkanatila

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Mei, 2014
**Nakala:** 1000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.ibn-tv-com
**Katika mtandao:** www.alitrah.info

# YALIYOMO


Neno la Mchapishaji .......... 1

Utangulizi .......... 3

Pengo la Uongozi Baada ya kutawafu Mtume .......... 5

Uchaguzi wa Khalifa wa kwanza .......... 7

Hali Ilivyokuwa Katika Mkutano .......... 11

Hotuba ya Abu Bakar .......... 26

Tukio la Karatasi .......... 34

Uteuzi wa Makhalifa Wengine .......... 64

Uteuzi wa Umar .......... 67

Kuteuliwa kwa Uthman .......... 69

Uteuzi wa Imamu Ali (a.s) .......... 73

Uongozi Baada ya Khalifa Ali (a.s) .......... 77

Mtindo Usio wa Kiislamu! .......... 83

Mgawanyiko wa Waislamu .......... 94

Upinzani wakati wa Ukhalifa wa Ali .......... 96

Hitimisho .......... 124

بسم الله الرحمن الرحيم

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako ni tanbihi juu ya kitabu, Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha Nne, kilichoandikwa na Islamic Education Panel, chini ya usimamizi wa Bakwata na Wizara ya Elimu Zanzibar.

Ingawa mwandishi amekikosoa zaidi kitabu hiki cha nne, lakini ukweli ni kwamba vitabu vyote vilivyoandikwa na taasisi hii inayojiita Islamic Education Panel kwa ajili ya mitaala ya kufundishia wanafunzi wa shule za Sekondari vina makosa ya kimakusudi kabisa.

Malengo makubwa ya taasisi hii ni kuwapotosha vijana wetu ili kukidhi fikra za uovu wao kwa kuwatumia vijana. Na hiki ni kiashiria cha uvunjaji wa amani katika jamii yetu.

Je, wameandika kwa kuwaelemisha wanafunzi au kwa ajili ya upinzani wao dhidi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na madhehebu nyingine za Kiislamu ambazo hazikubaliani na itikadi zao?

Sisi tunawashauri wanafunzi wasome vitabu sahihi vya historia ya Uislamu ili wajionee ukweli na wasikubali kamwe kuburuzwa na hao wanaojiita wasomi wenye chuki za kimadhehebu na ambao kwa kweli hawautakii mema Uislamu.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina tena nafasi katika akili za watu.

Kwa hivyo, taasisi yetu ya Al-Itrah imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu Sayyid Muhammad A. Bahsan kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kukichmbua kitabu hiki na kuweka wazi makosa yaliyomo ndani yake. Allah (‘Azza wa Jalla) amzidishie ilmu, fahamu, afya njema na maisha marefu katika huduma hii ya Uislamu. Aidha, tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kitabu hiki. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na kesho Akhera – Amin kisha amin.

**Mchapishaji**
**Al-Itrah Foundation**

بسم الله الرحمن الرحيم

# UTANGULIZI

## KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU, MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

Sifa zote njema zinamstahikia Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, kisha Swala na Salamu zimwendee Mtume wetu Mtukufu (s.a.w.w.) ambaye aliletwa ili awe ni rehema kwa walimwengu wote, pia ziwaendee watu wa nyumbani kwake waliotakaswa na Maswahaba zake walio wema.

Ndugu msomaji mpendwa, kitabu hiki kilicho mikononi mwako ni masahihisho (majibu) yatokanayo na kitabu kijulikanacho kwa jina la *'Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha Nne'* kilichoandikwa na Islamic Education Panel, Chini ya Usimamizi wa Bakwata na Wizara ya Elimu Zanzibar, katika sehemu ya Historia. Kila mwenye kuyasoma yale yaliyoandikwa katika maudhui hayo ataona ni namna gani Historia ya Kiislamu ilivyopindishwa kombo, kwa kubebeshwa lawama na tuhuma nzito wale wasiostahiki hayo, hasa kwa yule ambaye ni mtu bora baada ya Mtume (s.a.w.w.), mtu huyo ni Imamu Ali (a.s.), pamoja na wafuasi wake miongoni mwa Maswahaba. Kutokana na umuhimu wa historia katika kila jamii, kwani historia ndio kioo chao, tumeona ni wajibu kufanya hiki tulichokifanya ili ukweli ubainike na Waislamu watambuane na kujuana kwa ukweli, badala ya kila mmoja kujipa jukumu la kuzungumza juu ya mwengine kwa kumsingizia yale asiyoyaamini na kuyafuata.

Katika utafiti huu hatuna lengo la kuleta mfarakano kati ya Waislamu, bali ni kusahihisha yale yasio sahihi kwa mujibu wa kauli za Maulamaa wa Kiahli Sunna, kwa hivyo tumetumia zaidi njia ya kunakili katika utafiti huu. Na ikiwa kuna yeyote aliyeguswa na utafiti huu, atambue kwamba lengo letu si hilo, bali ni kubainisha haki na ukweli, na tunaelewa kwamba ukweli unatabia ya kuuma, lakini ndio wa kufuatwa.

**Ewe Mola! Tusaidie,**
**Muhammad A. Bahsan.**

بسم الله الرحمن الرحيم

# PENGO LA UONGOZI BAADA YA KUTAWAFU MTUME ((S.A.W.W.))

Jambo la mwanzo ambalo tumeamua kulijadili na kueleza ukweli ulivyo, ni namna hali ilivyotokea baada ya kufariki Mtume (s.a.w.w.), ambapo tunaona kwamba watayarishaji hao wa Kitabu hicho hawakutenda haki katika kuelezea hali halisi ilivyojiri wakati huo, katika kichwa cha habari walichokitaja hapo juu wamesema yafuatayo:

> "Kifo cha Mtume kiliacha pengo la kiongozi wa Dola, Muhammad alikuwa Mtume wa mwisho hakua na naibu wala Mtume mwingine baada yake. Hivyo kabla ya kuzikwa Mtume, wazo la kupatikana kiongozi wa Dola ndilo lililotawala huzuni ya kila Sahaba. Mtume (s.a.w.) hakuacha usia wowote wa nani awe kiongozi baada ya kifo chake, sio kauli wala ishara. Kule kumuachia Abubakar kuongoza swala asipokuwepo na pale alipokuwepo siku chache kabla ya kifo chake kamwe sio vielelezo vya kumtawaza Abubakar. Ingawa inaweza kuchukuliwa kuwa ni dokezo la kiongozi anaefaa."[1]

Ni kweli kifo cha Mtume (s.a.w.w.) kiliacha pengo kwa Waislamu, lakini kutokana na umuhimu wa jamii yeyote ile kwa kuanzia ngazi ya familia inatambua umuhimu wa kuwepo kiongozi, pindi kiongozi wa familia anaposafiri hata kama ni kwa muda wa siku chache, humteua mtu fulani kuwa mwangalizi wa familia yake. Basi ni vipi kwa Mtume (s.a.w.w.) asifanye hivyo, na ilhali alikuwa

[1] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.320.

akitambua vyema kwamba ataiaga dunia? Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akitambua vyema umuhimu wa kiongozi katika jamii, hii ndio maana alikuwa haondoki katika mji wa Madina ila humuacha mtu atakayeshika nafasi yake.

Kwa hivyo pengo la kuondoka kwake alilitafutia mtu wa kulijaza, na haya tunayashuhudia katika maneno yake mwenyewe kama tutakavyoyabainisha, kwani si tu kwamba kuna ishara za nani awe kiongozi baada yake, bali kuna maandiko sahihi juu ya jambo hili.

Ni kweli kule kumwachia Abu Bakar kuongoza Swala asipokuwepo na pale alipokuwepo siku chache kabla ya kifo chake kamwe sio vielelezo vya kumtawaza Abu Bakar. Na hii haiwezi kuchukuliwa kuwa ni dokezo la kiongozi wa umma anaefaa, kwani Abu Bakar si mtu wa kwanza kuamrishwa kuongoza Swala, kama tulivyoeleza ni kwamba ilikuwa ni tabia ya Mtume (s.a.w.w.) kumuacha mtu wa kuongoza baadhi ya mambo pindi anaposafiri.  Na hata pale Umar alipopigwa panga alimteua Suhaib ibn Sinan kuongoza Swala na wala yeye hakuwa Khalifa baada yake, bali alikuwa Uthman, hii inamaana uongozi wa Swala ni jambo jingine na uongozi wa dola ni jambo jingine.

# UCHAGUZI WA KHALIFA WA KWANZA

Kuhusiana na tukio la kuchaguliwa Khalifa wa kwanza wameandika yafuatayo:

> "Mara tu baada ya habari za kutawafu kwa Mtume (s.a.w.) zilipoenea Masahaba ambao ni wajumbe wa Shura wakati wa uhai wa Mtume walisahau wajibu wao wa kudhibiti pengo lililojitokeza, hali hii ikatoa nafasi kwa Waislamu miongoni mwa Ansari kukutana katika ukumbi ulioitwa Saqifa Bani Saidah na kuanza kuzungumzia uongozi."[2]

Katika kipengele hiki wameeleza kuwepo wajumbe wa Shura wakati wa uhai wa Mtume (s.a.w.w.), tunaloweza kusema ni kwamba, ni kweli Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akiwashauri baadhi ya Maswahaba wake katika baadhi ya mambo, na si katika kila kitu, na wala hakukuwa na watu maalumu aliokuwa akishauriana nao, bali ushauri wake ulikuwa ni kwa mujibu wa watu waliokuwepo katika tukio fulani, kama vile alivyowashauri Maswahaba wale tu waliokuwepo katika uwanja wa vita, kama vile katika vita vya Khandaki na vyenginevyo, ama dai la kuwepo watu maalumu waliojulikana kama wajumbe wa Shura ni dai ambalo halina mashiko.

Na wajibu mkubwa uliokuwa ukiwakabili Maswahaba wakati huo, ulikuwa ni kuishughulikia maiti ya Mtume (s.a.w.w.) kwa kumuosha, kumvisha sanda, kumswalia na hatimaye kumzika, lakini kama walivyoeleza ni kwamba, mara baada ya kifo hicho cha Mtume (s.a.w.w.) Maanswari walikusanyika kwa lengo la kujadiliana juu ya suala la uongozi, na Muhajirina watatu (Abu Bakar, Umar

[2] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.320.

na Abu Ubaida al-Jarrah) walipopata habari juu ya kufanyika kikao katika ukumbi wa Saqifa nao walijiunga katika kikao hicho, na kuacha wajibu wao wa kuishughulikia maiti ya Mtume (s.a.w.w.), kama wanavyosema:

> "Umar na Abubakar walipopata taarifa hii nao wakaenda kujiunga katika ukumbi huo, halikadhalika pia walikuwepo Abu Ubaida Al-Jarrah nakadhalika; lakini wakati huo huo Bani Hashim nao walikuwa wanakutana katika nyumba ya Fatma kuzungumzia Ukhalifa."[3]

Ama kuhusiana na uongozi baada ya Mtume (s.a.w.w.), ni kwamba ilikuwa ni jambo ambalo Mtume (s.a.w.w.) alikwishalibainisha na kuwabainisha wale wanaostahiki nafasi hiyo, kama ilivyokuja katika Riwaya mbalimbali ambazo tutazitaja katika kurasa za mbele.

Kudaiwa kwamba Bani Hashim nao walikaa katika nyumba ya Bibi Fatma (a.s.) kujadili suala la Ukhalifa, hili ni dai ambalo halikubaliki, tunalopenda kuwafahamisha watu hasa wanafunzi wenzangu wanaosomeshwa au wale wanaojisomea kitabu hicho (Elimu ya Dini ya Kiislamu, Kitabu cha Nne), ni kwamba dai hili si sahihi, na ni jambo ambalo halifanywi na mtu yeyote mwenye akili timamu, haiwezekani kwa watu kufiliwa na mpenzi wao wa dhati wauwache mwili wake pasi na kuufanyia yale yaliyowajibu, na badala yake waanze kujadili uongozi, hasa ikizingatiwa mtu mwenyewe akiwa ni mbora wa viumbe vyote. Ukweli ni kwamba wakati ilipokuwa harakati za kugombania madaraka zikiendelea watu wa ukoo wa Hashim (Bani Hashim) walikuwa wakiushughulikia mwili mtukufu wa Mtume (s.a.w.w.) kwa kuuosha, kuuvisha sanda na hatimaye kuuzika, kwa hivyo kulikuwa na matukio mawili tofauti yaliokuwa yakifanyika wakati mmoja: Kugombania madaraka na kuutayarisha

[3] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.320.

mwili wa Mtume Mtukufu (s.a.w.w.), na haya ameyaeleza mwanachuoni maarufu wa Afrika Mashariki, Sheikh Abdullah Saleh Farsy kwa kusema:

> "Muda huu walipokuwa wanachagua Khalifa, Sayyidna Ali na jamaa zake walikuwa katika kazi ya kumwosha Mtume. Mtume alipakatwa na Bwana Al-Fadhil bin Abbas bin Abdul Muttalib; akaoshwa na Sayyidna Ali bin Abi Talib bin Abdul Muttalib; na aliyekuwa akitilia maji ni Bwana Abbas bin Abdul Muttalib, ama mahuru wake Mtume wawili- Bwana Usama bin Zayd na Bwana Shakran- wao walikuwa wakiwasaidia. Baada ya kuoshwa lilichimbwa Kaburi huko huko chumbani alikokufa- chumba cha Bibi Aysha- na aliyesimama kutengeneza hilo Kaburi na kulititilia mwanandani ni Bwana Abu Talha wa Kiansar. Baada ya hapa wakamvua nguo za kuoshea, wakamkafini kwa nguo tatu nyeupe za pamba baada ya kufukizwa udi vyema na kutiwa manukatovizuri. Kisha akalazwa juu ya kitanda kwenye ukingo wa kaburi akafunikwa Guo moja kwa moja. Baadaye wakapewa ruhusa watu kuingia kumuaga Mtume wao. Yakawa makundi haya yanaingia na haya yanatoka, mchana kutwa na Jumatatu na mchana kutwa wa Jumanne na usiku kucha wa kuamkia Jumatano. Hata karibu na alfajiri ya hii Jumatano, Mtume alishushwa kaburini mwake; akazikwa kama wanavyozikwa Waislamu wote wengine. Walioshuka kaburini siku hiyo ni: Bwana Abbas, Sayyidna Ali na mabwana hawa wengineo wajao: Al Fadhil bin Abbas, Qutham bin Abbas na Shakran."[4]

Bila ya shaka kwa mujibu wa maneno haya ya Sheikh Abdullah yanathibitisha kwamba, wale waliokuwa katika ukumbi wa Saqifa Bani Saida hawakuhudhuria mazishi ya Mtume (s.a.w.w.) wakiwemo hao walioshika Ukhalifa baada yake! Bali walishughulishwa mno na kujitafutia madaraka!

[4] Maisha ya Nabii Muhammad (s.a.w); cha Sheikh Abdallah Farsy, Uk.81.

Ama watu wa ukoo wa Hashim kukaa katika nyumba ya Bibi Fatma (a.s.), ni kwamba wao walikaa kikao, lakini kikao hicho kilikuwa ni kujadili namna walivyonyang'anywa haki yao, kama ilivyothibiti katika Hadithi mbalimbali za Mtume (s.a.w.w.), kama tutakavyozibainisha, na kuzungumzia hatua za kuchukua, na pia walionesha masikitiko yao ya kufanywa mashauri hayo bila ya wao kushirikishwa, na baya zaidi kufanyika katika wakati ambao wao walikuwa wakiutayarisha mwili Mtukufu wa Mtume (s.a.w.w.)

# HALI ILIVYOKUWA KATIKA MKUTANO

Katika kinyang'anyiro hicho cha kuwania madaraka, hali haikuwa shwari, kwani kila upande ulikuwa ukivutia kwake, wanasema:

> "Mjadala mrefu ulipita, wapo waliotaka Khalifa atoke upande wa Ansar, wapo waliotaka ukhalifa utoke upande wa Muhajirina, wapo waliopendekeza kuwa Khalifa na naibu wake hatimaye walikubaliana pawe na Khalifa mmoja ndipo Abubakar akampendekeza Umar upande wa Muhajirina na Saad Ubaida upande wa Ansar. Wote kwa pamoja (Umar na Saad) wakasema katika jambo hili hatuwezi badala yako.
>
> Baada ya kauli hii Umar hakuchelewa akampendekeza Abubakar na kumpa mkono na ahadi ya utii. Ndipo wote waliokuwepo wakampa Abubakar mkono wa ahadi ya utii na hivyo Abubakar kuchaguliwa na wengi kuwa Khalifa wa kwanza wa Dola ya Kiislamu. Siku ya pili jambo hili lilipelekwa msikitini na wale ambao walikuwa hawajafanya hivyo walimpa ahadi ya mkono wa utii msikitini humo humo. Karibu watu thelathini na tatu elfu walichukua ahadi na kumpa mkono wa ahadi ya utiii ndani ya msikiti. Lakini Ali aliendelea na kikao chake hakuwepo mkutanoni, na alichukua miezi kabla ya kumpa Khalifa ahadi ya utii na kutambua Ukhalifa wake."[5]

Katika maneno haya kuna vipengele vingi, lakini ambacho tutakijadili, ni maneno yao kwamba Abu Bakar alimpendekeza Umar upande wa Muhajirina na Sa'd bin Ubada upande wa Ansar, na wote

[5] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.320-321.

kwa pamoja (Umar na Sa'd) wakasema katika jambo hili hatuwezi badala yako.

Usahihi wa mambo ni kwamba Abu Bakar hakumpendekeza Sa'd, bali alimpendekeza Umar na Abu Ubada ibn Jarrah, ambao ni Muhajirina wenzake,[6] kwani mikakati yao ilikuwa nafasi hiyo isiende kwa wasiokuwa Muhajirina, na hivi ndivyo ilivyofanyika, kwani hakuna Khalifa hata mmoja aliyetokana na Maanswari.

Ama kuhusiana na hoja kwamba Imamu Ali (a.s.) alichukua muda mrefu kabla ya kumpa Khalifa (Abubakar) ahadi ya utii wa kutambua Ukhalifa wake. Ukweli ni kwamba Imamu Ali a.s. hakuutambua Ukhalifa wa Abu Bakar, kama vile ambavyo mke wake (Bibi Fatima a.s.) alivyokuwa hakuutambua na alikufa katika hali hiyo. Alichokifanya Imamu Ali a.s. ni kutoa ushauri kwa Abu Bakar pale alipomuomba ushauri, kwani Mtume (s.a.w.w.) amesisitiza juu ya kumpa ushauri wa ukweli yule mwenye kutaka ushauri. Lau kama Imamu Ali (a.s.) angejizuia kutoa ushauri, jambo hili lingetoa nafasi kwa maadui wa Uislamu kuushambulia na hatimaye kuumaliza, hasa ikizingatiwa kwamba Dola ya Kiislamu ilikuwa imezungukwa na maadui waliokuwa na nguvu kubwa za kijeshi, kama vile dola ya Kirumi na Kifursi. Kwa maelezo zaidi juu ya hoja hii unaweza kurejea kitabu *'Ali Ibn Abi Talib (a.s.) na baiyah'* cha Allamah Sayyid Said Akhtar Rizvi

Tumeeleza kwamba Imamu Ali (a.s.) hakuthubutu kukaa kikao cha kujadili uongozi pale ambapo wengine walipokuwa wakijadili jambo hilo katika ukumbi wa Saqifa, bali alikuwa katika harakati za kumuosha Mtume (s.a.w.w.). Na pia nawaomba wanafunzi wenzangu wapendwa, wafahamu kwamba, Sa'd ibn Ubada ambaye alikuwa kiongozi wa Maanswari hakumbayi Abu Bakar (hakuutambua Ukhalifa wake), na alitishiwa maisha yake, na Umar mwe-

[6] *Sahih Bukhar*, Jz. 8, Uk. 27. *Tarikh Madinat Dimishqi*, Jz. 3, Uk. 279.

nyewe anasema kwamba: "Tulimrukia Sa'd." Basi msemaji miongoni mwao akasema: "Munamuua Sa'd ibn Ubada! Umar akasema: "Mwenyezi Mungu amuuwe."[7]

Kwa kweli siku hiyo ilikuwa ni nzito kwa Sa'd ibn Ubada pamoja na wale wote waliokataa kumtambua Abu Bakar akiwemo mtoto wa Sa'd, Imamu Ali (a.s.) Zubeir, Abbas, Bani Hashim na baadhi ya Maswahaba, kwani waliona haki hiyo ya Ukhalifa ni ya Ahlul-Bayt(a.s.), na pale walipojikusanya katika nyumba ya Imamu Ali (a.s.) kujadili hali iliyotokea walitishiwa kuchomwa moto![8]

Wanaendelea kusema:

> "Wapo waliodai kuwa aliathiriwa sana na kifo cha Mtume na alishughulishwa sana na mazishi."[9]

Maneno haya si madai, bali ni ukweli uliowazi kabisa, kwamba Imamu Ali (a.s.) aliathiriwa sana na kifo cha Mtume (s.a.w.w.) ambaye alikuwa mtoto wa ami yake, mkwe wake na babu wa watoto wake. Lakini si hivyo tu alidhani kwamba Waislamu watakuwa ni wenye kuyatii maneno ya Mtume wao, pale alipowabainishia kwa uwazi kwamba haki ya uongozi ni ya Ahlul-Bayt(a.s.) ikianzia kwa Imamu Ali (a.s.), na hata pale Abbas alipomtaka anyooshe mkono wake ili ampe mkono wa utiifu wa kumtambua kwamba yeye ndiye Khalifa baada ya Mtume (s.a.w.w.), Imamu Ali (a.s.) alimuuliza ammi yake huyo: "Je, kuna mtu mwengine anayelitafuta jambo hili asiyekuwa sisi?"[10]

---

[7] *Sahih Bukhar*, Jz. 8, Uk. 542 na Jz. 5, Uk. 14.

[8] Tukio hili la kutishiwa kuchomwa nyumba ya bibi Fatima ((a.s.)) ni mashuhuri, kwani limenakiliwa na Ibn Qutayba katika *al-Imama Wassiyasa*: Jz. 1, Uk. 11-12, At-Tabariy katika *Tarikhul-Tabari*: Jz. 3, Uk. 202, Dhahabiy katika *Muruju Dhahabiy*: Jz. 1, Uk. 414, Ibnul Hadidi Katika *Sharhu Nahjul Balaghah*: Jz. 1, Uk. 34.

[9] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk. 321.

[10] Ibn Qutayba, *al-Imama Wassiyasa*: Jz. 1, Uk. 12.

Wanaendelea kusema:

> "Katika tukio hili tunaona msingi wa Uislamu ambao tumeshauweleza ulivyofuatwa katika kupata kiongozi kama ilivyo msikitini waumini wanavyomchagua Imamu wao, basi kitaifa ni hivyo hivyo."[11]

Kila mwenye kuyasoma maelezo yaliyotangulia namna Khalifa wa Kwanza alivyopatikana, itambainikia wazi kwamba kana kwamba Uislamu hauna utaratibu bora wa kumpata Khalifa, kiasi cha kupelekea Maswahaba wakubwa kutoushughulikia mwili wa Mtukufu wa Mtume (s.a.w.w.) na badala yake kujiingiza katika kinyang'anyiro cha kuwania uongozi. Pia ikiangaliwa namna makundi ya Waislamu yaliyokuwepo wakati huo, ni kwamba baadhi ya makundi yalikosa uwakilishi katika mkutano wa Saqifa Bani Saida, Waislamu wa Kianswari baada ya kupata habari ya kifo cha Mtume (s.a.w.w.) walikimbilia katika ukumbi wao na kukusanyika ili kuchagua kiongozi. Abu Bakar, Umar pamoja na Abu Ubayda al-Jarrah ambao ni Muhajirina, na wao waliposikia kwamba Maanswari wamekusanyika kwa lengo hilo nao walijiunga nao, bila ya kuwapasha wenzao habari, ama kwa upande wa Bani Hashim, hakuna yeyote aliyeshiriki, kwani wao walikuwa na shughuli ya kutayarisha maziko ya Mtume (s.a.w.w.)

Kwa kweli ni jambo la aibu kuambiwa kwamba namna hii na hasa ikizingatiwa hali ilivyokuwa ukumbini, kwamba ni moja kati ya misingi ya kumpata kiongozi katika Uislamu! Leo tunashuhudia taratibu za kistaarabu zisizo na mizozo na uhasama katika nchi mbalimbli namna wanavyowapata viongozi iwapo kutatokea pengo lolote la uongozi. Basi ni kwa nini palitokea hayo yaliyotokea katika umma huu ambao ni umma bora, je ni kweli Mtume (s.a.w.w.) hakuelekeza juu ya kumpata kiongozi wa dola pale atakapofariki dunia, je si Mtume huyo huyo aliyekuwa akimuainisha mtu kushika

[11] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.321.

nafasi yake pale alipokuwa akiondoka katika mji wa Madina, mji ambo ulikuwa ndio makao makuu ya dola ya Kiislamu?

Uislamu umeweka utaratibu mzuri zaidi wa namna ya kumpata kiongozi, na hayo ameyafanya Mtume wetu (s.a.w.w.) kama walivyofanya Mitume waliotangulia, kwa mfano Nabii Musa (a.s.) alipohitajiwa na MolaWake kwenda kujitayarisha kwa ajili ya kwenda kupokea sheria za Mwenyezi Mungu, alimuacha mdogo wake ambaye ni Nabii Harun(a.s.) ili ashike nafasi yake ya kuwaongoza watu, hakuondoka hivi hivi kwa kutarajia kwamba wao watajichagulia kiongozi wanayemtaka, Mwenyezi Mungu amelieleza jambo hili kwa kusema:

وَوَاعَدْنَا مُوسَى ثَلَاثِينَ لَيْلَةً وَأَتْمَمْنَاهَا بِعَشْرٍ فَتَمَّ مِيقَاتُ رَبِّهِ أَرْبَعِينَ لَيْلَةً وَقَالَ مُوسَى لِأَخِيهِ هَارُونَ اخْلُفْنِي فِي قَوْمِي وَأَصْلِحْ وَلَا تَتَّبِعْ سَبِيلَ الْمُفْسِدِينَ

**"Na tulimwahidi Musa masiku thalathini na tukayatimiza kwa kumi; ndipo ikatimia miadi ya Mola Wake siku arubaini. Na Nabii Musa akamwambia ndugu yake Harun: Shika mahali pangu katika watu wangu na utengeneze wala usifuate njia ya mafisadi." (Qur'ani, 7:142)**.

Tukiangalia muda alioghibu Nabii Musa kwa watu wake ni siku arobaini tu, lakini ndani ya siku hizo alimteua kiongozi wa kushika mahala pake, tena mtu huyo ni ndugu yake. Basi kwa nini mnayafananisha madhehebu ya Kishia na Uyahudi na Ukrtisto kwa sababu wanaamini Khalifa baada ya Mtume (s.a.w.w.) ni ndugu yake, basi ikiwa ni Uyahudi huu aliokuja nao Nabii Musa na iwe hivyo na tunaupokea kwa mikono miwili.

Wanaendelea kusema:

> "Pengine pia hapa ni mahala pekee kuondoa yale mawazo yasiyo sahihi kuwa Umar ndiye aliyepelekea Abubakar awe Khalifa, hivyo kusingiziwa tukio la karatasi n.k. Hili si sahihi. Abubar amepewa Ofisi ya ukhalifa sio kwa sababu yoyote zaidi ya kuwa ndiye aliyestahili kwa wakati ule."[12]

Ni ukweli usio pingika kwamba Umar alitoa mchango mkubwa wa kufanikisha Abu Bakar kushika ofisi ya utawala, na hili halina mafungamano yoyote na tukio la karatasi lililothibiti kutokea kwake licha ya waandishi wa kitabu hicho (Elimu ya Dini ya Kiislamu) kudai kutokusihi kutokea kwake, haya yanadhihirika namna idara hiyo ya uongozi ilivyokuwa ikiendeshwa, na pia Abu Bakar kudiriki kumuusia Ukhalifa Umar baada yake, jambo ambalo linakwenda kinyume na namna yeye alivyochaguliwa, alifanya hivyo ikiwa ni tunzo kwake, kwani alikuwa ni mmoja wa Wahajirina watatu walioshiriki katika ukumbi wa Bani Saida na kumfanikisha kutwaa madaraka. Muhammad Abdalla Riday anaeleza hali ilivyo katika ukumbi wa Saqifa na mchango alioutoa Umar kwa Abu Bakar:

> "Baada ya maneno machache aliyoyasema Abubakar, kisha akainuka mtu mmoja katika Ansaar, akasema: 'Sisi tutakuwa na amiri na nyinyi muwe na amiri wenu, enyi Makurayshi.' Baada ya kukaa huyo Ansaari, kukawa kuna maneno mengi na sauti zikainuka juu ya maneno ya utesi baina ya Ansaari na Muhajirina, mpaka kukahofiwa kutokea fujo baina ya makundi mawili hayo. Sayyidna Umar alipoona hatari hiyo ya utesi mara akamwambia Abu Bakar, nyoosha mkono wako nikupe kiapo changu cha utii( ahadi ya kumchagua mtu kuwa kiongozi wa umma au kundi la watu. Huwa si kwa kumpa mkono tu, bali pia na kutamka ahadi zako za utiifu kwake). Kwa hivyo Abubakar alinyoosha mkono

[12] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.321.

> na wa kwanza kumpa kiapo cha utii alikuwa ni yeye Umar, kisha Muhajirina wakampa kiapo cha utii kisha wakafuata Ansaar (Radhi za Mwenyezi Mungu ziwashukie wote). Hiyo ilikuwa hikma nzuri na ya upesi aliyoifanya Sayyidna Umar, kama hakufanya hivyo, bila shaka pangetokea utesi baina ya Muhajirina na Ansaar."[13]

Ndugu zangu hiyo shura inayotetewa iko wapi?!

Sasa msikie Umar mwenyewe anavyoielezea hali iliyopelekea kuchaguliwa Abu Bakar, anasema:

> "Hakika kubaiwa (kuteuliwa kuwa Khalifa) kwa Abu Bakar ilikuwa ni jambo la kushitukizia, lakini Mwenyezi Mungu aliikinga shari yake, basi atakayerudia kama hivyo muuweni."[14]

Si dhani kwamba mna shaka yoyote juu ya kauli ya Khalifa Umar, hasa ikizingatiwa kwamba yeye ni Farruq.  Basi hapa ametupambanulia haki na batili, ukweli na mapindisho ya ukweli. Amekiri kwa ulimi wake kwamba kuchaguliwa kwa Abu Bakar lilikuwa si jambo lililopangwa na watu kushauriana.[15]Ama kuhusianana mchango wake mwengine, ni kwamba ulianzia pale alipokataa kumpelekea Mtume (s.a.w.w.) wino na kalamu ili aandike usia wake kwa madai kwamba Mtume (s.a.w.w.) anaweweseka! Na tukio hili si la kubuniwa bali ni tukio lililotokea katika historia ya maisha ya Mtume (s.a.w.w.) na kunakiliwa na vitabu sahihi vya Hadithi, zaidi tutalielezea huko mbele.

Mchango mwengine alioutoa ni pale Mtume alipofariki, alitangaza kwamba Mtume hajafariki na kuwatishia kuwakata mikono na miguu ya kila ambaye anadai kwamba Mtume (s.a.w.w.) alishafari-

[13] Kitabu "Masahaba Kumi Waliobashiriwa Pepo," Uk. 11-12.
[14] Al-Ya'qubiy, *Tarikhul Ya'qubiy*: Jz. 2, Uk. 158
[15] *Sahihul Bukhariy*: Kitabul Muharibina min Ahlil Kufri Warridah, Jz. 8, Uk. 18.

ki.[16] Hiyo ni kwa sababu Abu Bakar hakuwepo katika Mji wa Madina, na baada ya kuwasili alikiri kwamba kweli Mtume amefariki.

Mchango mwengine mkubwa alioutoa, ni pale walipopata habari ya kukusanyika kwa Maanswari katika ukumbi wa Saqifa kwa lengo la kumchagua mtu ambaye atashika Ukhalifa, Umar alimpasha habari rafiki yake huyo, na huko aliweza kupambana dhidi ya Maanswari na mwisho akafanikiwa kumtawalisha Abu Bakar, na kuwatishia wale waliokataa kutoa viapo vyao vya utiifu kwa Abu Bakar, kiasi ambacho alifikia kutishia kuichoma moto nyumba ya Imamu Ali (a.s.) ambapo ndani yake walikusanyika Maswahaba waliopinga uteuzi wa Abu Bakar![17] Baada ya hapo kitabu hicho kimeandika baadhi ya mambo yaliopelekea usahihi wa Ukhalifa wake, mambo hayo ni kama kama yafuatavyo:

> "Kwanza alikuwa na sifa zote za kuwa kiongozi wa dola kama zilivyotajwa katika kitabu hiki sehemu ya siasa na uendeshaji wa dola katika Uislamu."[18]

Kuhusiana na sifa za uongozi, ni kwamba Qur'ani Tukufu ambayo Mwenyezi Mungu anaisifu kwa kusema:

مَا فَرَّطْنَا فِي الْكِتَابِ مِنْ شَيْءٍ

**"Hatukupuuza kitu katika Kitabu." (Qur'ani,6:38)**.

Sidhani kwamba kuna Mwislamu anafikiri kwamba Qur'ani imeghafilika na jambo hili lililo na umuhimu wa kipekee katika Uislamu, kwani kwa kutowekewa misingi madhubuti, natija yake ni

[16] *Tarikh Tabariy*: Jz.2, Uk. 66
[17] Al-Imama wassiyasa: J.1,Uk.19.
[18] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.321.

kumwagwa damu za watu wasio na hatia, na umwagaji wa damu nyingi za Waislamu zilizomwagwa kutokana na watu kwenda kinyume na taratibu zilizowekwa na Uislamu katika kumpata kiongozi, na fitina kubwa ikaingia kati yao, kiasi ya kuathiri katika zama zote, mpaka kufikia katika zama zetu hizi. Na kama kweli alikuwa na sifa zote za kuwa kiongozi, ni kwanini ifikie wakati ajutie kuwa Khalifa? Bila ya shaka majuto ni natija ya mtu kuhisi kwamba hakufanya yale yaliyokuwa anastahiki kuyafanya:[19]

> "Pili ni kuwa Abubakar alikuwa karibu zaidi na Mtume pengine kuliko swahaba yoyote. Hili linadhihirika zaidi katika msimamo wake wa kufuata hatua kwa hatua kila ambalo Mtume (s.a.w.) amelifanya au kuliruhusu katika uhai wake alipo endesha Dola ya Kiislamu. Usahibu wa Mtume na Abubakar umetajwa katika Qur'an na hivyo Abubakar kutajwa kwenye Qur'an wakati wa Hijra kama ilivyo katika sura (9:40).

إِلَّا تَنْصُرُوهُ فَقَدْ نَصَرَهُ اللَّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ الَّذِينَ كَفَرُوا ثَانِيَ اثْنَيْنِ إِذْ هُمَا فِي الْغَارِ إِذْ يَقُولُ لِصَاحِبِهِ لَا تَحْزَنْ إِنَّ اللَّهَ مَعَنَا فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَيْهِ وَأَيَّدَهُ بِجُنُودٍ لَمْ تَرَوْهَا وَجَعَلَ كَلِمَةَ الَّذِينَ كَفَرُوا السُّفْلَى وَكَلِمَةُ اللَّهِ هِيَ الْعُلْيَا وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ

> ''Kama hamtamnusuru (Mtume), basi Mwenyezi Mungu alimnusuru walipomtoa wale walio kufuru, alipokuwa (Mmoja tu

[19] "Si sikitikii chochote katika dunia isipokuwa juu ya mambo matatu niliyoyafanya, ningependa lau kama sikuyafanya…, ningependa lau kama sikuikashifu nyumba ya Fatima kwa lolote lile, ningependa lau kama sikumchoma moto al-Fuj-at Assulamiy, badala yake ningemuua au kumuacha huru, ningetamani lau kama mimi katika siku ya Saqifa Bani Saida ningeliweka jambo (Ukhalifa) katika shingo ya mmoja wa watu wawili (anamkusudia Umar na Abu Ubada), mmoja wao akawa amiri (Khalifa) na mimi nikawa waziri."(Ibn Asaki,Tarikh Madinatu Dimishqi: Jz.30, Uk.419)

> na Mwenziwe) wa pili yake, (peke yao) alipomwambia sahib yake; ‘’Usihuzunike kwa yakini Mwenyezi Mungu yupamoja nasi, Mwenyezi Mungu akamteremshia utulivu wake, na akamnusuru kwa majeshi msiyoyaona, akafanya neno la wale waliokufuru kuwa chini; na neno la Mwenyezi Mungu ndilo la juu. Na Mwenyezi Mungu Ndiye anayeshinda na Ndiye mwenye Hikima.’’ (9:40).[20]

Kwa hakika sifa ya Uswahaba ni sifa wanayosifiwa nayo wale wote waliomuona Mtume (s.a.w.w.) na kumuamini na kufa katika imani hiyo, ama kuhusisha usuhuba maalumu kwa Abu Bakar juu ya Mtume (s.a.w.w.) kwa ushahidi wa Aya hii (9:40), na kuonekana ana sifa za kipekee, nadhani inatokana na kutoeleweka vyema makusudio ya Aya.

Wafasiri wanaeleza kwamba Aya hii ilitereremka wakati Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa akihama kutoka Makka na kuelekea Madina, alikuwa pamoja na Swahaba wake katika pango, ambaye alikuwa ni Abu Bakar. Kwa mujibu wa Aya hii, inaonesha kwamba Abu Bakar alishikwa na huzuni ambayo hakutakiwa kuwa na huzuni ya aina hiyo, ndiyo maana Mtume (s.a.w.w.) akamkataza kwa kumwambia: ‘’Usihuzunike kwa yakini Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi.” Na si hivyo tu pale nusra ya Mwenyezi Mungu na utulivu Wake, viwili hivyo vilimshukia Mtume (s.a.w.w.) peke yake, kama inavyosema: “Mwenyezi Mungu akamteremshia utulivu Wake, na akammnusuru kwa majeshi msiyoyaona.”

Na kama sifa ya ukuruba kwa Mtume (s.a.w.w.) ni sababu ya mtu kuwa Khalifa, basi ni kwa nini inaponasibishwa kwa Imamu Ali (a.s.) ionekane ni kioja kwa wale wanaosema haki ya uongozi ni haki ya wanafamilia ya Mtume (s.a.w.w.).

---

[20] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.321.

> "Sihivyo tu, lakini Abu Bakar ndiye aliyekuwa Imamu aliyeteuliwa na Mtume (s.a.w.) kuendesha swala alipokuwa anaumwa karibu na siku za kutawafu kwake baada ya Hija yake ya kwanza na ya mwisho (Al-Hijjatul wadah). Dr. Majid Ali Khan katika kitabu chake The Pious Caliphs of Islam Abubakar; anaeleza tukio linaloonesha nafasi ya Abubakar ilivyokuwa ni ya kuhesabiwa mbele ya Mtume wa Waislamu kwa jumla. Katika siku hizo ambazo Abubakar ndiye aliyeteuliwa kuwa Imamu ilitokea kuwa Abubakar hakuwepo wakati wa swala ya jamaa. Mtume aliposikia sauti isiyokuwa ya Abubakar (aliyeswalisha alikuwa Umar Ibn Khattwab) aliuliza juu ya Imam (Abubakar) ambaye hakuwepo. Mtume hakupendezewa na akasema. ''Asiswalishe mtu mwengine ila Abu Qahafa (Abubakar). Baada ya hapo akaitwa Abubakar lakini wakati huo Imamu alikwisha maliza swala. Mtume aliamuru swala ile irudiwe na ikaswalishwa na Abubakar. Abubakar alikuwa mtu mashuhuri anayekubalika, anayejiamini, mtaratibu, mwenye istiqama, ikhlaswi, mpevu wa uoni na mwenye uamuzi na mfuasi wa nyayo za Mtume (s.a.w.). Yote haya ukiyachanganya na umri, kwa wale waliokuwa kwenye ukumbi wa mkutano, Abubakar ndiye aliyewazidi kiumri, hivyo kuchaguliwa kwa Abubakar kulitokana na kuwa na uwezo wa sifa za kuwa Khalifa. Kwa maelezo haya, kutupilia mbali madai ya ukoo wa Hashim ilikuwa lazima."[21]

Suala la Abu Bakar kuteuliwa kuwa imamu wa kuongoza Swala, ni jambo ambalo hata wale waandishi wa kitabu hicho (Elimu ya Dini ya Kiislamu) wameeleza bayana kwamba hii si sababu ya wazi ya kumfanya kuwa Khalifa. Bila ya shaka hoja yao hii ni sahihi, hasa ikizingatiwa kwamba ilikuwa ni tabia ya Mtume (s.a.w.w.) kumtea mtu atakayeshika nafasi ya kuongoza Swala pale alipokuwa akiondoka kutoka katika mji wa Madina. Na hata pale Khalifa Umar alipopigwa panga alimteua Suhaib ibn Sinan kuwa imamu wa kuongoza Swala, na mwishowe Ukhalifa ukashikwa na Uthman, na

[21] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.321-322.

hakuna yeyote aliyemfikiria mteuliwa wa uimamu wa Swala (Suhaib) kuwa Khalifa baada ya Umar. Hoja hii ikiwa ni kweli imesihi kwamba Mtume (s.a.w.w.) alimteua Abu Bakar kuwa Khalifa. Na ikiwa kwamba ni kweli Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha Swala iliyoswalishwa na Umar irudiwe na iswalishwe na Abu Bakar, basi ifahamike kwamba hoja hii inamshusha chini sana Khalifa Umar ambaye inadaiwa kwamba rai yake ilikuwa inawafikiana na Qur'ani! Kwani haiwezekani Abu Bakar akapata sifa nzuri bila ya wengine kushushwa?

Ama kuhusiana na suala zima za uendeshaji wake wa Dola na sifa mbalimbali walizozieleza hapa, ni vyema tumsikilize Abu Bakar mwenyewe maneno aliyoyasema baada ya kusifiwa kwa sifa mbalimbali, kwani kukiri ni ushahidi usio na shaka, amesema:

"Si sikitikii chochote katika dunia isipokuwa juu ya mambo matatu niliyoyafanya, ningependa lau kama sikuyafanya…,ningependa lau kama sikuikashifu nyumba ya Fatima kwa lolote lile, ningependa lau kama sikumchoma moto al-Fuj-at Assulamiy, badala yake ningemuua au kumuacha huru, ningetamani lau kama mimi katika siku ya Saqifa Bani Saida ningeliweka jambo (Ukhalifa) katika shingo ya mmoja wa watu wawili (anamkusudia Umar na Abu Ubada), mmoja wao akawa amiri (Khalifa) na mimi nikawa waziri. "[22]

Bila ya shaka Abu Bakar alikuwa na haki ya kujuta na kulia kutokana na mambo ambayo yeye mwenyewe anakiri kuyatenda, alitambua kwamba mwanadamu hana haki ya kumwadhibu mwanadamu mwenzake kwa adhabu ya kumchoma moto. Alitambua vyema nafasi ya watu wa nyumba ya Mtume (s.a.w.w.) licha ya kwamba alipeleka kikosi cha watu katika nyumba ya Binti wa Mtume (s.a.w.w.) na kuikashifu, kwa vile ndani yake kulikuwa na watu waliokataa kutoa mkono wa utiifu kwa Abu Bakar, kiongozi wa operesheni hiyo

[22] Ibn Asakir, *Tarikh Madinatu Dimishqi*: Jz. 30, Uk. 419

alikwenda na kijinga cha moto kwa lengo la kuichoma, mtu mmoja alimtanababahisha kwamba ndani ya nyumba hiyo yumo Fatima (a.s.), hata hivyo alijibu: 'Hata kama yumo nitaichoma!' Si hivyo tu, Binti huyo alinyimwa mirathi yake na haki zake mbalimbali za msingi, kwa hoja kwamba eti Mtume harithiwi. Kutokana na dhulma hizi Bibi Fatima aliamua kumsusa Abu Bakar pamoja na waziri wake, Umar, na alifariki dunia akiwa katika hali hii. Abu Bakar alilijutia sana tendo hili kwa vile alitambua heshima ya Mtume (s.a.w.w.) hupatikana kwa kuwaheshimu Ahlul-Bayt wake, anasema Abu Bakar:

ارقبوا محدا صلى الله عليه وسلم في أهل بيته.

"Mchungeni (muheshimuni) Muhammad (s.a.w.w.) kwa kupitia (kuwaheshimu) watu wake."[23]

Abu Bakar alijutia kuikashifu nyumba ya Binti wa Mtume (s.a.w.w.) kwa vile alijua uzito wa jambo hilo, kwani alimsikia Mtume (s.a.w.w.) akisema:

فاطمة بضعة مني فمن أغضبها أغضبني.

"Fatima ni sehemu ya mwili wangu, basi mwenye kumkasirisha atakuwa amenikasirisha mimi."[24]

Ama kuhusiana na suala la Ukhalifa ambalo wapenzi wa Abu Bakar hulitolea hoja za kudhania, na kumuona adui kila ambaye anamawazo hasi, kutokusihi Ukhalifa wake kwa vile Mtume (s.a.w.w.) alikwisha wateuwa wale wanaostahiki kushika nafasi hiyo, mwenyewe anaeleza kinagaubaga kwamba anajutia nafasi hiyo na ange-

[23] Ibn Hajar, *Fat-hul Baariy*, Babu Manaqibu Qarabatu Rasuli llahi (s.a.w.w): Jz.7, Uk. 63.
[24] *Sahihul Bukhariy*, Babu Manaqibul Muhajirina wafadhlihim: Jz.4, Uk.210.

tamani nafasi hiyo angempa mmoja kati ya wasaidizi wake (Umar au Abu Ubada). Ametambua wazi kwamba nafasi hiyo imemsababishia kutenda yale yasiofaa katika sheria ya Kiislamu, kama alivyoyabainisha mwenyewe (kumchoma mtu moto na kuikashifu nyumba ya Bibi Fatima binti wa Mtume (s.a.w.w.).

Ama kuhusiana na umri, ni kwamba jambo hili halina nafasi yoyote katika Uislamu, kwani Mwenyezi Mungu aliwapa baadhi ya watu vyeo vya Utume wakiwa na umri mdogo sana, kama vile Nabii Isa na Nabii Yahya (a.s.) licha ya kuwepo watu waliokuwa na umri mkubwa zaidi ya wao. Pia Nabii Musa (a.s.) alikuwa ni Mtume Mtukufu zaidi ikilinganishwa na Nabii Harun, licha ya kwamba alikuwa mdogo kiumri ikilinganishwa na Nabii Harun (a.s.) Hata hivyo, Sa'd ibn Ubada alikuwa na umri mkubwa zaidi kuliko Abu Bakar, lakini alinyimwa nafasi hiyo, na pia zama hizo baba wa Abu Bakar alikuwa hai, lakini hakuna aliyemfikiria kumpa Ukhalifa.

Pengine huenda suala la umri mkubwa wa Abu Bakar limemsababishia kutokuwa na maamuzi thabiti katika mambo yanayohusiana na utekelezaji wa sheria za Mwenyezi Mungu, na mara nyingi alikuwa akitegemea maamuzi ya waziri wake (Khalifa mtendaji), kwa mfano katika suala la haki ya mgao wa Zaka kwa watu wanaotiwa nguvu nyoyo zao, Abu Bakar alilitolea maamuzi sahihi kwa mujibu wa Qur'ani kwamba wapewe haki yao hiyo kama Mtume (s.a.w.w.) alivyokuwa akiwapa, lakini shauri hilo lilipomfikia Umar alilitolea maamuzi hasi, na maamuzi ya waziri huyo yakawa ndio yenye kufuatwa na ya Khalifa Abu Bakar yakawekwa pembeni! Kisa hicho kilikuwa kama ifuatavyo:

Hakika Iyaynatu ibn Husni, Aqra-a ibn Habis na Abbas ibn Murdaas walikwenda kwa Abu Bakar kutaka wapatiwe sehemu yao ya Zaka, Abu Bakar aliwaandikia, baada ya kuandikiwa walikwenda kwa Umar na wakamkabidhi ile hati, Umar baada

ya kupewa aliichanachana, kisha akasema: Fungu hili alikuwa Mtume (s.a.w.w.) akikupeni ili kukuzoesheni katika Uislamu na amekutajirisheni kwa hilo, basi ikiwa mumeshathibiti katika Uislamu ni vyema, na kama bado basi kati yetu sisi na nyinyi ni upanga tu, na sema (akasoma Aya ifuatayo**): "Na ukweli unatoka kwa Mola wako, basi anayependa akubali na anayependa akatae." (Qur'ani,18: 29).**Wale watu walirejea kwa Abu Bakar r.a. na kumuuliza: Khalifa ni wewe au ni Umar? Kwani wewe ulitupa hati na Umar akaichanachana, Abu Bakar akawajibu: Khalifa ni yeye akipenda."[25]

Hivi ndivyo ulivyokuwa uendeshaji wa dola ya Kiislamu katika zama za utawala wa Abu Bakar! Na jambo la kusikitisha ni kuwepo baadhi wa madhehebu ya Kiislamu kushikana na Sunna ya waziri huyu wa Abu Bakar na kufumbia macho maneno ya Mwenyezi Mungu yenye kuthibitisha kwamba miongoni mwa watu wanaostahiki kupewa Zaka ni watu wanaotiwa nguvu nyoyo zao, kama ilivyokuja katika Aya hii:

إِنَّمَا الصَّدَقَاتُ لِلْفُقَرَاءِ وَالْمَسَاكِينِ وَالْعَامِلِينَ عَلَيْهَا وَالْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمْ وَفِي الرِّقَابِ وَالْغَارِمِينَ وَفِي سَبِيلِ اللَّهِ وَابْنِ السَّبِيلِ فَرِيضَةً مِنَ اللَّهِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ

> "Hakika sadaka ni ya (hawa) tu: Mafukara na masikini na wanaozitumikia na wanaotiwa nguvu nyoyo zao, na kuwakomboa watumwa na wenye madeni na katika njia ya Mwenyezi Mungu na mwana njia. Ni faradhi kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye hekima."(Qur'ani,9: 60).

[25] Sayyid Sabiq, *Fiqhu Sunna*: Jz. 1, Uk. 390.

# HOTUBA YA ABU BAKAR

> “Hotuba ya Abubakar nayo ina umuhimu wake katika uongozi wa Uislamu kwani inaonesha wajibu wa kiongozi pale aliposema:’’Enyi watu mmenichagua niwe mdhamini wenu ingawa mimi sio bora kuliko wengi miongoni mwenu. Nikiwa sahihi nitiini. Nikipotoka nirekebisheni,[26] kwani ukweli ni uaminifu na uongo ni kutoaminika, aliyedhaifu atakuwa na nguvu mbele yangu mpaka nishindwe kumpatia haki zake Insha-Allah; na mwenye nguvu (Uwezo) mbele yangu atakuwa dhaifu mpaka alipe haki za wengine Insha-Allah. Allah huteremsha. Na kama kwa watu walioacha Jihadi katika njia yake. Vilevile Mwenyezi Mungu huteremsha maafa kwa watu ambao hufanya maovu.’’Alipomaliza alitokea mtu mmoja aliyesema kama hutafuata haki tutakunyoosha kwa ncha ya upanga. Angalia uhuru wako! Yule raia hakuogopa wala Khalifa hakukasirika.”[27]

Uchaguzi wa Abu Bakar ulifanyika katika mazingira ambayo watu wengi walikuwa katika nyumba ya Mtume (s.a.w.w.) wakisubiri kumsitiri Mtume wao, huku Ahlulbayti wa Mtume (s.a.w.w.) wakishughulika kumuosha. Kwa hivyo maneno yake haya yanawahusu wale wachache tu waliokuwa katika ukumbi wa Saqifa Bani Saida au waliohudhuria katika msikiti baada ya kutoka Saqifa, na pia uchaguzi wake ulifanyika katika mazingira ya kushitukizia na

[26] Dini ya Mwenyezi Mungu itaongozwaje na mtu anayepotoka! Ukweli huu mnaupata kutoka kwake mwenyewe lakini bado mnampa sifa ya kustahiki kuliko wale waliotakaswa na Mwenyezi Mungu ambao ni Ahlul-Bayt (a.s.) kwa ushahidi wa Qur’ani na Hadith? Naye mwenyewe hapo amekiri kwamba kuna wabora zaidi yake, hamkuliona hilo? **“Na aminini niliyoyateremsha ambayo yanasadikisha mliyonayo, wala msiwe wa kwanza kuyakataa, wala msiuze Ishara Zangu kwa thamani ndogo, na niogopeni Mimi tu. Wala msichanganye Haki na batili, mkaificha haki na hali mnajua.” (al-Baqara; 2:41-42).**

[27] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.322.

sio jambo lililokuwa limepangiliwa kama Khalifa Umar Farruq alivyoeleza.

Ama kuhusiana na hotuba aliyoitoa Abu Bakar, ni kuwa ameweka bayana kwamba yeye sio bora kuliko wengi miongoni mwao. Huku ni kukubali kwake kwamba miongoni mwa Maswahaba wa Mtume (s.a.w.w.) mulikuwa na watu bora kuliko yeye, na kwa utafiti wa haraka haraka tutaona kwamba wale waliobakia katika nyumba ya Mtume (s.a.w.w.) baada ya kufariki na kuutayarisha mwili wake mtukufu kwa ajili ya makaazi yake ya akhera, na bila ya kujali kile kilichokuwa kikiendelea katika ukumbi wa Saqifa, watu hao ni bora zaidi kwani walitambua heshima ya Mtume wao, na bila ya kumtofautisha katika hali ya uhai wake na umauti wake, kwani miongoni mwao wamo wale waliotakaswa na Mwenyezi Mungu na kila aina ya uchafu.

Pia Abu Bakar anatambua vyema juu ya fadhila mbalimbali walizonazo watu wa nyumba ya Mtume (s.a.w.w.), watu ambao Mtume (s.a.w.w.) aliwausia Waislamu washikamane nao baada ya yeye kufariki. Na hata Abu Bakar mwenyewe amesikika akisema: "Mchungeni (muhifadhini) Muhammad (s.a.w.w.) kwa kuwaheshimu Ahlulbayt wake."Anatambua wazi kwamba heshima ya mtu ya kumheshimu Mtume (s.a.w.w.) ni kuwaheshimu wanafamilia yake Mtume (s.a.w.w.), hii ni kuonesha ubora wa watu hao. Baada ya kulitambua hilo, ndio maana akasema kwamba yeye si bora kuliko wengi miongoni mwao, kwani sifa hiyo yeye hanayo. Zaidi ya hayo tumeona ni namna gani alivyojuta mwishoni mwa uhai wake kutokana na mambo aliyoyafanya, likiwemo hili la kujitwalia Ukhalifa na kuikashifu nyumba ya watu walio bora.

# MAWAZO TOFAUTI KUHUSIANA NAUCHAGUZI WA KHALIFA WA KWANZA

Kuhusiana na maudhui haya wamenakili maneno yafuatayo:

> "Wapo wasemao uchaguzi ule ulifanyika katika mazingira ya kuchanganyikiwa, kwani mkutano haukuwa rasmi. Maelezo ya kundi hili yameegemea kauli zisemazo kuwa Abubakar (r.a.) na Umar (r.a.) walistushwa na taarifa ya kuwa Ansar walikuwa wamekutana katika ukumbi wa mikutano wa Saqifa Bani Saida, kuchagua kiongozi anayetokana na wao ambaye angeshika uongozi wa dola ya Kiislamu baada ya Mtume (s.a.w.). Kwa mujibu wa kauli hizo Abubakar (r.a.) na Umar (r.a.) walilazimika kwenda kwenye mkutano huo wakiwa na dhamira ya kuzuia usiendelee, hasa ikizingatiwa kuwa Mtume bado alikuwa hajazikwa na hilo ni suala zito lililohitajia mwafaka wa Waislamu wote."[28]

Kwa kweli hii ni kauli sahihi, kwani miongoni mwa watu wanaounga mkono rai hii ni Umar Farruq. Amekiri waziwazi kwamba uchaguzi wa Abu Bakar ulikuwa ni jambo la kushitukiza (halikupangwa rasmi). Na ni vyema hapa wanafunzi wenzangu na wasomaji wengine wakaelewa kwamba wale waliohudhuria katika kinyang'anyiro cha Ukhalifa hawakuhudhuria maziko ya Mtume (s.a.w.w.), kama alivyoeleza Sheikh Abdulla Saleh al-Farsiy.

Na halikuwa ni jambo ambalo linahitaji muwafaka wa Waislamu, kwa vile tayari Mtume (s.a.w.w.) alikwishalitolea maamuzi, kwamba haki ya uongozi baada yake ni ya Ahlul-Bayt(a.s.) Jambo lililokuwa linahitajika ni kushughulikia mwili wa Mtume (s.a.w.w.) na baada ya kumaliza shughuli ya maziko, Waislamu kuwa tayari kuwa chini ya uongozi wa Imamu Ali (a.s.) kwani yeye ndiye waliyempa viapo vyao vya utiifu wa kuwa Khalifa katika bonde la Khum, baada ya

[28] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.322.

Mtume (s.a.w.w.) kuwatangazia kwamba amewaachia vizito viwili: Qur'ani na Ahlulbayt wake.[29]

> "Kundi jengine lina mawazo kuwa: Pamoja na kuwa mkutano wa Ansar haukuwa rasmi, lakini kuchaguliwa Abubakar (r.a.) kuliafikiwa, kwa kuzingatia dokezo za Mtume, ishara zitokanazo na Qur'ani na aliyokuja kuyafanya Abubakar (r.a.) wakati wa uongozi wake, ambayo yalidhihirisha usahihi wa chaguo la mkutano wa Saqifa Bani Saida."[30]

Bila ya shaka kitu ambacho kimejengwa juu ya msingi usio sahihi hakiwezi kuwa sahihi. Ni vipi kundi hili likubali kwamba uchaguzi haukuwa sahihi, kisha kuchaguliwa kwake kuwe kumeafikiwa, kumeafikiwa msingi upi?!

Ni vipi suala hili zito liwe limejengewa katika misingi ya ishara na dhana?!Yale aliyoyafanya ni wazi yalidhihirisha kuwa chaguo la mkutano wa Saqifa halikuwa sahihi, kwani kama tulivyoeleza huko nyuma tumeona namna alivyotenda mambo ambayo mwishowe aliyajutia, na zaidi alijutia hata kujitwalia Ukhalifa.

Ama kuhusiana na dokezo pamoja na ishara za Qur'ani kwamba zimeashiria kwamba yeye ndiye mtu anayestahiki zaidi Ukhalifa, ni kwamba maneno ya Mtume (s.a.w.w.) yako wazi kabisa kwamba haki ya Ukhalifa baada yake ni ya Ahlubayti wake (a.s.) Na Aya za nyingi za Qur'ani zimebainisha utukufu na ubora wa Ahlul-Bayt wa Mtume (s.a.w.w.), na kuna Aya mbalimbali zilizoteremka kuwalaumu Maswahaba, lakini hakuna Aya hata moja iliyoteremka kumlaumu Imamu Ali (a.s.), hii ni kwa sababu yeye ni mtu mkamilifu aliyetakaswa na Mwenyezi Mungu Mtukufu dhidi ya uchafu kama ilivyokuja katika Aya ya 33 ya Sura ya 33.

---

[29] Sahihu Muslim, Babu fi Fadhaili Ali r.a: J.7, Uk.123.

[30] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.322.

> "Wapo wanaosema kuwa kutokuwepo kwa watu wa nyumba ya Mtume (Ahlul-Bayt) katika mkutano ule, kunabatilisha zoezi zima la uchaguzi wa khalifa wa kwanza. Maelezo ya kundi hili yanatiwa tashdid na usia, unaodaiwa kuachwa na Mtume (s.a.w.) kwa 'Ahlul-Bayt' muda mfupi kabla ya kutawafu kwake; unaosema kwamba haki ya uongozi wa umma huu baada yake ni ya 'Ahlul-Bayt'. Kwa hivyo Ali (r.a.) alistahiki nafasi hiyo, na warithi baada yake ni wanawe Hassan na Husein kwa kuwa ni wajukuu wa Mtume (s.a.w.), kundi hili linadai kuwa Ukhalifa wa Abubakar (r.a.) na Umar (r.a.) na Uthman (r.a.) ni 'batili' kwa kuwa hao si katika watu wa nyumba ya Mtume (s.a.w.) na walipewa uongozi katika mikutano isiyo rasmi. Aidha hatua ya kuwafanya Makhalifa ni kudhulumu haki ya Ali (r.a.) akiwa ndugu wa Mtume."[31]

Kwa vile Mtume (s.a.w.w.) alikuwa ameshalimaliza suala hili kwa kuwabainishia Waislamu viongozi wao, kulikuwa hakuna haja ya kufanyika mkutano wa kujadili jambo ambalo Mtume alishalitolea maamuzi, na kama ilikuwa hajalitolea maamuzi, basi ilikuwa ni vyema na uungwana kushirikishwa katika jambo hilo kutokana na umuhimu wao na mchango wao mkubwa usio na kifani katika kuisimamisha Dini ya Mwenyezi Mungu, na si wao tu bali ilikuwa na Waislamu wengine washirikishwe, hasa ikizingatiwa kwamba ni idadi ndogo sana ya Muhajirina walioshiriki mkutano huo wa Saqifa.

Ikiwa kuna madai yanayodaiwa kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliacha usia na kwamba haki ya uongozi ni ya Ahlul-Bayt wa Mtume (s.a.w.w.), basi madai hayo yamo katika vitabu sahihi vya kisunni kama vile Sahih Muslim na vinginevyo, kwani vimetamka wazi kwamba alivyotuachia Mtume (s.a.w.w.) ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Ahlul-bayt wa Mtume (s.a.w.w.).

> "Na kuna wasemao kwamba, kwa kuwa Uislamu ni dini ya Mwenyezi Mungu si ya ukoo, kabila au Taifa fulani, na kwa

[31] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.322.

> kuwa hakuna aya katika Qur'ani inayomuamrisha Mtume (s.a.w.) kurithisha dhima ya uongozi baada yake kwa watu wa nyumbani kwake (Ahlul-Bayt), basi jukumu la uongizi la umma limeachwa mikononi mwa waumini wenyewe. Kiongozi atachaguliwa kwa kuzingatia sifa mbalimbali zikiwemo uoni, ucha Mungu, siha n.k. sifa zote zimepelekea kuongoza kwa haki na uadilifu. Kwa hivyo Ukhalifa wa Abubakar, Umar na Uthman si suala la kubishaniwa."[32]

Bila ya shaka yeyote ile, Uislamu ni Dini ya Mwenyezi Mungu na si ya watu fulani, lakini izingatiwe kwamba hakuna haki ya kuingilia maamuzi ya Huyu Mwenye Dini hii, kwani katika uendeshaji wa Dini Yake huteuwa watu wa familia fulani ili kuwaongoza wengine, kama alivyofanya kwa familia ya Imran na ile ya Nabii Ibrahim.

Ni kweli hakuna Aya inayomuamrisha moja kwa moja Mtume (s.a.w.w.) kuwarithisha watu wake uongozi baada yake, lakini alilolifanya Mtume (s.a.w.w.) kumuomba Mwenyezi Mungu amfanye ndugu yake waziri wake kama vile alivyofanya Nabii Musa kumuomba Mwenyezi Mungu amfanye ndugu yake, Harun (a.s.) waziri, kama ambavyo Mwenyezi Mungu alimkubalia ombi lake hilo, pia alimkubalia Mtume (s.a.w.w.) ombi lake, maelezo ya hoja hizi tutayaeleza kwa kina huko mbele Mwenyezi Mungu akipenda.

Na lau kama kungezingatiwa sifa mbalimbali za kumpata kiongozi zikiwemo uoni, ucha Mungu, siha n.k. bila ya shaka kusingekuwa na Swahaba yeyote ambaye angekuwa na sifa za kumshinda Ali ibn Abi Talib, kwani yeye ndiye mlango wa mji wa elimu ya Mtume (s.a.w.w.), kama Mtume (s.a.w.w.) anavyosema:

أنا مدينة العلم وعلي بابها فمن أراد العلم فليأته من بابه.

[32] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.323.

> "Mimi ni mji wa elimu na Ali ni mlango wake, basi mwenye kuitaka elimu auwendee mlango wake."[33]

Ama kuhusiana na siha, ushujaa aliouonesha katika vita mbalimbali ambavyo aliweza kuleta ushindi mnono, ni dalili tosha kwamba alikuwa na siha njema iliyochanganyika na ucha Mungu.

Miongoni mwa hoja kubwa zilizotawala katika ukumbi wa Saqifa na kuwafanya Answari washindwe na Muhajirina wachache katika ukumbi wao wa mikutano ni hoja ya ukabila, ni pale Maanswari walipotoa hoja kwamba wao wana haki zaidi ya kuwa watawala kutokana na mchango wao mkubwa walioutoa katika Uislamu, Umar alisimama na kuwaambia: Waarabu hawataridhika kutawaliwa na nyinyi ilhali Nabii wao anatokana na watu wasiokuwa nyinyi, lakini Waarabu hawaridhiki isipokuwa jambo hili (Ukhalifa) lishikwe na wale ambao Utume uko kwao na wenye mamlaka watoke kwao, sisi tuna hoja ya wazi juu ya hilo dhidi ya yeyote anayetukhalifu miongoni mwa Waarabu, na pia tuna dalili madhubuti, ni nani anayezozana nasi juu ya usultani wa Muhammad na mirathi yake, na ilhali sisi ni marafiki zake na jamaa zake, hazozani nasi isipokuwa mwenye kutoa hoja batili au mwenye kumili katika maovu au mwenye kuzama katika maangamizi."[34]

Je, huoni kwamba ubaguzi wa kikabila ndiyo iliyokuwa hoja ya Maquraysha katika ukumbi wa Saqifa?! Ili kuhakikisha hili ndio maana katika hao Makhalifa waongofu wakiwa ni wanne au watano akiwemo Imamu Hasan ibn Ali ibn Abi Talib (a.s.), au sita akijumuishwa Umar ibn Abdul Azizi wote wana asili ya Makka, anakotokea Mtume s.a.w.w., hakuna yeyote mwenye asili ya Madina (Maanswari) aliyeinusa harufu ya Ukhalifa, si hilo tu hata nafasi kubwa kama za ugavana wengi wao waliozishika ni Makureyshi wa

[33] Attabraniy, *Mu'jamul Kabir*: Jz. 11, Uk. 55.
[34] Ibn Qutayba, *al-Imama Wassiyasa*: Jz. 1, Uk. 16

Makka, kwani waliamini kwamba ukhalifa ni milki yao na mirathi yao kutoka kwa Mtume ambaye anatokana na kabila lao!

Kama kweli waliongoza kwa haki basi Abu Bakar asingejutia yale aliyoyafanya katika Ukhalifa wake kama tulivyobainisha huko nyuma. Na pia Khalifa Umar asingeanzisha Swala ya tarawehe kwa jamaa, na kuiharamisha ndoa ya Mut'a (ndoa ya muda), na kuwakusanya watu waswali Swala ya jeneza kwa takbira nne.[35] Na wala Khalifa Uthman asingewapa nafasi kubwa kubwa jamaa zake ambao walisifika na sifa mbaya kama vile Walid ibn Uqba, aliyewaswalisha watu rakaa nne kwenye Swala ya Asubuhi huku akiwa amelewa, na kumrejesha mjomba wake, Hakam katika mji wa Madina baada ya kuishi uhamishoni kutokana na kutimuliwa na Mtume (s.a.w.w.) kwenye mji huo, na asingetangaza wazi kwamba lau kama funguo za Pepo zingekuwa mikononi mwake angewaingiza banu Umayya wote.[36] Kwa vile funguo za Pepo zimo mikononi mwa Mwenyezi Mungu, aliamua kuwazawadia nafasi mbalimbali za uongozi licha ya kuwa ni watenda maovu dhahiri shahiri!

[35] *Masahaba kumi waliobashiriwa Pepo*: Uk.26.
[36] *Masahaba kumi waliobashiriwa Pepo*: Uk.38.

# TUKIO LA KARATASI

Waandishi wa kitabu hicho wameshikilia hoja yao ya kuthibitisha Makhalifa waliowathibitisha kwa kupinga tukio mashuhuri lililotokea katika historia ya Uislamu, na wakadhani kwamba wale wanaoamini ya kwamba Ukhalifa ulikuwa ni haki ya watu wa nyumba ya Mtume (s.a.w.w.) (Ahlul-Bayt) wanategemea usahihi wa kutokea tukio hili (Tukio la Karatasi). Ukweli ni kwamba tukio hili lilitokea kama vile lilivyonakiliwa na Bukhari na Muslim katika sahihi zao, lakini hata kama tukikubali kimjadala tu kuwa hakukuwa na amri ya Mtume (s.a.w.w.) ya kutaka apelekewe kalamu na karatasi ili aandike yale ambayo kwayo watu hawatopotea, bado haki ya Ukhalifa itabaki kwa wale waliousiwa na Mtume (s.a.w.w.). Tukio hilo wamelielezea kama ifuatavyo:

"Tukio la 'KARATASI' lililonakiliwa katika vitabu vya Muslim na Bukhari kuwa siku tatu kabla ya kutawafu Mtume(s.a.w.) alitamka; Nipeni peni na wino ili niwaandikie maelezo yatakayowafanya watu wasipotee" (Nipeni peni na wino ili niwaandikie usia ambao utawafanya watu wasipotee), halina ukweli. Kutokana na kauli hii inadaiwa kuwa Umar alihutubia watu na kusema kuwa ''Mtume yuko katika maumivu makali, Qur'an kama muongozo unatutosha kwa watu. Baadhi ya watu wanasema Mtume amepoteza fahamu. Ipo kauli pia isemayo maneno haya yamesemwa na Umar (Khalifa wa pili).

Moja ya hadithi hizo imo katika kitabu cha Bukhari juzuu ya 1 hadithi namba 114 katika ukurasa wa 86 tafsiri ya Kiarabu, kingereza isemayo hivi: Amesimulia Ubaidulla bin Abdulla, kuwa Ibn Abbas amesema:

> ‘’Hali ya Mtume (s.a.w.) ilipokuwa mbaya alisema: ‘’Nileteeni karatasi ya kuandika, na nitawaandikia tamko litalowapelekea kutopotea.’’ Lakini Umar akasema: Mtume anaumwa sana na tuna kitabu cha Mwenyezi Mungu ambacho kinatosheleza. Lakini masahaba wa Mtume wakatofautiana juu ya jambo hili. Kutokanana zogo hili Mtume akawaambia: Ondokeni (na niachieni peke yangu) sio sahihi mbishane mbele yangu. Ibn Abbas akatoka nje na kusema: Imekuwa bahati mbaya na msiba mkubwa kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amezuiliwa kuandika tamko kwa sababu ya kutokubaliana kwao na makelele yao.’’

Baada ya maelezo yao hayo, wameandika dondoo zifuatazo:

> Kutokana na hadithi hii ni dhahiri kuwa Ibn Abbas ameshuhudia tukio hili na akatoka nje na kusema kauli hii. Ukweli sio huu kwa sababu Ibn Abbas alikuwa anatamka kauli hii alipokuwa anasimulia hadithi hii, lakini yeye binafsi hakushuhudia tukio hili. Kwa maelezo zaidi juu ya hili rejea Fat-h al-Barr juzuu ya 1, ukurasa wa 220.”[37]

Haya ndiyo waliyoyanakili kuhusiana na tukio hili, licha ya kukiri kwamba ni tukio lililo nakiliwa katika vitabu sahihi (*Bukhari* na *Muslim*), lakini wanadai kwamba hakuna ushahidi wa kutosha wa kutokea tukio hili, wanasema:

> “Pamoja ya kuwepo maandishi juu ya tukio hili na wanahistoria kuwa na mifano na tafsiri tofauti, hakuna ushahidi wa kutosha kama tukio hili limetokea kweli au ni maandishi tu yenyewe yaliyopachikwa ili kukidhi haja ya waliyobuni tamko hili. Tukio hili halina ukweli wa kihistoria kwa sababu zifuatazo:[38]

---

[37] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.323.

[38] Wenyewe Ahlus-Sunnah wal-Jama’a mnasema kila kilichomo kwenye Bukhari ni sahihi. Sasa je, nyinyi mnataka kutuambia kwamba mmebadilika na kusema kwamba ndani ya Bukhari kuna ya uwongo!

Ni muhali kudhani kuwa Mtume anaweza kuzuiwa na swahaba au na yeyote asiye Allah (s.w.) kutekeleza jambo la Utume wake; inashangaza zaidi kuwataja maswahaba? Mbaya zaidi ni tukio hili linavyonasibishwa na maudhui ya aya tatu za mwanzo za Suratul Hujrat zinazosomeka hivi:

1. Enyi mlioamini! Msitangulie (kusema lenu) mbele ya (neno la) Mwenyezi Mungu na Mtume wake, mcheni Mwenyezi Mungu, hakika ni mwenye kujua.

Kuwa wanaweza kumpinga Mtume katika Utumewakati huu akiwa katika kitanda cha mauti. Linaloshangaza zaidi ni lengo la tukio hili: Kwa mujibu wa maelezo (323) yaliomo ni kuwa Mtume (s.a.w.) hakuandika tamko alilokusudia ingawa aliishi siku nne baada ya tukio hili akiwa katika hali isiyo mbaya sana hata Abubakar akarudi kitongojini kwake, kulipokuwa na umbali wa maili mbili hivi kutoka mjini Madina. Kama hali ilikuwa hii kwa nini basi usia huu usiandikwe?

1. Enyi mlioamini; msipaze sauti zenu kuliko sauti ya Mtume wala msiseme naye kwa sauti ya ngumu kama mnavyosemezana nyinyi kwa nyinyi, visije vitendo vyenu vikakosa thawabu, na hali hamtambui.

2. Kwa hakika wanaoangusha sauti zao mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, hao ndiyo Mwenyezi Mungu amezisafisha nyoyo zao kwa kumuogopa Mungu. Basi yatakuwa kwao maghufira na thawabu kubwa (kabisa).

Sura hii ni ya 106 kwa utaratibu wa kushushwa na tukio hili lilitokea siku nne kabla ya kutawafu kwa Mtume (s.a.w.). Wafasiri wa Qur'an wa mrengo wa unaohusisha tukio hili la Karatasi na aya

1-3 za sura 49 wanaonesha kutotokea kwa jambo hili kwani Suratil Hujrat ilishushwa zamani kabla ya tukio la Karatasi.

Baya kuliko yote yaliokwishatajwa ni kumsingizia Mtume (s.a.w.) kuwa amepoteza fahamu. Utume wa Mtume umekoma tu pale alipotawafu, kwa sababu yoyote ile, hali hii ingepelekea utata katika utume na ujumbe wake ndio maana makafiri wa Kikureish walipomwita majnuni Mwenyezi Mungu amekanusha hili. Hivyo Mwenyezi Mungu asingejipinga tena na kuruhusu Mtume hata kwa nukta moja awe majnuni. Hali inakuwa ngumu zaidi wakati usia huu unapohusishwa na Ali na kudaiwa kuwa ulikuwepo. Mtume alipotawafu Ali, Abbas na nduguze Mtume walikaa katika nyumba ya Fatma binti ya Muhammad kupanga mashauri ya uongozi. Kama usia huu ungekuwepo basi tungemtegemea Ali auwakilishe kwenye ukumbi wa mikutano wa Saqifa Bani Saidah ambapo Ansar na Muhajirina walikuwa wanajadili juu ya jambo hilo hilo la uongozi wa dola baada ya kufa Mtume (s.a.w.), isitoshe katika siku aliyokufa Mtume (s.a.w.) Bukhari katika sura ya ugonjwa wa Mtume (s.a.w.) amenakili hadithi isemayo Abbas alimshika mkono Ali na kumwambia twende kwa Mtume (s.a.w.) kumuuliza kabla hajafa nani ashike nafasi ya uongozi baada yake, kama sisi ni warithi wa halali Mtume ataacha usia. Ali alijibu kuwa hutauliza swali hilo kwani Mtume akisema hapana matumaini yote ya baadae yatatoweka. Hivyo ni dhahiri hakukua na usia wowote kutoka kwa Mtume juu ya nani atawale baada yake."[39]

Bila ya shaka ukweli wa tukio la karatasi hauhitaji sisi tuuthibitishe, kwani wao wenyewe wameeleza wazi kwamba tukio hilo limesajiliwa katika vitabu sahihi zaidi baada ya Qur'ani, *Sahih Bukhari* na *Sahih Muslim*.

[39] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.322-324.

Na kwa vile wamesimamia katika misingi ya kupinga tukio hili sahihi, bila ya shaka na mengi mengineyo yasiyo na ukweli yatatarajiwa kuzushwa, kama vile hoja ya kufikishwa madai ya usia juu ya Imamu Ali (a.s.) katika ukumbi wa Saqifa Bani Saida wakati watu walipokuwa wakijadiliana juu ya uongozi! Kwa kweli hoja hii haina mashiko yoyote, hasa ikizingatiwa kwamba wakati huo wa kujadiliana juu ya uongozi, ndiyo wakati ambao Imamu Ali (a.s.) akisimamia kumuosha Mtume (s.a.w.w.). Na wala hakutaarifiwa juu ya kadhia hiyo, yeye na masababa mashuhuri wa Mtukutu Mtume (s.a.w.w.) kwa lengo la kuwaficha jambo hilo, wakihofia mpango wao kutofanikiwa.

Lau kama waandishi wa kitabu hicho, wangekukuwa na kumbukumbu juu ya yale waliyoyasema kuhusiana na namna Imamu Bukhari alivyokuwa akiswali rakaa mbili kabla ya kuiandika hadithi, wasingeikanusha Riwaya hii, wamesema: "Alisema Imamu Bukhari kwamba hakuwahi kuiandika hadithi kwenye kitabu chake ila baada ya kuswali rakaa mbili, kufanya hivyo ili kumuomba Mwenyezi Mungu ampe taufik (amkubalie). Imamu huyo alikusanya jumla ya hadithi 600,000 na alihifadhi 200,000,lakini hadithi sahihi alizozichagua kwenye kitabu chake ni 7275."[40]

Na wala tukio hili halina mafungamano na ushukaji wa Suratul Hujrat, huko wametajwa wale waliopaza sauti zao mbele ya Mtume (s.a.w.w.) kabla ya tukio hili, lililojitokeza katika tukio hili ni kukariri kile walichokifanya mwanzo, na Mwenyezi Mungu kuwakataza wasifanye hivyo, lakini masikini waliweza kurudia kitendo hicho ambacho kina athari mbaya katika matendo mema ya Muumini, kwani huweza kuyaharibu matendo hayo yote na mtu kuwa muflisi.

---

[40] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari Kitabu cha 2, Uk. 226.

Zaidi ya hayo wanachuoni wakubwa waliosherehesha vitabu hivyo hakuna hata mmoja aliyethubutu kuikana hadithi hiyo kwa kudai kwamba si sahihi au ni ya kupangwa, bali walichokifanya ni kuonesha namna yule aliyeongoza kuzuia pasiandikwe usia huo alivyokuwa mahiri, mwenye hekima na uwelewa wa kina, kwani alikhofia lau kama Mtume angepewa kalamu na wino angeandika mambo ambayo yangekuwa mazito kutekelezeka! Anasema Imamu Nawawiy: "Ama kuhusiana na kauli ya Umar r.a., ni kwamba wanachuoni wenye kuisherehesha hadithi hii, wanaona ni kwamba inaonesha uelewa wa Umar na fadhila yake na ukomavu wa uoni wake, kwani alichelea Mtume (s.a.w.w.) kujakuandika mambo ambayo huenda wakashindwa kuyatekeleza, na wakaja wakastahiki kuadhibiwa kwayo, kwa vile ni mambo yaliyoamrishwa kwa uwazi, na hayahitaji kufanyiwa ijtihadi, kwahivyo ndio maana Umar akasema: Kinatutosha kitabu cha Mwenyezi Mungu…"[41]

Kulikataa kwao tukio hili sahihi, kunamalengo ya kukataa suala zima la usia wa Mtume (s.a.w.w.) aliotaka kuuandika, kwani hata miongoni mwa maulamaa wa madhehebu ya Ahlu Sunna wako wanaoona kwamba, Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na lengo la kutaka kuandika wasia juu ya mtu atakayeshika nafasi yake baada yake.[42]

Kwa maelezo zaidi juu ya usahihi wa tukio hili unaweza kurudia kitabu cha Sheikh Abdillahi Nasir katika kitabu chake kiitwacho *'Ukweli wa Hadithi ya Karatasi.'* Huko Sheikh wetu amefafanua kwa kina ukweli kuhusu kutokea kwa tukio hili baada ya wasomi hao wa I.P.C. kuyasambaza haya yaliyomo katika kitabu chao hicho kwa kupitia gazeti la Annur.

Kwa kweli si muhali kudhani kuwa Mtume anaweza kuzuiwa na swahaba au na yeyote asiye Allah (s.w.) kutekeleza jambo la Utume

[41] Annawawiy, *Sharhu Muslim*: Kitabul Waswiya, Babul Waqfu: Jz. 11, Uk. 90
[42] Kitabu kilichotangulia.

wake, kama walivyodai waandishi wa kitabu hicho, kwani kuzuiliwa kufikisha Ujumbe ni jambo dogo miongoni mwa changamoto kubwa walizokabiliana nazo Mitume ya Mwenyezi Mungu, kwani Mitume wengine walioteuliwa kufanya kazi ya kufikisha Ujumbe wa Mola Wao waliuwawa, na wengine kuingizwa katika ughaibuni. Na hata Mtume (s.a.w.w.) alilazimika kuuhama mji wake alimozaliwa na ambao ulikuwa ukihitaji zaidi ulinganio wake kutokana na kuzama katika ushirikina.

Mtume katuachia, viwili vya kuongoa.
Qur'ani ya Jalia, na watu wake Nabia.

Ikiwa tutavishika, uongofu tutapata.
Katu hatutopotoka, kwenye haki kutoka.

Alipotaka waandikia, wengine walifoka.
Wakasema: Waumia, na akilizo hazijatulia.

Mtume hakuvumilia, kwa yale walomwambia.
Tahamaki kawatimua, nje wakajitokea.[43]

Wito wetu kwa wana wa IPC, ikiwa mmediriki kuikataa Riwaya ilionakiliwa na Bukhariy na Muslim, kwa vile mnaona kusihi kwake kunashusha hadhi ya wale waliokataa maagizo ya Mtume (s.a.w.w.), basi tambueni kwamba katika vitabu hivyo mna mambo yanayowadhalilisha mno Mitume wa Mwenyezi Mungu, akiwemo Mtume Muhammad (s.a.w.w.), mkitaka kuyajua, rejeeni katika kitabu kiitwacho, *Shia na Hadithi,* kilichoandikwa na Sheikh Abdillahi Nasir. Tungefurahi lau kama mtajasirika na kusema kwamba si sahihi, kwa kweli hiyo itakuwa ni heshima kubwa sana kwa waja hao watukufu wa Mwenyezi Mungu.

[43] Rejea utenzi wa Marehemu Sheikh Abdallah Saleh Farsy.

Kuhusiana na maandiko yanayoaminiwa na baadhi ya Waislamu (Mashia) kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliwacha wasia juu ya mtu atakaeshika uongozi wa Dola ya Kiislamu baada ya yeye kufariki, jambo hili limeonekana ni kioja na jambo lisilo na msingi katika Uislamu, na kama kwamba ni jambo geni katika Dini hii Tukufu kuanzia kwa Adam (a.s.) hadi kwa Mtume Mtukufu (s.a.w.w.), wanasema:

> "Lakini ni akili ya ajabu inayofikiria kuwa uongozi wa Kiislamu utokane na ukoo wa Mtume tu kwa sababu hili ni jambo geni katika historia ya Mitume. Hakuna Mtume yeyote aliyeusia nduguze ndiyo wawe viongozi wao wanapotawafu, ingekuwa ni suna yao pangekuwa na hoja ya kuelezeka."[44]

Jibu la hoja yao hii, ni kwamba si kila mtu anayekuwa katika ukoo wa Mtume anakuwa yuko katika nafasi ya kuwa kiongozi kama vile ilivyo katika mfumo wa kifalme. Lakini tunaporudi katika historia ya Mitume tuaona ni namna gani Mitume hao walivyokuwa wakimuomba Mwenyezi Mungu ili awafanye viongozi watu wa koo zao, kwa kuanzia, tuanze na baba wa Mitume, Nabii Ibrahim(a.s.) alivyotaka nafasi aliyokuwa nayo pia waipate watoto wake baada yake, ni pale baada ya kutahiniwa na Mwenyezi Mungu na kuweza kufaulu mtihani huo, zawadi aliyopewa na Mola Wake ni zawadi ya Uimamu (Uongozi), alimuomba Mwenyezi Mungu pia awape watoto wake kama Qur'ani inavyosema:

وَإِذِ ابْتَلَى إِبْرَاهِيمَ رَبُّهُ بِكَلِمَاتٍ فَأَتَمَّهُنَّ قَالَ إِنِّي جَاعِلُكَ لِلنَّاسِ
إِمَامًا قَالَ وَمِنْ ذُرِّيَّتِي قَالَ لَا يَنَالُ عَهْدِي الظَّالِمِينَ

---

[44] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.324.

"Na Mola wake alipomjaribu Ibrahim kwa matamko, naye akayatimiza. Alimwambia: Hakika Mimi nimekufanya Imam wa watu. Akasema: Na katika kizazi changu (pia)? Akasema: Ahadi yangu haiwafikii madhalimu." (Qur'ani, 2:124).

Hapa Mwenyezi Mungu hakumkaripia Nabii Ibrahim (a.s.) kwa ombi lake hilo la kutaka pia watoto wake wawe viongozi kama alivyo yeye, ila Mwenyezi Mungu aliweka sharti la mtu kutokuwa dhalimu. Na tukiisoma historia ya Kiislamu inatuonesha ni idadi kubwa ya wana wa Ibrahim waliopata nafasi hiyo.

Mtume mwengine ni Nabii Musa (a.s.), alimuomba Mwenyezi Mtukufu amfanye ndugu yake, Harun (a.s.) awe na madaraka ya uwaziri katika harakati zake za uongozi, kama Mwenyezi Mungu anavyosema:

قَالَ رَبِّ اشْرَحْ لِي صَدْرِي وَيَسِّرْ لِي أَمْرِي وَاحْلُلْ عُقْدَةً مِنْ لِسَانِي يَفْقَهُوا قَوْلِي وَاجْعَلْ لِي وَزِيرًا مِنْ أَهْلِي هَارُونَ أَخِي اشْدُدْ بِهِ أَزْرِي وَأَشْرِكْهُ فِي أَمْرِي كَيْ نُسَبِّحَكَ كَثِيرًا وَنَذْكُرَكَ كَثِيرًا إِنَّكَ كُنْتَ بِنَا بَصِيرًا قَالَ قَدْ أُوتِيتَ سُؤْلَكَ يَا مُوسَى

"Akasema: Ewe Mola Wangu! Nikunjulie kifua change. Na unifanyie wepesi jambo langu. Na ulifungue fundo lilo katika ulimi wangu.Wapate kufahamu kauli yangu. Na nipe waziri katika watu wangu.Harun ndugu yangu. Niongeze nguvu zangu kwaye. Na umshirikishe katika jambo langu. Ili tukutakase sana. Na tukukumbuke sana. Hakika Wewe unatuona. Akasema: Hakika umepewa maombi yako ewe Musa." (Qur'an, 20:25-36).

Huyu ndiye Nabii Musa namna alivyomuombea ndugu yake kupata nafasi hiyo, na Mwenyezi Mungu, bila ya kinyongo akatamka kwa uwazi kwamba amemkubalia maombi yake. Na tunafahamu kwamba pale ambapo Nabii Musa (a.s.) alipokuwa akisafiri,alikuwa akimuacha ndugu yake huyo kuwa Khalifa, ila ni kwamba Nabii Harun alifariki dunia kabla ya kaka yake, na lau kama ingekuwa kinyume chake, basi bila ya shaka yoyote pasingefanyika shura ya kumchagua Khalifa baada ya Nabii Musa (a.s.) kwani nafasi hiyo ingekuwa ni ya Nabii Harun kutokana na uteuzi huu wa Mwenyezi Mungu. Licha ya kwamba Nabii Harun alifariki mwanzo kabla ya Nabii Musa (a.s.), ni kwamba baada ya kifo cha Nabii Musa (a.s.) hapakuwa na uchaguzi, kwani nafasi ya uongozi baada yake ilikwisha ainishwa kwa wasii wake aliyekuwa akiitwa Joshua ibn Nuun.[45] Na hili mmelieleza wenyewe katika kitabu chenu cha kwanza, kama ifuatavyo: "Baada ya Nabii Musa na Harun (a.s.), nafasi ya uongozi ilishikwa na Joshua akisaidiwa na Kalebu."[46]

Kwa hivyo huu ndio utaratibu halali wa kumpata kiongozi katika Uislamu, na wala si suala la ukoo bali ni maandiko, kwani ni Mwenyezi Mungu Ambaye huiteuwa nyumba ya watu fulani na kutoa Manabii, Makhalifa na watu wengine wema kwa ajili ya maslahi ya jamiii zao, kama anavyosema katika Qur'ani:

إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَىٰ آدَمَ وَنُوحًا وَآلَ إِبْرَاهِيمَ وَآلَ عِمْرَانَ عَلَى الْعَالَمِينَ ذُرِّيَّةً بَعْضُهَا مِنْ بَعْضٍ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

[45] Tajil Arusi: Jz. 18, Uk. 565.
[46] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 1, Uk. 292.

> "Hakika Mwenyezi Mungu alimchagua Adam na Nuh na watoto wa Ibrahim na watoto wa Imran juu ya walimwengu wote. Ni kizazi cha wao kwa wao na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kujua." (Qur'an 3: 33 – 34).

Miongoni mwa wateule wa Mwenyezi Mungu ambaye si Mtume wala Khalifa wa Mtume ni Bibi Maryam (a.s.), Bibi ambaye historia inamtambua vyema juu ya nafasi yake ya kipekee aliyokuwa nayo, ikiwa hayo yamefanyika kwa Bibi huyo Mtukufu, basi ni kwa nini ionekane ni akili ya ajabu kwa Mwenyezi Mungu au Mtume kumuainisha Khalifa wa kuuongoza umma, na isionekane ajabu kwa Khalifa Abu Bakar kuacha wasia tena bila ya ushauri wa kumshauri mtu katika hilo kama wasomi hao walivyoeleza katika maudhui ya kuteuliwa Umar kuwa Khalifa?!

Pia suala la baba kuwarithisha watoto wao, limeombwa na Nabii Zakaria, baada ya kukaa kwa muda mrefu bila ya kupata mtoto, na alikuwa na khofu kubwa juu ya umma pindi atakapoondoka hakutakuwa na mtu atakayeendeleza kazi yake, alimuomba Mola wake kwa kusema:

وَإِنِّي خِفْتُ الْمَوَالِيَ مِنْ وَرَائِي وَكَانَتِ امْرَأَتِي عَاقِرًا فَهَبْ لِي مِنْ لَدُنْكَ وَلِيًّا يَرِثُنِي وَيَرِثُ مِنْ آلِ يَعْقُوبَ ۖ وَاجْعَلْهُ رَبِّ رَضِيًّا

> "Na mimi nahofia jamaa zangu baada yangu na mke wangu ni tasa. Basi nipe mrithi kutoka Kwako. Atakayenirithi mimi na arithi ukoo wa Ya'qub. Ewe Mola Wangu mjaaliye mwenye kuridhisha."(Qur'ani, 19:5-6).

Kama kawaida yake Mwenyezi Mungu hakumkaripia kutokana na ombi lake hili, bali alimwambia maridhawa kabisa:

يَا زَكَرِيَّا إِنَّا نُبَشِّرُكَ بِغُلَامٍ اسْمُهُ يَحْيَىٰ لَمْ نَجْعَلْ لَهُ مِنْ قَبْلُ سَمِيًّا

> "Ewe Zakariya! Hakika Sisi tunakubashiria mwana, jina lake ni Yahya, hatujapata kumpa jina hilo yeyote kabla yake." (Qur'ani,19:7).

Kuhusiana na Aya hii Sheikh Abdullah Saleh al-Farsy anasema: "Nabii Zakaria anamuomba Mola wake amruzuku mtoto mwema wa kuja kushika kazi yake atakapoondoka yeye."[47]

Pia Nabii Suleiman (a.s.) alirithi utawala kutoka kwa baba yake bila ya kuwepo kwa uchaguzi, jambo hili nalo mmelieleza wenyewe katika juzuu ya kwanza: "Utawala wa Bani Israil nchini Palestina ulikoma baada ya kutawafu Nabii Suleiman ambaye naye alirithi utawala huo kutoka kwa baba yake Nabii Daud (a.s.)"[48]

Ama kuhusiana na suala la haki ya Ahlul-Bayt(a.s.) kuwa ndio wenye haki ya kuwa Makhalifa baada ya Mtume (s.a.w.w.), pia ni jambo ambalo lililothibiti katika maandishi matakatifu, kwani ni Mwenyezi Mungu Ndiye aliyewatakasa watu wa ukoo wa Mtume (s.a.w.w.) pale aliposema:

إِنَّما يُرِيدُ اللهُ لِيُذْهِبَ عَنْكُمُ الرِّجْسَ أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيراً.

> Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaondosheeni uchafu enyi watu wa nyumba ya Mtume na kuwatakasa kabisa. (Qur'ani, 33:33).

[47] Tafsiri ya Qur'ani Tukufu: Uk.394.
[48] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Juzuu ya 1, Uk.295.

Hivi ndivyo ambavyo Mwenyezi alivyofanya kwa watu wa ukoo wa Mtume (s.a.w.w.), kama alivyofanya kwa Bibi Maryam (a.s.). Na wafasiri wote wa Qur'ani wamenukuu Hadithi mbalimbali zinazoashiria kwamba watu hao wa ukoo wa Mtume (s.a.w.w.) waliotakaswa na kila aina ya uchafu ni Imamu Ali ibn Abi Talib, Bibi Fatima, Imamu Hasan na Imamu Husein (a.s.). Na katika kusisitiza juu ya haki ya Ahlul-Bayt ya kushika uongozi, Mtume (s.a.w.w.) ameeleza bayana na kwa msisitizo juu ya kushikamana nao, kwani wao ndio kizito cha pili baada ya kile cha kwanza ambacho ni Qur'ani Tukufu, maneno hayo ya Mtume yamepokelewa katika Hadithi ifuatayo:

حدثني زهير بن حرب وشجاع بن مخلد جميعا عن بن علية قال زهير حدثنا إسماعيل بن إبراهيم حدثني أبو حيان حدثني يزيد بن حيان قال ثم انطلقت أنا وحصين بن سبرة وعمر بن مسلم إلى زيد بن أرقم فلما جلسنا إليه قال له حصين لقد لقيت يا زيد خيرا كثيرا رأيت رسول الله صلى الله عليه وسلم وسمعت حديثه وغزوت معه وصليت خلفه لقد لقيت يا زيد خيرا كثيرا حدثنا يا زيد ما سمعت من رسول الله صلى الله عليه وسلم قال يا بن أخي والله لقد كبرت سني وقدم عهدي ونسيت بعض الذي كنت أعي من رسول الله صلى الله عليه وسلم فما حدثتكم فاقبلوا وما لا فلا تكلفونيه ثم قال قام رسول

الله صلى الله عليه وسلم يوما فينا خطيبا بماء يدعى خما بين مكة والمدينة فحمد الله وأثنى عليه ووعظ وذكر ثم قال أما بعد ألا أيها الناس فإنما أنا بشر يوشك أن يأتي رسول ربي فأجيب وأنا ثقلين أولهما كتاب الله فيه الهدى والنور فخذوا بكتاب الله واستمسكوا به فحث على كتاب الله ورغب فيه ثم قال وأهل بيتي أذكركم الله في أهل بيتي أذكركم الله في أهل بيتي أذكركم الله في أهل بيتي...“

“Katuhadithia Zuhair ibn Harb na Shujaa ibn Makhlad wote kutoka kwa ibn Uliyyah. Kasema Zuhair: Katuhadithia Ismail ibn Ibrahim kuwa:Kanihadithia Abu Hayyan kuwa:Kanihadithia Yazid ibn Hayyan kuwa alisema: “Niliondoka mimi na Husain bin Sabra na Umar bin Muslim kwenda kwa Zaid ibn Arqam. Tulipokaa naye, Husain akamwambia: ‘Ewe Zaid! Kwa hakika umekuta kheri nyingi, umemuona Mtume (s.a.w.) na umesikia Hadithi zake na umekwenda vitani pamoja naye, na ukaswali nyuma yake, kwa hakika umekuta kheri nyingi ewe Zaid! Tuhadithie ewe Zaid yale ulioyasikia kutoka kwa Mtume(s.a.w.).’ Akasema (Zaid bin Arqam): ‘Ewe mwana wa ndugu yangu! Wallahi, miaka yangu imekuwa mikubwa (nimeshakonga), na umri wangu umekuwa mkongwe, na nimesahau baadhi ya yale niliokuwa nimeyahifadhi, basi nitachokusimulieni kikubalini na nisicho (kusimulieni) basi musinikalifishe.’ Kisha akasema: ‘Alisimama Mtume (s.a.w.) siku moja pamoja nasi akahutubia katika (sehemu yenye) maji yanayoitwa ‘Khumman’ baina ya Makka na Madina. Basi akamuhimidi Mwenyezi Mungu na kumsifu na akatoa mawaidha na kukumbusha. Kisha akasema:

> 'Baada ya hayo, Enyi watu! Hakika yangu mimi ni mtu (ambaye) amekaribia kunijia Mjumbe wa Mola wangu (Malaika wa kutoa roho) nami nitaitika**.** Nami nakuachieni vizito viwili. Cha kwanza: Ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu, Ndani yake kuna uongofu na nuru, basi kishikeni Kitabu cha Mwenyezi Mungu na mushikamane nacho. Basi akahimiza juu ya (kushikamana na) Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kuwataka (watu) wakipende. Kisha akasema: Na Ahlul-Bayti (watu wa nyumba yangu), nakukumbusheni Mwenyezi Mungu kuhusu watu wa nyumba yangu, nakukumbusheni Mwenyezi Mungu kuhusu watu wa nyumba yangu, nakukumbusheni Mwenyezi Mungu kuhusu watu wa nyumba yangu…'''[49]

Katika kuthibitisha zaidi maneno haya ya Mtume (s.a.w.w.) mfasiri maarufu wa Qur'ani, Ibn Kathir anasema:"Hakika imethibiti katika kitabu sahihi ya kwamba Mtume(s.a.w.w.) alisema katika khutba yake aliyoitoa Ghadir-Khum, ya kwamba:

إنّي تاركم فيكم الثقلين كتاب الله وعترتي وإنّهما لم يفترقا حتى يردا عليّ الحوض.

> "Hakika mimi ninawaachieni vizito viwili, Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Kizazi changu, na viwili hivyo havitaachana mpaka vitakaponifika katika Hodhi.»[50]

Hadithi hizi zitakuwa ni hoja kwa kila Mwislamu mwadilifu, ila tu kwa wale ambao watasema kwamba si sahihi kama walivyosema kuhusiana na Hadithi ya Tukio la Karatasi. Wale waliomzuia Mtume (s.a.w.w.) kuandika alichotaka kukiandika walitambua vy-

[49] *Sahihi Muslim* Jz. 7, Uk. 123
[50] *Tafsir Ibnu Kathir* Jz. 4, Uk. 122

ema kwamba Mtume (s.a.w.w.) alitaka kuandika yale aliyoyasema kwa ulimi wake mara kwa mara, kwamba haki ya uongozi ni ya watu wa nyumbani kwake, kwani tukiangalia ibara iliyomo katika Hadithi ya Vizito viwili inayosema kwa uwazi mwenye kushikamana na vizito viwili (Qur'ani na Ahlul-Bayt (a.s.)) katu hatopotea, na ile ibara iliyomo katika Tukio la Karatasi isemayo: "Nileteeni karatasi ya kuandika, na nitawaandikia tamko litalowapelekea kutopotea."

Napenda kuwafahamisha waandishi hao na Waislamu kwa ujumla, kwamba msingi mkubwa wa Ushia ni maandiko haya yaliyonakiliwa kutoka katika kinywa cha Mtume (s.a.w.w.). basi kama yanamaana nyengine kinyume na kushikamana na Ahlulbayti wa Mtume (s.a.w.w.), tunaomba tuelezwe kwa dalili za wazi, kwani sisi ni watu wa dalili, daima humili kule kwenye dalili.

Ni wazi kwamba wale waliozuia jambo hilo lisifanyike walitambua kwamba alitaka kuacha wasia wa uongozi kwa Ahlul-Bayt wake (a.s.), na wale waliokuwa katika hadhara ya Mtume (s.a.w.w.) walikuwa na tamaa ya kuwa viongozi baada yake, na hayo yanadhihiri pale tu baada ya Mtume (s.a.w.w.) kufariki dunia, ni namna gani walivyokimbilia katika ukumbi wa Saqifa bani Saida na kuuwacha mwili Mtukufu wa Mtume Mtukufu ukishughulikiwa na Ahlul-Bayt wake. Wanasema:

"Lakini hata kama ingekuwa hivyo tungetegemea (Uk. 324) watoto wa kiume wa Mtume wangekuwa hai ili kukamilisha mpango huu. Matumaini ya ukoo wa Mtume kuwa ndio ungeongoza, yanapotea ukizingatia hali ya ukoo wake haikuruhusu wapate uongozi. Ali akiwa na miaka thalathini hivi Abbas alikuwa na miaka kumi na tatu au kumi na nne na mwengine ni Abu Sufiyan aliyesilimu mwakawa nane waHijiria (Mwaka wa Fat-hu Makka) hivyo ni dhahiri pamoja na kuwa ukoo wa Mtume ulikaa kujadili uongozi, sawa, walikuwa na haki hiyo kama Waislamu wengine walipaswa

wajitokeze, lakini kukaa kama ukoo wa Mtume haikuwa sahihi. Inashangaza zaidi katika ule utaratibu wa kuahidiana waliojipangia Hassan na Muawiya kuwa Muawiya atakapokufa Ukhalifa uende kwa mdogo wake Husein, hasa kwa vile ni mjukuu wa Mtume (s.a.w.), lakini vile vile kama Mtume angeacha usia kuwa awe fulani ingekuaje baada ya yule fulani kufa? Kwa kuwa Mtume hawakilishwi katika utume wake na uteuzi wake ungekuwa na ukomo kwa yule aliyemteuwa tu, wakati dola na watu vipo daima hadi siku ya mwisho isingewezekana kwa Mtume kuacha usia. Ni hivyo hivyo kwa ukoo wa Mtume unaukomo, ingefikia mahali ingebakia historia tu kama ilivyo leo watu wanajiita masharifu kwa kisingizio kuwa wana ukoo wa Mtume. Kwa kuwa ukoo wa Mtume ungekoma kama koo nyingine zilizoishi hapa duniani zimetoweka na kwa kuwa dola ingeendelea kuwepo hadi mwisho wa dunia basi asingefanya usia kwa mtu yeyote katika ukoo wake."[51]

Kuhusiana na kauli yao hii, majibu yetu ni kama yafuatavyo:

Ni wazi kwamba watoto wa Mtume (s.a.w.w.) walikuwa hai kama tutakavyobainisha, au kwa kauli nyingine ni kwamba wale waliokusudiwa kushika Ukhalifa mara baada ya kifo cha Mtume (s.a.w.w.) walikuwa hai, na wala katika jambo hili halimhusu Abu Sufiyani, mtu ambaye alitumia mali yake na nguvu zake kuupiga vita Uislamu, na mwisho wake akalazimika kusilimu kwa kukosa budi wakati wa ukombozi wa mji wa Makka. Ama kuhusiana na Imamu Ali (a.s.) kuambiwa alikuwa hakustahiki nafasi hiyo kwa sababu ya umri wake, hili si sahihi, kwani umri wake wakati huo ulikuwa ni sawa na umri aliokuwa nao Nabii Isa (a.s.), pale alipopewa majukumu ya kuwalingania watu Dini ya Mwenyezi Mungu, na zaidi ya hayo, Hadithi mbalimbali za Mtume (s.a.w.w.) zinaashiria kwamba yeye ndiye wasii na mrithi wake, na hilo walilitambua wale waliom-

[51] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.324-325.

zuilia Mtume (s.a.w.w.) asiandike wasia wake, na wale waliokimbilia Saqifa kabla ya Mtume (s.a.w.w.) kuoshwa na kuzikwa, kwani walitambua Ali ibn Abi Talib kamwe hawezi kuuwacha mwili wa Mtume (s.a.w.w.) na kwenda kuzozana kwa ajili ya madaraka.

Na tumeeleza kwamba, umri mkubwa aliokuwa nao Abu Bakar haukuwa kigezo cha kufuata haki, kwani alilazimika katika baadhi ya wakati kufuata mawazo ya waziri wake hata kama mawazo ya waziri huyo yalikhalifu mafunzo ya Uislamu, kama tulivyoeleza katika kisa cha watu wanaostahiki kupewa Zaka.

Tunasisitiza tena kwamba ukoo wa Mtume (s.a.w.w.) haukukaa kujadili uongozi, bali kilichowaweka pamoja ni kuushughulikia mwili wa Mtume (s.a.w.w.), kama Sheikh Abdalla Saleh Farsiy alivyoeleza, ni kwamba palitokea matendo mawili wakati mmoja: Wengine walikuwa wakimuosha Mtume (s.a.w.w.) na wengine walikuwa katika ukumbi wa Saqifa wakigombania uongozi. Ama kikao walichokaa kilikuwa ni kujadili namna watu walivyofanya, wamechaguana baada ya kuwa jambo hilo tayari Mtume (s.a.w.w.) alikwisha lielezea, na kama si hivyo ilikuwaje wakachaguana bila ya wao kushirikishwa,walijadili namna ya kuirudisha haki hiyo kwao, hichi ndicho kilichofanyika.

Ama kuhusu kuambiwa kwamba ukoo wa Mtume ungekwisha na kukoma kama koo nyingine, kwa kweli huku ni kumhuzunisha Mtume (s.a.w.w.) kama vile Wail ibn Aswi alivyomhuzunisha kwa kumuambia ni mkiwa (aliyekatikiwa na kizazi), Mwenyezi Mtukufu alimjibu kafiri huyo kwa kumliwaza Mtume Wake kwa kuteremsha Sura inayomuelezea kwamba adui yake ndiye atakayekatikiwa na kizazi, ama Mtume Wake atakuwa na watoto wengi.

Pia Hadithi zinazobainisha ya kwamba kabla ya dunia hii kumalizika, Mwenyezi Mungu atamleta mtu anayetokana na kizazi cha

Mtume (s.a.w.w.) ambaye ataijaza dunia uadilifu na haki baada ya kujaa dhulma na jeuri. Mtu huyo anatambuliwa kwa jina la Imamu Mahdi, ambaye atakuwa katika zama moja na Nabii Isa (a.s.), sasa ikiwa mtu huyo hajazaliwa kwa mujibu wa itikadi ya maulamaa wa wengi wa Kiahli Sunna, ni vipi tuambiwe ukoo wa Mtume umefikia ukomo na wale wanaojiita masharifu, kwa maana ya kujinasibisha na nasaba ya Mtume (s.a.w.w.) wasiwe wakweli. Khofu yangu katika hili ni kwa wasomi hao kutuambia kwamba Hadithi hizo zilizomo katika baadhi ya vitabu sahihi si sahihi! Na ikiwa watasema ni sahihi, basi si sahihi kusema ukoo wa Mtume (s.a.w.w.) umekatika na hawa masharifu ndio ambao mmoja wao atamzaa huyo Imamu Mahdi.

Na zaidi ya hayo tumsikilize tena Sheikh Abdallah Saleh al-Farsiy, ambaye ni mwenye kuheshimika na kukubaliwa na Waislamu wengi hapa Afrika Mashariki wakiwemo Waislamu wa Bakwata na wale wa Wizara ya elimu Zanzibar ambao nadhani hawajui vitabu hivi vinavyosomeshwa vijana wasio na uwezo wa kufanya utafiti vimeandikwa nini ndani yake, anasema:

> "Kizazi cha Sayyidnal Hasan kimetangaa zaidi Misri na Kaskazini yote ya Afrika na Asia Minor na kusini mwa Urusi, Afghanistan, Hijaz, Sham na Yaman. Na kizazi cha Sayyidnal Husein kimetangaa sana Hadhramout na kulikokuwa kukiitwa Indonesia, Malay, Filipine na Mashariki ya Afrika yote hii na visiwa vyake na Bara Hindi."[52]

Baadhi ya Hadithi zinazoelezea kwamba dunia hii haitomalizika mpaka atakapotokea Kiongozi wa mwadilifu anayetokana na familia ya Mtume (s.a.w.w.) ni kama zifuatazo:

[52] Maisha ya Sayyina Hasan: Uk.43-44.

يملك الناس رجل من أهل بيتي, اسه اسمي واسم أبيه اسم أبي, يملأ الأرض عدلا وقسطا كما ملئت ظلما وجورا.

"Mtu katika Ahlul-Bayt wangu atawatawala watu, jina lake ni kama jina langu, na jina la baba yake ni kama jina la baba yangu, ataijaza ardhi uadilifu na haki, kama ilivyojazwa dhulma na jeuri"[53]

لايذهب الدنيا حتى يلي رجل من أهل بيتي يملأ الأرض قسطا و عدلا كما ملئت ظلما وجورا,يواطئ اسه اسمي.

"Dunia haitomalizika mpaka atokee mtu miongoni mwa Ahlul-Bayt wangu, aijaze ardhi haki na uadilifu kama ilivyojazwa dhulma na jeuri, jina lake linafanana na jina langu."[54]

Pia imepokewa kutoka kwa Ummi Salama akisema: Mtume (s.a.w.w.) aliingia kwa Ali huku akiwa amefurahi, kisha akasema: Je, nikupeni habari njema? Ni kwamba Mahdi anatokana na mtoto wa Fatima."[55]

المهدي منا أهل البيت يصلحه الله في ليلة واحدة.

Mahdi anatokana na sisi Ahlul-Bayt, Mwenyezi Mungu atampa uwezo wa kutengeneza mambo katika usiku mmoja.[56]

---

[53] Al-Khatib Baghdad, *Tarikhu Baghdad*: Jz. 1, Uk. 278.
[54] Tabraniy, Almu'jamul Kabir: J10, Uk.134.
[55] Al-Mazziy, Tahdhibul kamali: J.9,Uk.347, Dhahabiy: Siyaru A'lami Annubalai: J.10, Uk.663.
[56] Musnad Ahmad: J.1, Uk.84. Sunanu ibn Majah: J.2, Uk.137.

Hadithi hizi zinatufunza mambo yafuatayo:

a. Ikiwa Mtume (s.a.w.w.) alimuainisha Kiongozi atakayetawalia mambo ya Waislamu, baada ya kupita miaka mingi ya kifo chake, (kifo cha Mtume (s.a.w.w.), ambaye atatawala bila ya kuwepo shura, ni kwa nini Waislamu wengine wadiriki kusema kwamba Mtume (s.a.w.w.) hakueleza ni nani atawale mara tu baada ya kifo chake!

b. Mtume (s.a.w.w.) ameeleza wasifu wa Kiongozi huyo atakaye tawala mambo ya Waislamu mwishoni mwa dunia.

c. Kama vile ambavyo Mtume (s.a.w.w.) alivyobainisha kwamba ametuachia vizito viwili: Kitabu cha Mwenyezi Mungu naAhlul-Bayt wake, ameeleza wazi kwamba Kiongozi huyo wa mwisho, pia atatokana na kizazi chake.

d. Suala la Uongozi katika Uislamu ni la Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na ni juu ya Mwislamu kukubali na kutii uteuzi wao pasi na pingamizi yeyote.

Zaidi ya haya, ni kwamba pale Ibn Kathir alipojaribu kuisherehesha Hadithi isemayo kwamba viongozi baada ya Mtume (s.a.w.w.) ni kumi na mbili, alimtaja Imamu Mahdi (a.s.) kuwa ni miongoni mwao.[57]

Hiyo shura iko wapo? Na mbona haionekani kuwani akili ya ajabu? Na ni vipi mdiriki kusema kwamba ukoo wa Mtume (s.a.w.w.) umekatika na ilhali Khalifa wa mwisho anatokana na kizazi cha Mtume (s.a.w.w.)?!

Na katika urithi mkubwa tuliojaliwa kuwa nao hapa kwetu Tanzania, ni makaburi yaliyoko Bagamoyo katika kijiji cha Kaole, umuhimu wa makaburi hayo si jengine, bali ni kwamba waliolala

[57] Ibn Kathir, Tafsirul Qur'anil Karim: J2, Uk.24.

ndani yake ni Masharifu, kutokana na utukufu wao waliweza kumuomba Mola wao ayabadilishe maji ya kisima yaliyokuwa na ladha ya chumvi na kuwa matamu.  Leo kisima hicho ni pekee kilicho na maji matamu katika eneo hilo, na kubwa zaidi ni kwamba hayazidi na wala hayapungui kina chake!  Sijui na hili watalipinga na kudai kwamba makaburi hayo si ya Masharifu!

Katika kuzidi kupinga haki ya Ukhalifa kwa Ahlul Bayt wa Mtume (s.a.w.w.), wamesema yafuatayo:

"Katika Uislamu ukoo huhesabiwa kwa mwanaume, udugu kwa mfano wa Mtume na Ali haumfanyi Ali awe na damu ya Utume hivyo ahusike na Utume, hivi sio kweli na hili ni maarufu. Pengine kwa kujua hivi ndiyo sababu ya kutoachwa hai mtoto yeyote wa kiume wa Muhammad (s.a.w.).Watoto wa Fatuma binti ya Muhammad kwa msingi huu ni kweli Muhammad ni babu yao wa kikeni, lakini ukoo wao unahesabiwa kwa babu yao wa kiumeni."[58]

Majibu kuhusiana na maneno yao haya ni kama yafuatavyo:

Miongoni mwa mapinduzi makubwa yaliyofanywa na Uislamu ni kumkomboa mwanamke na kumuondoshea ile hali ya mfumo dume iliyokuwepo katika zama za kijahilia, kwani Warabu walifikia katika kiwango cha juu cha ukatili dhidi ya mwanamke, walikuwa wakiwazika watoto wakike wakiwa hai, kuwarithi mama zao wa kambo na kuwatendea aina mbalimbali za udhalimu, mpaka wakakawa wanasema:

"بنونا بنو أبنائنا, وبناتنا بنوهن أبناء الرجال الأبعاد."

> "Watoto wa watoto wetu wa kiume nao ni watoto wetu, na watoto wa watoto wetu wa kike ni watoto wa watu wengine."[59]

[58] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.325.
[59] *Mughnil Labib*: Jz. 2, Uk. 452.

Hivi ndivyo walivyokuwa Warabu majahili, ama Uislamu uko kinyume kabisa na nadharia hiyo ya kijahilia, kwani Qur'ani Tukufu imewanasibisha watoto wa mtoto wa kike kuwa ni watoto wa babu yao. Hebu tusome Aya hizi Tukufu:

وَتِلْكَ حُجَّتُنَا آتَيْنَاهَا إِبْرَاهِيمَ عَلَى قَوْمِهِ نَرْفَعُ دَرَجَاتٍ مَنْ نَشَاءُ إِنَّ رَبَّكَ حَكِيمٌ عَلِيمٌ وَوَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ كُلًّا هَدَيْنَا وَنُوحًا هَدَيْنَا مِنْ قَبْلُ وَمِنْ ذُرِّيَّتِهِ دَاوُودَ وَسُلَيْمَانَ وَأَيُّوبَ وَيُوسُفَ وَمُوسَى وَهَارُونَ وَكَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ وَزَكَرِيَّا وَيَحْيَى وَعِيسَى وَإِلْيَاسَ كُلٌّ مِنَ الصَّالِحِينَ

> "Na hiyo ndiyo hoja Yetu tuliyompa Ibrahim juu ya watu wake. Tunamuinua kwa vyeo yule tumtakaye. Hakika Mola Wako ndiye Mwenye hekima, Mjuzi. Na tukamtunukia (Ibrahim) Is-haq na Yaqub; kila mmoja tulimuongoza. Na Nuh tulimwongoza zamani. Na katika kizazi chake Daud na Suleiman na Ayyub na Yusuf na Musa na Harun. Na kama hivyo tunawalipa wafanyao mema. Na Zakariya na Yahya na Isa na Ilyas; wote ni katika wema." (Qur'ani, 6:83-85).

Katika Aya hizi tunaona namna Mwenyezi Mungu anavyomnasibisha Nabii Isa (a.s.) kuwa ni miongoni mwa kizazi cha Nabii Ibrahim (a.s.), huku tukielewa kwamba Nabii Isa (a.s.) hana baba, kwa hivyo unasaba uliomo kati yao ni kwa upande wa mama tu ambaye ni Bibi Maryam (a.s.) Qur'ani Tukufu imeeleza kwa uwazi kwamba yeye (Nabii Isa) ni katika watoto wa Nabi Ibrahim (a.s.)

Aya nyingine ni hii:

فَمَنْ حَاجَّكَ فِيهِ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ فَقُلْ تَعَالَوْا نَدْعُ أَبْنَاءَنَا وَأَبْنَاءَكُمْ وَنِسَاءَنَا وَنِسَاءَكُمْ وَأَنْفُسَنَا وَأَنْفُسَكُمْ ثُمَّ نَبْتَهِلْ فَنَجْعَلْ لَعْنَتَ اللَّهِ عَلَى الْكَاذِبِينَ

> "Na watakaokuhoji baada kukufikia elimu hii, waambie: Njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu, na wanawake zetu na wanawake wenu, na nafsi zetu na nafsi zenu, kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo." (Qur'an, 3:61).

Aya hii iliteremshwa baada ya Mtume (s.a.w.w.) kuwaeleza wakiristo wa Najran (Yemen) kwamba Nabii Isa (a.s.) si mtoto wa Mwenyezi Mungu kwa kuwapa dalili mbalimbali za kiakili, lakini wakristo hao wakabakia na ubishi wao, ndipo hatimaye Mwenyezi Mungu akamtaka Mtume Wake (s.a.w.w.) afunge mjadala, na watakaohoji, awaambie wakusanyike na kila upande waje na watoto wao, wanawake zao na wao wenyewe.  Kwa mujibu wa wafasiri wa Qur'ani na wanahadithi ni kwamba kwa upande wa watoto, Mtume (s.a.w.w.) aliwachukua Hasan na Husein. Tunaelewa kwamba wajukuu hao wawili wa Mtume (s.a.w.w.) ni kwa upande wa binti yake Fatima (a.s.) Na zaidi ya haya, tumsikilize tena Sheikh Abdulla Saleh al-Farsiy anavyosema kuhusiana na uhusiano wa Husein ibn Ali (a.s.) na Mtume s.a.w.w:

"Ingawa anakuwa mjukuu hasa wa Mtume kwa mama yake, anakuwa vilevile mtoto wa ibn aami yake Mtume, anakuwa jamaa kwa kukutana kwa Bwana Abdul Muttalib ambaye ni babu wa Mtume na babu wa baba yake Sayyidnal Husein. Amekuwa kama hivyo walivyozalikana baadhi ya Mitume, wenyewe kwa wenyewe, hata akasema Mwenyezi Mungu:*DHURRIYYATAN BAADHUHAA MIN BAADH*."[60]

[60] Maisha ya Sayyidna Husein: Uk.17.

Wanaendelea kusema:

“Vile vile dola ya Kiislamu ni ya dunia nzima, ni mawazo butu kudhania na kushikilia kuwa ukoo wa Mtume ambao kimsingi haupo ungeweza kugawanywa duniani kote na kuendesha dola mbali mbali za Kiislamu. Udhaifu huu pamoja na maelezo yaliotangulia yamefanya iwe vigumu kwa Mtume kuwa ameacha usia unaohusu ukoo wake au mwingine yeyote. Mtume (s.a.w.) hakuacha usia wa nani awe kiongozi baada ya kutawafu kwake kwa sababu aliwaachia Waislamu wateue na kuchagua kiongozi wao kwa kutumia vipaji vyao kupitia maamuzi yanayohusu Uislamu wao. Katika uhai wake Mtume (s.a.w.) aliwafundisha Waislamu kuhusu uwongozi katika dola ya kiislamu, lakini utawala na Ukhalifa ni wa watu wote, hakuna mwenye haki ya kuzuia mwingine kutawala kama aya ya 55 ya sura 24 inavyobainisha.” Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya wale kabla yao… (24: 55).

Ukiachilia mbali kuwa uongozi ni wa watu wote, Mtume vile vile amefundisha maana, umuhimu na hali ya kutawala kuwa madaraka, milki, hukumu au uwezo mtu alionao katika ardhi na vilivyomo amepewa na Allah (s.w.), nafasi yake hapa duniani ni mdhaminiwa tu, sio mtawala wa hivyo, kwa sababu hiyo, hana madaraka ya kutawala atakavyo, amuwakilishe Muumba na atawale kufuatana na maagizo yake:

“Na hakika tumekukalisheni katika ardhi na tumekuwekeeni humo vitu vyote vinavyohitaji maisha yenu… (7:10).

“…Hata Mola wenu atamuangamiza adui na kukufanyeni watawala katika nchi (hizi na aone jinsi mtakavyofanya (7: 129).

“Na kumbukeni (Mwenyezi Mungu) alivyokufanyeni Makhalifa baada ya Adi na kukuwekeni vizuri katika ardhi… (7:74).

Taifa lolote lenye mamlaka juu ya sehemu ya ardhi ni kaimu wa Mwenyezi Mungu:

"Yeye ndie aliyekufanyeni manaibu katika ardhi (35: 39).

Kwa yote hayo wote wanajukumu la kusimamisha uadilifu siyo ukoo wa Mtume tu.

"Kwa hakika tuliwapeleka Mitume wetu kwa dalili waziwazi na tukaviteremsha vitabu na uadilifu pamoja nao ili watu wasimamie uadilifu (57: 25).

Hivyo kwa makusudi Mtume (s.a.w.) hakuacha uteuzi wowote wa nani ashike uongozi baada ya kutawafu kwake kwa kuwa amewacha mafunzo ya kudumu ya namna ya kupata viongozi, watu wachaguwe wenyewe kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu."[61]

Kwa kweli hayo tuliyoyaeleza ndio mawazo sahihi na simawazo butu, kwani hata kama Waislamu wanatofautiana juu ya mtu wa mwanzo ambaye alistahiki kuwa Khalifa baada ya Mtume (s.a.w.w.). lakini wanakubaliana yakwamba Khalifa wa mwisho wa umma huu atakuwa anatokana na ukoo wa Mtume (s.a.w.w.), ambaye ni Imamu Mahdi kama tulivyolithibitisha hilo katika Hadithi sahihi, kwa hivyo ukoo wa Mtume (s.a.w.w.) haujakatika, na mwisho wake ni pale itakapokosekana Qur'ani katika ulimwengu huu, kwani pale Mtume (s.a.w.w.) alipotuachia vizito viwili (Qur'an na watu wa ukoo wake), alisema kwamba viwili hivyo havitaachana mpaka pale vitakapomfikia katika hodhi lake (Siku ya Kiyama). Kwa hivyo si jambo ambalo haliwezekani kwa Mtume kuacha wasia wa uongozi kwa watu wa ukoo wake, na hili halipingani na ile fikra ya kwamba dola ya Kiislamu ni ya ulimwengu mzima na inayotakiwa iwepo katika zama zote hadi kitakaposimama Kiyama.

---

[61] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.325-326.

Lau kama Mtume (s.a.w.w.) aliwafundisha Waislamu njia ya kuchagua Khalifa kinyume na njia ya kuusia, basi tungeona njia hiyo ikitumika katika kuwapa hao Makhalifa, kwa kuanzia katika ukumbi wa Saqifa, lakini hata hiyo inayoitwa shura, haikufanyika, kama Umar ibn Khattab anavyokiri kwa kusema: "Kubaiwa kwa Abu Bakar lilikuwa ni jambo la kushtukiza, Mwenyezi Mungu aliwakinga Waislamu, na atakaye rudia kama hivyo, muuweni, au alisema: Yeyote yule atakayefanya kampeni kama hiyo asipewe baia wala yule aliyembai."[62]

Hii hali ya kila Khalifa kuchaguliwa kinamna yake, kama walivyoeleza, ni dalili ya wazi ya kwamba njia hizo hazina msingi katika Uislamu, bali ni njia zilijitokeza kwa mujibu wa mazingira katika kila zama na baadaye kurasimishwa. Na lau kama wangetwaa madaraka kwa njia nyingine, pia nayo wangesema kwamba ni utaratibu unaokubalika katika Uislamu, lakini wakati huohuo wanadai kwamba Imamu Ali (a.s.) hakuchaguliwa kwa utaratibu wa Kiislamu! Ama kuhusiana na Aya walizozitolea ushahidi katika kuitilia nguvu hoja yao, ni kwamba watu wote hawawezi kuwa Makhalifa kwa maana ya kushika uongozi katika jamii fulani, bali kwa idadi yoyote ya watu itakavyokuwa kubwa, kiongozi huwa mmoja, kwani hata pale Mwenyezi Mungu aliposema kwamba:

وَنُرِيدُ أَنْ نَمُنَّ عَلَى الَّذِينَ اسْتُضْعِفُوا فِي الْأَرْضِ وَنَجْعَلَهُمْ أَئِمَّةً وَنَجْعَلَهُمُ الْوَارِثِينَ

"Na tunataka kuwafadhili waliodhoofishwa katika ardhi na kuwafanya wawe ni viongozi na kuwafanya ni warithi." (Qur'ani, 28:5).

[62] *Sahih Bukhar*, Jz. 4, Uk. 127.

Tukitolea mfano wa watu waliodhoofishwa katika nchi, ni Mayahudi wa zama za Nabii Musa (a.s.), lakini ilipowajia nusura ya Mwenyezi Mungu, sio wote walikuwa viongozi, bali alikuwa ni Nabii Musa mwenyewe, na pale alipokuwa akiondoka alikuwa akimuachia majukumu ya uongozi ndugu yake ambaye alimuomba Mwenyezi Mungu ampe nafasi hiyo ya usaidizi wa uongozi wa jamii ile, na kabla ya kufariki alimuusia Yusha ibn Nuun kuwa wasii wake, hapakuwa na ile inayodaiwa shura au njia nyingine kinyume na hii. Kwa hivyo ni vyema Aya hizo zifahamike kama ambavyo Mwenyezi Mungu alivyokusudia.

Na hata pale wana wa Israil walipoamua kuingia katika mapambano kwa ajili ya kutetea haki zao na baadhi ya vitu vyao vya thamani vilivyoporwa, walikwenda kwa Nabii wao ili awateulie mtu wa kuongoza mapambano hayo, hawakukaa tu na kumchagua, Mwenyezi Mungu analieleza jambo hilo katika Kitabu chake Kitukufu kwa kusema:

أَلَمْ تَرَ إِلَى الْمَلَإِ مِنْ بَنِي إِسْرَائِيلَ مِنْ بَعْدِ مُوسَىٰ إِذْ قَالُوا لِنَبِيٍّ لَهُمُ
ابْعَثْ لَنَا مَلِكًا نُقَاتِلْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ □ قَالَ هَلْ عَسَيْتُمْ إِنْ كُتِبَ عَلَيْكُمُ
الْقِتَالُ أَلَّا تُقَاتِلُوا □ قَالُوا وَمَا لَنَا أَلَّا نُقَاتِلَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَقَدْ أُخْرِجْنَا مِنْ
دِيَارِنَا وَأَبْنَائِنَا □ فَلَمَّا كُتِبَ عَلَيْهِمُ الْقِتَالُ تَوَلَّوْا إِلَّا قَلِيلًا مِنْهُمْ □ وَاللَّهُ عَلِيمٌ
بِالظَّالِمِينَ وَقَالَ لَهُمْ نَبِيُّهُمْ إِنَّ اللَّهَ قَدْ بَعَثَ لَكُمْ طَالُوتَ مَلِكًا □ قَالُوا أَنَّىٰ
يَكُونُ لَهُ الْمُلْكُ عَلَيْنَا وَنَحْنُ أَحَقُّ بِالْمُلْكِ مِنْهُ وَلَمْ يُؤْتَ سَعَةً مِنَ الْمَالِ □
قَالَ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَاهُ عَلَيْكُمْ وَزَادَهُ بَسْطَةً فِي الْعِلْمِ وَالْجِسْمِ □ وَاللَّهُ يُؤْتِي
مُلْكَهُ مَنْ يَشَاءُ □ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ

> "Je, Hukuona wakubwa wa wana wa Israil baada ya Musa walipomwambia Nabii wao: Tuwekee mfalme ili tupigane katika njia ya Mwenyezi Mungu. (Mtume wao) akasema: Je, haielekei kuwa hamtapigana mtakapoandikiwa kupigana? Wakasema: Itakuwaje tusipigane katika njia ya Mwenyezi Mungu na hali tumetolewa nje ya majumba yetu na watoto wetu? Walipoandikiwa kupigana, wakageuka isipokuwa wachache miongoni mwao. Na Mwenyezi Mungu anawajua madhalimu. Na Nabii wao akawaambia: Hakika Mwenyezi Mungu amewachagulia Jalut kuwa mfalme. Wakasema: Vipi atakuwa na ufalme juu yetu, na hali sisi tunastahiki zaidi ufalme kuliko yeye, naye hakupewa wasaa wa mali? Akasema: Hakika Mwenyezi Mungu amemteua juu yenu na amemzidishia ukunjufu wa elimu na kiwiliwili. Na Mwenyezi Mungu humpa ufalme Wake amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa, Mjuzi." (Qur'an 2: 246 – 247).

Aya inatubainishia kwa uwazi kabisa namna ufalme wa mbinguni unavyoingilia hata katika kumteua kamanda wa vita, kama inavyosema: "**Hakika Mwenyezi Mungu amewachagulia Talut kuwa mfalme.**" Na pia inaelezea sababu za kupewa mamlaka hayo baada ya watu wengine kuhoji uteuzi huo wa Mwenyezi Mungu: "**Mwenyezi Mungu amemteua yeye juu yenu na amemzidishia ukunjufu wa elimu na kiwiliwili.**"

Sasa kama kweli Waislamu wanataka kuwa na kiongozi, basi na watazame sifa hizi alizozieleza Mwenyezi Mungu katika Aya hii, sifa hizo ni kuwa na upeo mkubwa wa elimu na nguvu za kiwiliwili, kwa maana ya ushujaa. Na lau kama sifa hizi zingepewa nafasi katika ukumbi wa Saqifa bila ya shaka ambaye angeibuka mshindi tena bila ya kuwa na mpinzani ni Imamu Ali ibn Abi Talib (a.s.), kwani yeye ndiye aliyewakata vichwa majemedari wakubwa wa kishirikina kutokana na ushujaa wake uliokuwa hauna kifani, ni yeye ndiye peke yake aliyesimama kishujaa kuwa tayari kupambana na Amru

ibn Abdi Wuddi baada ya wengine kukhofia maisha yao, yeye ndiye aliyepewa bendera katika vita vya Khaybar baada ya wale waliopelekwa mwanzo kutorudi na ushindi, aliweza kuingia Khaybar na kurudi na ushindi mnono, yeye ndiye Simba wa Mwenyezi Mungu mwenye kushinda. Pia tunasikia wasomaji wa kasida wakisoma: "Sayyidna Ali na Mikidadi, ndio mashujaa wa lioshinda Jihadi."

Ama kwa upande wa elimu, Mtume (s.a.w.w.) alimuelezea kwamba ni yeye ndiye mlango wa mji wa elimu yake: "Mimi ni mji wa elimu na Ali ni mlango wake."[63] Yeye ndiye ambaye Umar alisema: "Lau kama si Ali, basi Umar angeangamia."[64] Pia alisema: "Najilinda kwa Mwenyezi Mungu, ili nisipate tatizo (la kielimu) wakati ambapo baba wa Hasan (Imamu Ali (a.s.)) hayupo."[65] Yeye ndiye ambaye ni marejeo ya elimu zote za Kiislamu, yeye ndiye aliyethubutu kusema: Niulizeni kabla hamjanikosa."[66]

Kwa hivyo huyu ndiye mtu mwenye kila sifa ya kuwa Khalifa baada ya Mtume (s.a.w.w.), lakini kama vile ambavyo watu hawakuridhika juu ya uteuzi wa kumteuwa Jaluti kuwa kiongozi, hali ni hiyo hiyo kwa upande wa wasii wa Mtume (s.a.w.w.).

[63] Ibn Arabiy, *Tafsiru Ibn Arabiy*: Jz. 1, Uk. 422. Al-Aalusiy, *Yafsirul-Aalusiy*: Jz. 25, Uk. 61.
[64] Al-Qanduziy, *Yanaabihul Mawaddati*: Jz. 1, Uk. 216.
[65] Ibn Hajar, *Fat-hul Baariy*: Jz. 13, Uk. 286. Ibn Athir, *Asadul Ghaba*: Jz. 4, Uk. 23.
[66] Ibn Asakir, *Tarikhu madinatu Dimishqi*: Jz. 17, Uk. 335.

# UTEUZI WA MAKHALIFA WENGINE

Baada ya waandishi hao kuelezea uteuzi wa Khalifa wa kwanza wanaendelea kueleza namna Makhalifa wengine walivyopatikana. Katika maudhui waliyoyapa kichwa cha habari kisemacho **'Utaratibu wa kupata Viongozi katika Uislamu.'** wameandika yafuatayo:

"Kwa kuwa tumeanza na namna Abubakar alivyochaguliwa na tumegusia tofauti zilizopo leo hii kuhusiana na uchaguzi huo ni vyema tukamilishe mada ya namna viongozi walivyopatikana katika Uislamu katika kipindi cha Makhalifa wanne.

Mtume (s.a.w.) hakusema kwa maneno lakini alisema kwa vitendo. Kumchagua Abubakar kuwa Imam wa msikiti na kutoruhusu mtu mwingine kuswalisha na aliposwalisha mtu mwingine swala ilirudiwa ni dhahiri kwa maoni yetu Mtume (s.w.w.) alikuwa amependekeza kuwa kiongozi awe Abubakar na akawaachia Waislamu kumkubali au kumkataa. Tunaamini kuwa Abubakar alimuelewa hivi Mtume (s.a.w.) ndio maana alipokaribia kutawafu aliwaita wajumbe wa shura na kushauri kuwa yeye anampendekeza Umar awe ndiye Khalifa baada ya kifo chake. Wajumbe wa shura walipokubali ndipo akamwambia Ali aandike usia huo. Abubakar alifanya hivi kwa ijtihadi yake ambayo inakubalika katika Uislamu na hasa akizingatia hali ilivyokuwa mara Mtume alipofariki, Waislamu walipogawanyika makundi matatu, hivyo alitumia njia hii ambayo ni ya Kiislamu, hakuiburuza shura na kulikuwa na mjadala kabla ya kukubalika rai hiyo. Wajumbe maarufu wa shura walikuwa Umar, Uthman, Ali, Abdul Rahman bin Auf, Muadh bin Jabal, Ubay bin Kaab, Zayd bin Thabit na wajumbe wengine mashuhuri kutoka muhajirina na Ansar. Abubakar alitoa pendekezo lake la kumteuwa Umar kuwa Khalifa

wa pili, wote walikubali ila walieleza wasiwasi wao juu ya ukali wa Umar, hii ndiyo hoja pekee iliyotolewa na Ali na Talha. Abubakar aliikataa hoja hii kwa kuwafahamisha kuwa Ukhalifa utamfanya asiwe mkali, kwa kuwa hoja dhidi ya Umar ilikuwa hii tu basi pendekezo likakubalika.

Hatua iliyofuata ambayo imeimarisha uhuru wa kuchagua viongozi ni kuwahutubia Waumini katika msikiti wa Mtume, akisaidiwa na jamaa zake alisimama kwenye membari, kwanza alitaka ule usia usomwe mbele ya watu wote waliokuwa msikitini na yeye azungumze nao. Usia wenyewe ulikuwa kama ifuatavyo:

"Bismillahi Rahman Rahiim. Hili ni tamko lililofanywa na Abubakar bin Abi Quhafah ambaye yuko karibu na kwenda akhera. Wakati wa kuwa katika hali ya kufa hata kafiri humuamini Mwenyezi Mungu, na hata mfanya madhambi hutubia (hurudi kwenye imani yake) na kafiri humtegemea Allah. Nimefanya kila jema kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kwa kuboresha dini yake na kwa manufaa kwa Waislamu na kwa mimi mwenyewe katika kuteuwa Umar kuwa Khalifa. Nategemea atakuwa muaminifu na mtekelezaji haki lakini akibadilika na kuwa dhalimu mimi sina lawama kwa kuwa sina elimu ya ghaib. Kila mmoja anawajibika kwa afanyalo."

Baada ya usia huu kusomwa, Abubakar alipanda kwenye membari huku akisaidiwa na kuuhutubia umma kama ifuatavyo:

''Enyi ndugu zangu, sikumchagua kuwa Khalifa ukoo wangu au ndugu zangu. Nimemteuwa aliye bora miongoni mwenu mnakubaliana na uteuzi wangu?'' Wote waliitikia kwa kukubali.

S.A. Husein anasema wote waliitikia ndiyo! Baada ya Waumini kukubali ndipo akamgeukia Umar na kumpa ushauri wa kuagana."[67]

[67] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.326-327.

Bila ya shaka waandishi hao wamekiri kwamba Mtume (s.a.w.w.) hakusema kwa maneno juu ya Abu Bakar kuwa Khalifa baada ya Mtume (s.a.w.w.), ila wanadai kwamba alisema kwa vitendo, na zaidi kitendo kinachotolewa ushahidi ni suala la kuamrishwa yeye kuwaswalisha watu. Lakini kama tulivyotangulia kusema, ni kwamba ilikuwa ni tabia ya Mtume (s.a.w.w.) pindi anaposafiri kutoka katika mji wa Madina huwacha mtu atakayeshika baadhi ya majukumu yake, likiwemo jukumu la kuwaswalisha watu, na hoja hii kama ilikuwa ni hoja yenye mashiko ya kumuhalalisha kuwa Khalifa, basi ingesikika huko Saqifa, bali ni hoja ya kudhania tu, basi ikiwa ni hivyo, ni kwamba Mtume (s.a.w.w.) alisema kwa kutumia ulimi wake mtukufu kwamba, Makhalifa wa umma huu ni watu wa ukoo wake, kama tulivyoashiria huko nyuma, na si hivyo tu, bali pia aliashiria kwa vitendo vyake, yeye Mtume (s.a.w.w.) ndiye aliyemshika mkono Ali ibn Abi Talib katika bonde la Ghadir Khum mbele ya maelfu ya Maswahaba huku akisema: “Ambaye mimi ni kiongozi wake, basi pia Ali ni kiongozi wake.”[68] Baada ya hapo Maswahaba walimpa mkono wa pongezi, miongoni mwao akiwa ni Umar ibn Khattab, alimpa mkono wake huku akimwambia: “Hongera sana ewe mtoto wa Abu Talib, umekuwa kiongozi wangu na kiongozi wa kila Muumini mwanamme na mwanamke.”[69]Na pia Mtume (s.a.w.w.) alisema kumuambia Imamu Ali (a.s): “Wewe ni Kiongozi wa kila Muumini baada yangu.”[70]

Ndugu msomaji mpendwa haya ndiyo maandiko sahihi yaliyomo katika vitabu sahihi. Kwa hivyo suala la Ukhalifa baada ya Mtume halikujengeka katika dhana bali ni katika maandiko sahihi.

---

[68] *Musnadu Ahmad*: Jz. 1, Uk. 84. An-Nasai, *Fadhaailus-Swahaba*: Uk. 14. Bukhariy, *Tarikhul Kabir*: Jz. 1, Uk. 375.

[69] Raziy, *Tafsiru Raziy*: Jz. 12, Uk. 50. al-Qanduziy, *Yanaabihul Mawadda*: Jz. 2, Uk. 249.

[70] *Mustadrak Abi Daud Tayalasiy:*Uk, 360, Hadithi Na. 2752.

# UTEUZI WA UMAR

Wameeleza bayana kwamba, wakati Abu Bakar alipokuwa anakaribia kufariki dunia aliwaita wajumbe wa shura na kuwaeleza kwamba yeye anampendekeza Umar, na wajumbe hao wakaridhia hilo. Kwanza, kama tulivyotangulia kusema ni kwamba, hakukuwa na watu maalumu waliokuwa wakitambulika kama ni wajumbe wa shura, na lau kama ilifanyika hivyo, basi itakuwa Umar amekabidhiwa ofisi kwa mujibu wa mashauriano ya Waislamu, lakini ni wazi kwamba Umar aliukweya ukhalifa kutokana na wasia aliyousia Abu Bakar na kuandikwa na Uthman na sio Imamu Ali (a.s.) kama walivyoeleza.

At-Tabariy amefafanua namna Umar alivyopata Ukhalifa, anasema:

> "Abu Bakar aliposhikwa na maradhi alimwita Uthman ibn Affan na akamwambia: "Andika kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu, haya ni yale aliyoamua Abu Bakar ibn Quhafa kwa Waislamu, ama bada ya hayo…," Mara Abu Bakar akazimia. Uthman ibn Affan akaandika: "Ama baada ya hayo, mimi nimemfanya Umar ibn Khattab kuwa Khalifa wenu na sikuwatawalisheni mtu mwema…" Kisha Abu Bakar akazinduka, Uthman akamsomea alichoandika, Abu Bakar akasema: "Nakuona uliogopa watu kukhitalifiana kama ningekufa katika kuzimia kwangu." Akasema: "Ndiyo." Akasema: "Mwenyezi Mungu akulipe kheri kwa ajili ya Uislamu na watu wake." AbuBakar akaafiki haya.[71]

Utaratibu huu wameuelezea kuwani miongoni mwa njia nyingine ya kumpata Khalifa katika Uislamu! Lakini huonekana ni ki-

[71] At-Tabariy, Tarikhu Tabariy: Jz. 2, Uk. 618

oja pale baadhi ya Waislamu wanaposema kwa mujibu wa ushahidi wa maandiko matakatifu kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliacha wasii wa kushika uongozi baada yake. Basi ikiwa Abu Bakar alifanya hivyo kwa kuchelea kutokea mgawanyiko kati ya Waislamu kama ilivyotokea baada kifo cha Mtume na kugawanyika makundi matatu, basi tuelewe kwamba Mtume (s.a.w.w.) ndiye aliyesema kwamba umma huu utagawika makundi sabini na tatu, na moja tu ndilo litakalookoka. Katika mazingira kama haya inawezekana mtu kama yeye ambaye Mwenyezi Mungu amemueleza kwamba ni mwenye pupa katika kuwaongoa watu, iweje asizibe mianya itakayopelekea maangamizi! Ukisema kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliusia, utaambiwa hiyo ni fikra iliyoasisiwa na Myahudi, ama usia wa Abu Bakar wakumuusia Ukhalifa sahiba wake, huo ndio msingi sahihi wa kumpata kiongozi![72]

[72] Sheikh mmoja wa Kishi'a akiwa katika majadiliano na wenziwe wa Ahlul-Sunna alisema: "Inavyoekelea Abu Bakr alikuwa na akili sana kushinda Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)." Wao wakamshitukia na wakamwambia bwana wewe una maana gani? Yeye akajibu akasema: "Huoni yeye aliacha usia wa nani ashike mamlaka baada yake, lakini Mtume hakulifanya hilo." Wakagundua anakoelekea na haraka wakabadilisha mwelekeo wa mazungumzo.

# KUTEULIWA KWA UTHMAN

Ama Khalifa Uthman naye aliutwaa Ukhalifa kwa namna yake, wanasema:

"Uislamu sio dini iliyofungwa katika mabano, inasifa ya kwenda na wakati katika maana kuwa maamuzi yake ilimradi yamo katika mfumo wa Uislamu yanakubalika. Hali ilivyokuwa wakati alipofariki Mtume imetofautiana na ile ya wakati alipotawafu Abubakar. Wakati wa kifo cha Abubakar, Umar alijitokeza kuwa ndiye Khalifa bila ya upinzani lakini wakati wa kifo cha Umar hali ilikuwa tofauti. Walikuwepo watu wengi wenye sifa zinazolingana hivyo alichokifanya Umar ni kuteuwa jopo la watu la wagombea sita wa ukhalifa ambao walikuwa Uthman, Ali, Saada bin Waqqas, Talha, Zubeir na Abdur-Rahaman bin Auf. Agizo lingine alilotoa ni kuwa katika muda wa siku tatu baada ya kifo chake wawe wameshaamua wao wenyewe nani miongoni mwao awe Khalifa.

Jopo hili lilikaa kwa muda mrefu bila ya kufikia uamuzi ndipo Abdur-Rahaman bin Auf aliposhauri kuwa kati yao mmoja ajitoe ili aweze kutoa uamuzi. Alipokosa jibu alijitoa mwenyewe na kuanza kazi ya kutafuta maoni ili kukamilisha uteuzi. Talha hakuwepo kwa hivyo wagombea walibaki wanne. Imetokea kuwa Ali alimpendekeza Uthman na Uthman alimpendekeza Ali. Zubeir na Saad walimpendekeza Uthman.  Baaada ya kushauriana na Maswahaba wengine na kwa kuzingatia muda wa siku tatu Abdur-Rahaman bin Auf alitoa uamuzi asubuhi ya siku ya nne na kumtangaza Uthman kuwa ndiyo Khalifa. Abdur-Rahaman bin Auf alianza kumpa mkono wa ahadi ya utii na kutambua Ukhalifa wake ndipo Waislamu waliokuwa msikitini wakafuatia na kwa namna hii Uthman akawa khalifa wa tatu. Talha aliporudi Madina, Uthman alimshauri moja kati ya

mawili, achukuwe nafasi ya Ukhalifa au ampe mkono wa ahadi ya utii. Talha alikubali kumpa mkono wa utii. (uk.327).

Utaratibu huu pia umo katika mkondo wa Uislamu na ni aina ya tatu ya utaratibu wa kupata viongozi katika Uislamu."[73]

Katika maelezo yao haya kuna vipengele vingi ambavyo vinahitaji kujadiliwa na kuelezwa ukweli wake, lakini kutokana na kutokurefusha maneno, ni kwamba kila mwenye kuyasoma hayo, ataona kwamba Uislamu haukuweka utaratibu wowote juu ya kumpata kiongozi, kama walivyoeleza bayana kwamba huku kuteuliwa Uthman ni aina ya tatu ya kumpata kiongozi katika Uislamu. Licha ya hayo tunamuona Khalifa Umar alivyoona umuhimu wa kuwaachia Waislamu kiongozi atakayewaongoza baada yake, hasa baada ya kujiona kwamba hatoishi tena kwa muda mrefu kutokana na kupigwa panga, lakini Mtume (s.a.w.w.) aliyeishi katika hali ya ugonjwa kwa siku kadhaa kabla ya kufikwa na mauti hakufanya, tunaambiwa eti hakuacha kiongozi, hakufanya kama walivyofanya Abu Bakar na Umar! Bila ya shaka Mtume (s.a.w.w.) ni mwenye pupa zaidi juu ya maslahi ya Waislamu kuliko mtu mwengine, aliwataka Maswahaba wake wampelekee kalamu na wino ili awaandikie yale ambayo hawatopotea baada yake, lakini wapi! Walidai kwamba amezidiwa na ugonjwa, na hawana haja na maandishi yake kwa kudai kwamba Kitabu cha Mwenyezi Mungu kinawatosha![74]

Kwa kutaka kujua ukweli juu ya namna shura hiyo ya watu sita aliyoiteuwa Khalifa wa pili baada ya kupigwa panga, ni vyema tusome maneno haya ya wanahistoria: "Umar alipochomwa jambia, akaambiwa ungeteua Khalifa, akasema: "Kama Abu Ubeida al-Jarrah angekuwa hai ningemteua kuwa khalifa na kama Salim mtumwa wa Abi Hudhayfa angekuwa hai ningemteua kuwa khalifa." Kisha

[73] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.327-328.
[74] Sahihu Bukhariy, Babu Mardhwan Nabiyyi (s.a.w.w.) Wawafaatihi: Jz. 5, Uk. 138

akawaambia:“Hakika watu wanasema kwamba kiapo cha utii cha kumpa Abu Bakar kilikuwa ghafla, Mwenyezi Mungu ameepusha shari yake, na kiapo cha utii cha kumpa Umar hakikuwa kwa mujibu wa shura, na ukhalifa baada yangu ni kwa shura.”[75]

Kisha alisema: “Nimefanya jambo lenu liwe shura baina ya watu sita miongoni mwa Muhajirina wa mwanzo, ambapo aliwataja kwa kusema: ‘Niitieni Ali ibn Abi Talib, Uthman, Talha, Zubeir, Abdu Rahman ibn Awfi na Sa’d ibn Abi Waqqas, kama wanne watakubaliana, basi wawili wafuate rai ya wanne, na kama watakubaliana watatu, basi fuateni rai ya Abdu Rahman ibn Awf, sikilizeni na tiini…”[76]

Bila ya shaka, hii ni aina ya tatu ya namna Makhalifa walivyopatikana, aina ya kwanza ilikuwa ni jambo la ghafla, ambapo kwao Abu Bakar aliutwaa ukhalifa, aina ya pili ni ile ambayo Khalifa Umar anakiri kwa ulimi wake kwamba aliusiwa na kuteuliwa na Abu Bakar, na aina ya tatu ni aina hii ya shura ambayo Umar ameiwekea masharti, kwa lengo la kuhakikisha Imamu Ali (a.s.) hatofanikiwa kuwa Khalifa licha ya kukiri uwezo wake wa kipekee katika jambo hilo. Na shura yenyewe iliwajumuisha watu sita tu ambao ni Muhajirini watupu.

Kama ambavyo Khalifa Umar alivyotarajia ndivyo ilivyotokea, kwani watu hao sita waligawanyika makundi mawili, wale waliopendekezwa ni Imamu Ali (a.s.) na Uthman ibn Affan, Abdu Rahman alitoa sharti kwa Imamu Ali (a.s.) iwapo atalikubali atampa kura yake, sharti lenyewe lilikuwa ni kufuata mwenendo wa masheikh wawili (Abu Bakar na Umar), Imamu alilikataa sharti hilo kwa kusema: “Nitafuata Kitabu cha Mwenyezi Mungu, Mwenendo wa Mtume wake (s.a.w.w.) pamoja na ijtihadi yangu.”[77]

---

[75] Tabariy, *Tarikh Tabariy*: Jz. 3, Uk. 292
[76] Kitabu kilichotangulia.
[77] Khalid Muhammad Khalid, *Khulafau Rasul:*Uk. 272.

Bukhari amelieleza tukio hili katika *Sahih*yake kama ifuatavyo: Akasema (Abdu Rahman ibn Awf): "Niitieni Ali ibn Abi Talib, akaitwa, akamnong'oneza mpaka usiku ukaingia, kisha Ali ibn Abi Talib akatoka kwake akiwa na matarajio, na Abdurahman akawa anaogopa kitu (fulani) kwa Ali ibn Abi Talib. Kisha akasema: Niitieni Uthman, akaitwa, akamnong'oneza mpaka mwadhini wa asubuhi akawatenganisha, alipowaswalisha watu Swala ya Asubuhi na kundi hilo likakusanyika, Abdu Rahman akatoa shahada kisha akasema: "Ama baada ya hayo!Ewe Ali ibn Abi Talib, nimetazama jambo la watu na sikuona kwamba wanamtaka mwengine isipokuwa Uthman ibn Affan, kwa hivyo usiipe nafsi yako mwanya." Na akasema kumwambia Uthman: "Nakupa kiapo cha utii kwa kufuata kitabu cha mwenyezi Mungu, Sunna za Mtume na mwenendo wa makhalifa wawili baada yake."Abdu Rahman akampa kiapo cha utii na watu wakampa kiapo cha utii."[78]

Hii ndiyo kura ya veto aliyopewa Abdu Rahman na hii ndio namna alivyoitumia. Kura ambayo imerithiwa na mataifa makubwa yaliongoza kwa kuuwa watu wengi katika vita vya dunia, kura ambayo inatumiwa katika Umoja wa Mataifa kwa lengo la kuwakandamiza wanyonge, kwani kura hii ndiyo inayowabakisha walowezi wa Kiyahudi katika ardhi ya Wapalestina.

Kama suala la uongozi ni kwa Waislamu wote kushauriana, ni kwa nini Khalifa Umar hakumteua hata Muanswari mmoja katika jopo la watu sita alililoliteuwa? Au katika zama hizo kulikuwa hakuna tena Maanswari, na kwanini Abdu Rahman apewe kura ya veto wakati kwa madai yenu ni kwamba: **"lakini wakati wa kifo cha Umar hali ilikuwa tofauti. Walikuwepo watu wengi wenye sifa zinazolingana?"** Na je hao wengi waliokuwa na sifa zinazolingana ni hao sita tu?

[78] *Sahih Bukhar*, Jz. 9, Uk. 239. Kitabul Ahkam, babu kayfa Yubayaul Imam linnas.

# UTEUZI WA IMAMU ALI (A.S.)

Baada ya kumalizika kwa kipindi cha utawala wa khalifa Uthman kwa kuuwawa, khalifa aliyefuatia alikuwa ni Imam Ali s.a., lakini kwa masikitiko na majonzi makubwa waandishi hao hawakubaliani na namna Imamu Ali (a.s.) alivyoupata Ukhalifa, wanasema:

"Mkondo wa historia ya Kiislamu juu ya utaratibu wa kuingia kwenye mamlaka umechukua sura mpya, pale alipouliwa Khalifa wa tatu na kundi hili la wapinzani likamtaka Ali awe ndiye Khalifa wa nne. Kwa hali ilivyokuwa naye akakubali kuchukua nafasi hiyo. Jambo hili lilipelekwa msikitini na wapo waliokubali Ukhalifa wa Ali bila masharti, wapo waliokubali kwa sharti kuwa wahalifu waadhibiwe na wapo waliokataa kumpa mkono wa ahadi ya utii miongoni mwao, ni Muhammad bin Muslimah, Usama bin Zaid, Hasan bin Thabit, Ka'ab bin Malik, Abu Said Khudri, Numan bin Bashir, Zaid bin Thabit, Mughira bin Shubah na Abdullah bin Salama. Na wengine waliokataa ni ndugu na jamaa wa Uthman. Baadhi ya waliokataa Ukhalifa wa Ali walihamia Syria."[79]

Kwa mujibu wa ukweli wa kihistoria, Imamu Ali (a.s.) alipewa ahadi ya utii na Maswahaba wasafi, na sio wauwaji kama wanavyodai, na tutaonesha ushahidi wa wazi juu ya hoja yetu hii.

Wanaendelea kusema:

"Utaratibu huu, ingawa kuna baadhi ya wanachuoni wanaoukubali lakini hauhitaji mjadala wowote, ni wazi kuwa hauna nafasi katika Uislamu; kwa hakika watu wa Madina walikuwa na khofu na kundi hili la wauwaji hivyo kukubali kwao ule Ukhalifa wa Ali

---

[79] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.328.

kwa mfumo ule yawezekana ni matokeo ya woga tu na sio hiyari yao. Majibu ya Talha na Zubeir walipoulizwa na mjumbe wa Gavana wa Basra katika msafara wa Bibi Aisha kwa nini wanavunja ahadi ya utii kwa Khalifa walisema: "Baiat ilifanywa mbele ya ncha ya upanga na ahadi ya kuwaadhibu wauwaji."

Inawezekana hata kule kukubali kwa Ali kuwa Khalifa kunatokana na woga kwa sababu walipomtaka mara ya kwanza awe Khalifa kabla ya hao wauwaji kumuua Khalifa Uthman alikataa. Si hivyo tu lakini alipoona wanamsonga kutaka kumshirikisha katika mzozo wao alihama Madina na kwenda Ahajar sehemu maili chache kutoka Madina. Ingawa pia tukio hili linaonekana kumuweka Ali mahali pabaya.[80]

Kwa kweli ni masikitiko makubwa kwa waandishi wa kitabu hicho kuandika haya waliyoyaandika, hasa kwa vile ni katika mafunzo yanayofundishwa wanafunzi wa Kiislamu! Si hivyo tu, bali wamediriki kusema kwamba Imamu Ali alichaguliwa kuwa Khalifa na wauwaji, ambao ndio waliokuwa wakiwafundisha watu kwamba Ali ni wasii wa Mtume. (s.a.w.w.)[81]

Licha ya kwamba kwa kipindi cha muda wa miaka isiopunga ishirini na tano Imamu Ali(a.s.) alikoseshwa haki yake ya Ukhalifa, lakini pale Waislamu walipozinduka walijitokeza kwa wingi na kwa kishindo kumpa mikono yao ya utiifu kwake tena katika mazingira ya dhahiri shahiri ila wachache waliokuwa na chuki dhidi yake, hebu tusome maneno haya yaliyoandikwa na mwanachuoni mkubwa na aliyekuwa Kadhi Mkuu wa Kenya:

> "**Kutawalishwa Ukhalifa:** Baada ya kupita msiba wa kuuliwa S. Uthman R.A, na Sydna Aly k.w. kurudi nyumbani kwake,

[80] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.328.
[81] Elimu ya Dini ta Kiislamu, Shule za Sekondari, kitabu cha 4, uk.367

> Masahaba walimjia na kumwambia: "Uthman ameuliwa, na watu hawana budi wapate muongozi. Na sisi hatumuoni mtu bora na mwenye haki zaidi kushika jambo hili kuliko wewe." Sydna Aly k.w. akawambia: "Musinitawalishe mimi, tazameni mtu mwengine mumfanye Khalifa, na mimi nitakuwa waziri na mshauri wake." Masahaba wasiridhike, wakamwambia: "Wallahi hatukubali illa tukutawalishe wewe." Sydna Aly k.w. alipowaona hawana budi kumtawalisha yeye, akawambia: "Iwapo hamuna budi illa mimi, basi sikubali kutawalishwa nyumbani kisirisiri, twendeni Msikitini mbele za Waislamu wote." Wakenda msikitini kama walivyotaka, na huko wakakusanyika Muhajirina na Ansar na wengineo, wakamtawalisha, isipokuwa jamaa zake S. Uthman (Bani-Umayyah) na kidogo katika Muhajirina na wawili watatu katika Ansar, wasikubali. Katika Bani-Umayyah wengi wakatoka na kukimbilia Sham kwa jamaa yao; Muawiyah, na wengine wakatukua (wakachukua) kanzu aliyokuwa amevaa S. Uthman wakati alipouliwa na iliyokuwa imetapakaa madamu, pamoja na vidole vya mkewe Mw. Nailah vilivyokatwa wakati alipokuwa akimkinga na upanga."[82]

Kwa hivyo, enyi wanafunzi wenzangu mnaokisoma kitabu chao hicho, eleweni kwamba Khalifa wenu wa kwanza (Imamu Ali (a.s.)) au wanne, hakuwa ni mwenye kung'ang'ania madaraka hasa katika wakati ambao fitina kubwa ilikuwa imeenea kati ya Maswahaba, na baada ya sheria mbalimbali kupewa mgongo na mafasiki kupewa nafasi ya ugavana katika dola ya Kiislamu, na Ukhalifa kufanywa kuwa ni sehemu ya kujikusanyia mali. Maanswari na Muhajirina walimlazimisha Imamu Ali (a.s.) awe Khalifa wa Waislamu na hatimaye akakubali. Sasa iweje kwa huyu aliyeteuliwa na maelfu ya Waislamu iwe uteuzi wake si sahihi, ama wale walioukwaa Ukhalifa kwa kuusiwa iwe uteuzi wao ndio sahihi! Sijui ni mizani gani wanayopimia mambo! Na wale waliodai kwamba walimpa Imamu Ali (a.s.) mikono yao ya utiifu baada ya kulazimishwa, hayo ni ma-

[82] Maisha ya al- Imam Aly: uk. 33).

dai yasio sahihi, na zaidi tumeyaeleza katika maudhui ya ‘Vita vya Ngamia,’ vita ambavyo viliongozwa na Bibi Aisha na kusababisha mauwaji makubwa ya Waislamu wasiopungua elfu kumi.

Kwa hakika Imamu Ali (a.s.) alikuwa hahitaji kuwa Khalifa wa Waislamu kutokana na uteuzi wao, kwani yeye alikwishaipata nafasi hiyo kwa mujibu wa Aya mbalimbali za Qur’ani na maneno ya Mtume (s.a.w.w.) kama tulivyokwisha ona huko nyuma. Kilichofanyika huko nyuma ni watu wenyewe kutokubali kumpa nafasi hiyo, kama vile kaumu mbalimbali kuwazuilia Mitume wao wasishike nafasi ya kuongoza dola, baada ya wao kuwa ndio watu pekee waliokuwa wana sifa zote za uongozi.

# UONGOZI BAADA YA KHALIFA ALI (A.S.)

Utaratibu wa kuingia katika uongozi wa dola ulizidi kuharibika alipouwawa Ali, mwanawe mkubwa Hassan aliteuliwa kuwa Khalifa wa tano. Lakini Muawiyah alipopata habari hizi aliivamia Iraq. Hassan nae kwa upande wake alimteuwa Qays kuongoza majeshi ya kupigana na Muawiyah. Kulitokea uvumi kuwa Qays ameuwawa na hali hii ilipelekea majeshi ya Khalifa kumgeukia mwenyewe. Hassan alielewa hali ilivyokuwa mbaya hivyo alisalimu amri kwa Muawiyah, akaacha Ukhalifa kwa makubaliano kuwa atapofariki amuachie nduguye Husein ukhalifa. Baada ya makubaliano haya na Muawiya, Hassan alirudi Madina, lakini aliuliwa kwa sumu aliyolishwa na mmoja wa wake zake kutokana na ushawishi wa Yazid. Huu ndio ulikuwa mwisho wa Hassan mjukuu wa Mtume.

Taratibu zote hizi ni za kupora madaraka kama alivyofanya Muawiyah ingawa alishinda kivita, kuwekeana makubaliano na watoto wa Ali, Hassan kuwa atawaachia madaraka Hussein baada ya kufa kwake, na utaratibu wa kurithishwa, taratibu zote hizi, hazikubaliki katika Uislamu, ingawa mfumo huu wa mwisho ndiyo uliotumika katika utawala wa Banu Umaya, Banu Abbas na Fatimiya."[83]

Ni vyema Waislamu waelewe kwamba, Khalifa wa pili aliushika Ukhalifa kwa njia ya kuusiwa na kurithishwa na Khalifa wa Kwanza, na mfumo huu wameueleza kwamba ni mfumo wa pili wa kumpata kiongozi, sasa ni vipi ikiwa wengine wakifuata sunna hiyo ya Khalifa wa Kwanza wawe wamekosea na kuambiwa utaratibu wao huo haufai!

[83] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.328.

Ama kuhusiana na mkataba kati ya Imamu Hasan na Muawiya ambao miongoni mwa vipengele vyake ni madaraka ya uongozi wa Waislamu ushikwe na Imamu Husein baada ya kufariki kaka yake, ilikuwa ni sharti lililowekwa na Imamu Hasan kwa lengo la kuirejesha haki hiyo kwa wenyewe wanaostahiki (Ahlul-Bayt(a.s.)), kwani kama tulivyoashiria, maandiko matakatifu ndiyo yaliyotoa haki hiyo na si vyenginevyo.

Ama hizo koo nyingine zilizopora madaraka na kurithishana wenyewe kwa wenyewe na hali hiyo kuendelea katika nchi mbalimbali za Kiarabu, ni kweli hawana haki ya kufanya hivyo, hasa ikizingatiwa kwamba ni watu wasiofaa kushika nafasi hizo, kwani historia inatuonesha namna Bani Umayya walivyofanya unyama dhidi ya Waislamu wasio na makosa, na baya zaidi walidiriki kumuua mjukuu wa Mtume (s.a.w.w.) na kumchinja, licha ya Qur'ani kuwataka Waislamu kumlipa Mtume wao kutokana na kazi kubwa aliyoifanya ya kuwaongoa watu, malipo hayo si mengine, ila ni kuwapenda na kuwakirimu Ahlul-Bayt wake, Mwenyezi Mungu anasema:

قُلْ لا أَسْئَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْراً إِلاَّ الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبى...

"Sema: Siwaombeni malipo, isipokuwa kuwapenda jamaa zangu wa karibu."(Qur'ani,42:23).

Isitoshe, Waislamu wana wajibu wa kuwatakia kheri na baraka watu hao katika Swala za Wajibu na za Sunna, ni pale tunaposema:

اللهم صلّ على محمّد وآل محمّد.

> "Ewe Mola Wangu! Mtakie rehema Muhammad na Aali zake Muhammad…"[84]

Na Mtume (s.a.w.w.) ametukataza kumswalia yeye bila ya Ahlul-Bayt wake, anasema:

لا تصلّوا عليّ الصلاة البتراء , وما الصلاة البتراء ؟ قال: تقولون: اللهم صلّ على محمّد وتمسكتون," بل قولوا : "اللهم صلّ على محمّد وآل محمّد.

> "Msiniswalie Swala iliyokatika (kibutu)." Maswahaba wakauliza:"Ni ipi hiyo Swala iliyokatika ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?" Mtume aliwajibu: Ni kusema:"Allahumma swali alaa Muhammad kisha mkanyamaza, lakini semeni: Allahumma swali alaa Muhammadwa alaa Aali Muhammad."[85]

Basi kama kuna madai dhidi ya Mashia wa Imamu Ali (a.s.) ya kwamba wanaona haki ya uongozi ni ya Ahlul-Bayt, na wameasisi fikra ya uwasii, basi ieleweke kwamba, hata katika ibada ya Swala anayoiswali kila Mwislamu ambayo ndiyo Mwislamu atakayoulizwa mwanzo Siku ya Kiyama, ndani yake imewajibishwa kuwatakia rehema jamaa wa Mtume (s.a.w.w.) kama vile ambavyo Mwenyezi Mungu alifanya hivyo kwa jamaa wa Nabii Ibrahim (a.s.). Kwa hivyo kila mmoja wetu atambue kwamba katika Swala zake anawatakia rehema Ali ibn Abi Talib, Bibi Fati-

---

[84] Mwishoni mwa swala hiyo inasema "Mbariki Muhammad na Aali zake Muhammad kama ulivyombariki Ibrahim na Aali Ibrahim juu ya walimwengu wote." Tujiulize ni Baraka gani juu ya walimwengu wote alizopewa Ibrahim juu ya walimwengu kama sio uongozi?

[85] *Yanabii'ul Mawaddah* Jz. 1, uk. 37

ma, Hasan na Husein, na mwenye kuacha kufanya hivyo atambue kwamba Swala yake haitosihi, kama anavyosema Imamu Shafi:

يآل بيت رسول الله حبّكم          فرض من الله في القرآن أنزله

كفاكم من فضل القدر أنّكم          من لم يصلّ عليكم لا صلاة له

> "Enyi watu wa nyumba ya Mtume, kupendwa kwenu ni faradhi (lazima) kutoka kwa Mwenyezi Mungu katika Qur'ani ameteremsha (42: 23). Inatosha kwenu kuwa ni heshima kubwa mliyonayo, yeyote asiyewatakia rehema hana Swala."

Watu hawa ndio ambao tawala hizo za Kibanu Umayya na Kibanu Abbasi ziliwadhulumu kwa aina mbalimbali za dhulma, licha ya kwamba Mwenyezi Mungu amewaainisha, akawatakasa na kuwatoharisha na kila aina ya uchafu, kama alivyosema:

إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنكُمُ الرِّجْسَ أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرا

> "Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume (s.a.w.w.), na kukusafisheni barabara." (Qur'ani, 33:33).

Bibi Aisha anathibitisha ya kwamba Aya hii inawahusu watuwa nyumba yaMtume (s.a.w.w.) na siwengineo, anasema:

” خرج النبي صلى الله عليه وسلم غداة و عليه مرط مرحل من شعر أسود فجاء الحسن بن علي فأدخله ثم جاء الحسين فدخل معه ثم جائت فاطمة فأدخلها ثم جاء علي فأدخله ثم قال : ”إنما يريد الله ليذهب عنكم الرجس أهل البيت و يطهركم تطهيرا“

> “Alitoka Mtume (s.a.w.w.) asubuhi naye akiwa na shuka yenye nakshi za matandiko (ya ngamia) imefanywa (shuka hilo) kutokana na manyoya meusi, basi akaja al-Hasan bin Ali akamuingiza, kisha akaja al-Husain akaingia pamoja naye, kisha akaja Fatima akamuingiza kisha akaja Ali akamuingiza kisha akasema: Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni baraabara.”[86]

Lakini kama vile ambavyo watu walivyojenga husda, chuki na choyo dhidi ya jamaa wa Nabii Ibrahim (a.s.) ambao nao pia walikuwa Mitume na waliopewa mamlaka ya kuwaongoza watu, ni hivyo hivyo baadhi ya watu walivyofanya dhidi ya watu wa nyumba ya Mtume (s.a.w.w.) kama Mwenyezi Mungu anavyosema:

أَمْ يَحْسُدُونَ النَّاسَ عَلَى مَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ فَقَدْ آتَيْنَا آلَ إِبْرَاهِيمَ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَآتَيْنَاهُمْ مُلْكًا عَظِيمًا

[86] *Sahih Muslim* Jz. 8, katika *Sharhu Nnawawiy* Uk. 46. Hadithi na. 6211. Ibn Jarir At-Tabari *Jamiul Bayaan* Jz. 22, uk. 5.

> **“Au wanawahusudu watu kwa alichowapa Mwenyezi Mungu katika fadhila yake? Basi tuliwapa watoto wa Ibrahim Kitabu na hekima na tukawapa ufalme mkubwa.” (Qur’ani, [87]4:54)**.

Pia wimbi hilo la husda na mauwaji liliendelezwa na watawala wa Banu Abbas, kiasi cha kupelekea Imamu wa kumi na mbili (Imamu Mahdi (a.s.)) kuishi mafichoni hadi hii leo.

[87] Mambo haya yako wazi kabisa na inaonesha wazi kwamba upinzani ulianza wakati wa uhai wa Bwana Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa akilitambulisha jambo hili la uongozi, kwani tamko Mwenyezi Mungu ni – ‘Au wanawahusudu’ – hao Ahlul-Bayt!

# MTINDO USIO WA KIISLAMU!

Kwa mara nyingi sana wamesisitiza kwamba, nadharia ya kuwepo wasii na mrithi wa Ukhalifa ni jambo lisilokubalika katika Uislamu, kusudio lao likiwa ni kupinga ile fikra inayoaminiwa na Mashia kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliacha usia juu ya mtu atakayeshika nafasi yake, wamekwenda mbali zaidi, kwa kuinasibisha fikra hii na dini zisizo sahihi, kama wasemavyo:

"Mtindo huu haumo katika mfumo wa Uislamu ingawa wafuasi wake wanatumia jina la Uislamu. Kwa nini mtindo huu haumo katika Uislamu tumeshazitaja sababu zake mwanzoni mwa sura hii,ila hapa tunataka kuongeza kuwa Imani hii ambayo ilipandikizwa baadaye katika historia ya Uislamu ina mizizi ya dini ya Uzoroastrian na Ukristu, dini ambazo zote zinamshirikisha Mwenyezi Mungu."[88]

Sijui wanasemaje kuhusiana na wasia wa Khalifa wa Kwanza juu ya Khalifa wa Pili, kwani wasia wake ndio uliomfikisha katika Ukhalifa. Na hata huyo Khalifa wa Pili alilazimika kuitisha shura ya watu sita ili washauriane juu ya mtu atakayeshika nafasi yake pale atakapofariki, kwa sababu tu Abu Ubayda alikuwa ameshafariki kabla yake, na ametamka wazi lau kama Abu Ubayda angekuwa hai, basi ningemtawalisha." Akimaanisha kwamba kusingekuwa na hata hiyo shura ya watu sita, izingatiwe kwamba Abu Ubayda alikuwa mmoja ya wale Wahajirina Watatu waliohudhuria katika ukumbi wa Saqifa baada ya kupata habari kwamba Maanswari walikusanyika kwa lengo la kumchagua Khalifa.

Na zaidi ya hayo khalifa Umar alikwenda mbali zaidi, kwa kutamka kwamba, lau kama Salim, ambaye alikuwa mtumwa wa

[88] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.330

Hudhayfa angekuwa hai, basi angemtawalisha ukhalifa bila ya kumshauri yeyote.[89]

Tumeona ni namna gani Muhajiri wa Kwanza alivyompasia wa Pili bila ya kuwashauri wengine, na huyu wapili anatamka wazi kwamba, lau kama yule watatu angekuwa hai, basi naye angempasia!Kuhusiana na hizo hali zilizojitokeza ndizo zinazoambiwa kwamba ndiyo njia sahihi za kuingia katika uongozi wa kitaifa, na ile aliyotumia Mtume (s.a.w.w.) ya kumteua Imamu Ali (a.s.) ni njia ambayo haina msingi katika Uislamu! Wanasema:

> "Hii ndiyo historia namna Mwislamu anavyoingia katika uongozi wa kitaifa. Kuna njia zilizotumika ambazo zimo katika Uislamu na zipo ambazo si katika Uislamu. Kwa Waislamu hivi leo, mfumo wa usia kama wanavyofanya wafuasi wanaojiita mashia si katika utaratibu unaokubalika katika Uislamu.[90] Mtume hakulifanya, na hata Ali alipokuwa katika kitanda cha mauti baada ya kujeruhiwa aliulizwa na mtu mmoja kuwa Waislamu wampe mkono wa ahadi ya utii mwanao mkubwa Hassan awe Khalifa Ali alijibu,'' Nawaachia Waislamu waamue."[91]

Tunapoisoma Hadithi aliyoipokea Muslim katika Sahihi yake, inayobainisha kwa ufasaha, kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) ametuachia vizito viwili, cha kwanza kikiwa ni Qur'ani na cha Pili ni Ahlul-Bayt wa Mtume (s.a.w.w.), ni wazi kwamba Imamu Ali hawezi kushiriki katika kumpinga Mtume (s.a.w.w.) na kuihamisha haki hiyo kutoka kwa wenyewe, Imamu Ali (a.s.) ndiye aliyesimama na kuwauliza Maswahaba: "Je hamkumsikia Mtume (s.a.w.w.) akiwaambia watu katika kitongoji cha Rahba: Ambaye

[89] Tareikh ibn Khaldun:J.1,Uk.194.

[90] Bali usia na kurithiana kwa Bani Umayyah na Bani Abbas ni sahihi? Kwa ushahidi gani wa aya ama hadithi? Mbona mnawakubali makhalifa wao ambao wamefanya kurithiana kiukoo?

[91] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.330.

Mimi ni Kiongozi wake, basi na Ali ni Kiongozi wake."[92] Yeye ndiye aliyeitafsiri kivitendo Aya hii isemayo:

إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَى آدَمَ وَنُوحًا وَآلَ إِبْرَاهِيمَ وَآلَ عِمْرَانَ عَلَى الْعَالَمِينَ ذُرِّيَّةً بَعْضُهَا مِنْ بَعْضٍ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

> "Hakika Mwenyezi Mungu alimchagua Adam na Nuh na watoto wa Ibrahim na watoto wa Imran juu ya walimwengu wote. Ni kizazi cha wao kwa wao na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kujua." (Qur'ani 3:33 – 34).

Pale alipomtaka mtoto wake Hasan asimame na kuwahutubia watu, Hasan akasema: "Mimi nakuonea haya kuzungumza na ilhali mimi nakuona. Basi Imamu Ali (a.s.) akajificha kwenye sehemu ambayo anamsikia sauti yake, hapo Hasan akasimama, akaanza kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumsifu na akazungumza, kisha akateremka kwenye mimbari, basi Ali (a.s.) akasema: "Kizazi wao kwa wao; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia na Mwenye kujua."[93]

Lau kama ni kweli Imamu Ali (a.s.) alimjibu hivyo mtoto wake huyo maneno hayo, pengine ni kutokana na hali ilivyokuwa imezidi kuharibika, ikiwa yeye alifanyiwa hivyo alivyofanyiwa kwa sababu ya kuwa Khalifa wa Waislamu, basi watoto wake watafanyiwa makubwa zaidi, kwani yeye alipigwa vita na Bibi Aisha, Muawiya na Makhawariji, na mwisho wake akapigwa panga ambalo lilikuwa sababu ya kifo chake.

Bila ya shaka baadhi ya Waislamu walitambua kwamba haki ya Ukhalifa ni ya Ahlul-Bayt(a.s.), ndio maana mara tu baada ya kuu-

[92] Al-Haythamiy, *Majmauz Zawaid*: Jz. 9, Uk. 105.
[93] Assuyutiy, Addurul Manthur; J.2, Uk.18, Tafsiri ya Aya ya 33-34, Sura ya 3.

wawa Imamu Ali (a.s.) makundi kwa makundi ya Waislamu walimuendea Imamu Hasan na kumpa mkono wa utii wa kuwa Khalifa, lakini Muawiya akampiga vita vikali na kuwanunua makamanda wa Imamu Hasan na damu nyingi ya Waislamu ikamwagika, Hapo Imamu Hasan akaona ni vyema kuingia katika suluhu ili kuzuia damu za Waislamu zisiendelee kumwagika.

Na hapa napenda niwaeleze ndugu wanafunzi wenzangu kwamba, Waislamu wasiojiita mashia walifanya njama ya kuficha ukweli juu ya wasia aliousia Mtume (s.a.w.w.), ili kufanikisha malengo yao ya kisiasa na kuutoa umma wa Kiislamu katika barabara aliyoiweka Mtume (s.a.w.w.). Wakati Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa katika kitanda cha mauti aliusia mambo matatu: Kutolewa washirikina katika bara Arabu, kuwataka Waislamu waendeleze kuwakirimu wageni wanaoingia humo kama ambavyo yeye Mtume (s.a.w.w.) alivyokuwa akifanya, lakini msimulizi wa Hadithi hii alijizuia kutaja jambo la tatu.[94] (Ambalo Maulamaa wetu wanasema kwamba lilikuwa ni usia juu ya kushikamana na Ahlulbayti a.s.)

Hii ndio khiyana kubwa waliyofanyiwa Waislamu, kwa kufichwa kitu kimoja ambacho Mtume wetu alikiusia, iweje watu walioweza kuhifadhi Qur'ani yote wajisahaulishe sentensi moja fupi kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.), wameweza kututajia mambo yote saba yenye kuangamiza, ambayo Mtume (s.a.w.w.) ametutaka tujiepushe nayo.  Kwa kweli siasa ni mchezo mchafu, kwa vile madaraka ni matamu!

[94] Sahihi Bukhariy, Babu Mardhan Nabiyyi (s.a.w.w.) na kifo chake: J.5, Uk.138.

# UPINZANI KUTOKA MIONGONI MWA WAISLAMU

Katika maudhi waliyoyapa kichwa hicho hapo juu wanasema yafuatayo:

"Ukhalifa wa Uthman ulichukua miaka 12, katika miaka sita ya kwanza dola ya Kiislamu iliimarika na mipaka yake kupanuka kama ilivyokwishaelezwa. Katika miaka sita aliyomalizia Ukhalifa wake kulikuwa hakuna utulivu, kulizuka miongoni mwa Waislamu malalamiko ya uongo dhidi ya Khalifa na serikali yake. Kiongozi wa kundi hili la wapinzani ni Abdullah Ibn Sanda alijulikana sana kwa jina la Ibn Sanda au Ibn Saba. Ibn Sanda alikuwa Myahudi anayetoka Yemen, alisilimu kinafiq kama alivyosilimu Abdallah bin Ubeidah lakini ibn Saba tangu aliposilimu alikuwa na mpango wake wa kuudhuru Uislamu hatua kwa hatua, kundi la wanafiki hawa liliiloongozwa na Ibn Saba lilitumia shutuma dhidi ya Khalifa na serikali yake kuficha unafiq wao kwa sababu madai yao yalikuwa ni ya uongo na pale walipopewa maelezo ya kweli waliyafumbia macho na hawakuyakubali.

Tutaonesha unafiki wao huo katika mbeya mbili: kwanza tutaonesha udhaifu wa madai yao yaliozusha uasi na hatimaye kumuua Khalifa wa pili [tatu], vitendo vyao vilivyokuwa dhidi ya Uislamu hivyo kudhihirisha unafiq wao. Sababu zilizowapelekea kuzusha uasi na hatimaye kumuuwa Khalifa Uthman ni hizi zifuatazo:

Wasabai hao walidai kuwa Khalifa anapendelea ndugu zake katika kugawa kazi za ngazi za juu kama ugavana. Dai hili halikuwa na ukweli wowote. Ni kweli Muawiyah ni ndugu wa karibu wa Uthman, lakini amiri aliteuliwa Gavana wa Syria tangu wakati wa Umar. Kadhalika Sa'ada aliyeiteka Persia aliteuliwa wakati

wa Umar. Kutokana na malalamiko kidogo dhidi yake aliondolewa kwenye ukhalifa na Umar na nafasi yake ikashikwa na Mughira lakini Umar alidhamiria kumrudisha wadhifa wake Sa'ad, lakini kulizuka kutoelewana baina ya Gavana na Ibn Ma'ud mkusanyaji wa kodi wa Kufa. Sa'ad aliondolewa na nafasi yake ikajazwa na Walid bin Aqaba. Walid alikuwa ndugu wa karibu wa Uthman, lakini aliyeteuliwa mwanzoni mwa ukhalifa wake kabla ya tuhuma hizi, hata hivyo Walid alipopatikana na hatia ya kunywa pombe aliadhibiwa kwa mujibu wa sheria na kuvuliwa Ugavana, kama angemteua kwa udugu tu Khalifa angeweza kunyamazia jambo hili. Baada ya Walid, Sa'ad aliteuliwa kuwa Gavana wa Kufa lakini wapinzani wa Kufa chini yake walipata mafanikio makubwa hivyo akateuliwa Abu Musa Ashari mwaka 34 A.H. ambaye hakuwa na uhusiano wa damu kabisa na Uthman. Abu Musa alikuwa Gavana wa Basra na malalamiko ya upendeleo yalimfanya aondolewe na mahala pake akawekwa Gavana aliyeteuliwa na wapinzani.

Madai mengine ya wanafiki wa kundi la Saba ni matumizi mabaya ya pesa za serikali. Lawama nyingine ambayo ni kuhusu mjomba wa Uthman Hakam Ibn Al-Aas ambaye alikuwa akiwatendea vibaya jirani zake na kumchezea shere Mtume. Alihamishwa Madina. Baada ya miaka michache Uthman alimuombea kwa Mtume na baada ya kuombwa mara nyingi Mtume aliahidi kulitazama upya suala hilo. Mtume alipokufa jambo hili lilikuwa halijapatiwa ufumbuzi. Uthman aliwaomba Abubakar na Umar wamrejeshe kutoka uhamishoni katika ukhalifa wao, lakini hawakuruhusu. Katika ukhalifa wa Uthman alimrudisha mjomba wake baada ya miaka 17 ya kuishi uhamishoni. Hili nalo limemfanya Khalifa kulaumiwa.

Hadithi zikavumishwa kuwa khalifa amewanyanyasa baadhi ya maswahaba mfano unaotolewa ni wa Abu Dharr Ghiffar, Swahaba huyu alikuwa mchamungu kama maswahaba wengine ila yeye ali-

chukua muelekeo wa kisufi. Kwa Imani yake hii alilaumu waliokuwa wanaishi maisha ya kujikweza hasa baada ya watu kupata utajiri kutokana na ngawira. Halikadhalika alitaka Baitul Mal, pasiwe na salio. Fedha au mali igaiwe na itumike kadiri inavyokuja, alianza kueneza imani yake hii Syria. Gavana wa jimbo la Syria Amir Muawiyah alimuandikia Khalifa kumfahamisha juu ya shughuli za Abu Dharr Ghifari. Khalifa alimwita Abu Dharr Madina. Abdallah bin Saba alijaribu kumuombea alipokuwa Syria lakini Gavana Muawiya alisema imani anayofundisha ni mpya katika Uislamu na nia yake ni kuleta mtafaruku miongoni mwa Waislamu.

Abu Dharr (alipofika Madina alijadiliana na Khalifa. Khalifa alimuuliza Abu Dharr watu wakishatekeleza wajibu wao mimi nina mamlaka gani kuwataka watoe zaidi? Abu Dharr alipoona hakuweza kumbadili Khalifa alikwenda kuishi kijiji cha Rabdhah karibu na Madina na alifia hapo. Wanafiki waligeuza maneno na kusema Abu Dharr alitakiwa aishi kijijini hapo kwa amri ya serikali hivyo alinyanyaswa. Ni dhahiri Khalifa hata kama alifanya hivyo alikuwa sahihi kwa vile ni kweli imani ya Abu Dharr haikuwa ya Kiislamu. Inasemekana pia maswahaba aliowanyanyasa ni pamoja na Ammar bin Yasir na Abdullah bin Masud. Dai hili ni la uongo kama tulivyoonesha. Lakini linathibitika zaidi wakati Abu Ammar [Ammar bin Yasir] alipoteuliwa kuwa miongoni mwa wajumbe wa kwenda mikoani kuchunguza matatizo ya magavana.

Khalifa Uthman anatoka ukoo wa Bani Umayya wa Makureish. Kabla ya kuzaliwa Mtume kulikuwa na kutoelewana baina ya ukoo wa Banu Ummayah na ukoo wa Banu Hashim anaotoka Mtume ambao ni wa Kikureish. Wasabai waliwashawishi ukoo wa Hashim kuwa khalifa anapendelea ukoo wa Banu Umayya kwa kuwapa nafasi za juu na kuwaondoa madarakani ukoo wa Hashim.”[95]

[95] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk.356-359.

Kwa kweli inasikitisha kutoelezwa kwa usahihi matukio ya kihistoria yaliotokea katika zama za Khalifa Uthman, mengi yaliyoelezwa ni kujaribu kumili upande mmoja hata kama uhakika unapingana na mawazo yao, wamejaribu kutetewa wale waliosababisha umwagaji damu katika umma huu na kutiwa katika hatia za kubuni Maswahaba watukufu kama vile Abu Dharr (r.a.), na baya zaidi ni kubuniwa kwa mtu ambaye hakuwahi kuumbwa katika ulimwengu huu (Abdullah ibn Sabai), ambaye amefanywa kama ndio nyota katika mchezo huo wa kuigiza. Haya ndiyo ambayo tutayachambua hapa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu ili kubainisha ukweli kwa mujibu wa maandiko sahihi.

Si sahihi kwamba Waislamu walizua malalamiko ya uongo dhidi ya Khalifa Uthman, bali yalikuwa ni malalamiko ya msingi, na hasa ikizingatiwa kwamba Waislamu wengi walikuwa dhidi ya Khalifa kutokana na baadhi ya matendo yake, na kuamua kumuua na kuuacha mwili wake kwa muda wa siku tatu, na ni watu wasiozidi kumi ndio waliomzika akiwemo binti yake, Aisha binti Uthman. Wakati alipokuwa anapelekwa kuzikwa, baadhi ya watu walisimama njiani na kulirembea mawe jeneza lake, zaidi ya hayo walizuia hata asizikwe katika makaburi ya Waislamu, hatimaye akazikwa pamoja na Mayahudi![96]

Waandishi mbalimbali wamenakili juu ya hali ya ukabila iliyokuwapo katika zama hizo, hebu tumsikilize mwandishi wa Kitabu kiitwacho Masahaba Kumi Waliobashiriwa Pepo anavyosema: “Msingi wa fitna zote zilizomfika Amir Al-Muuminin bin Afan (r.a.) ilikuwa ni kutokana na Marwan bin Hakam, huyu alikuwa akimshauri vibaya Sayyidna Uthman, naye Uthman alikuwa hamfahamu kuwa Marwan amuwashia moto mkubwa sana wa fitina, sababu Uthman alikuwa amekwisha konga sana. Akifa alikuwa na umri wa miaka 86, ali-

[96] Tarikh Tabariy, J. 3, Uk. 437.

kuwa mzee sana, na huyu Marwan alikuwa ndiye mshauri mkubwa wa Uthman (r.a.)"

Mwandishi anaendelea kutaja sababu zilizopelekea watu kukereka na Khalifa Uthman, anasema: "La kwanza lililowaudhi sana watu ni kuwa Uthman alikuwa na ukabila sana, akipendelea jamaa zake Bani Umayyah. Kazi kubwa zote walikuwa wakipewa Bani Ummayah, tena Uthman alikuwa akifuata sana na kusikiliza sana fitina za huyo Marwan bin Al-Hakam mpaka watu wa mamlaka zote za Kiislamu wakati huo zikawa zimechoshwa na ukhalifa wa Uthman bin Affan (r.a.)"[97]

Lau kama Khalifa Uthman angetambua vyema yale aliyoyasema Mtume (s.a.w.w.) juu ya Marwan ibn al-Hakam, katu asingempatia nafasi hiyo aliyompa ya kuwa mshauri wake wa karibu, kwani alilaaniwa na Mtume (s.a.w.w.), na kumwita mjusi mtoto wa mjusi.[98] Baba wa Marwan (al-Hakam) ni yule ambaye naye pia alilaaniwa na Mtume (s.a.w.w.) kutokana na kumchezea shere Mtume (s.a.w.w.) na kuwaudhi majirani zake, Mtume (s.a.w.w.) alimuhamisha kutoka Madina, lakini Khalifa alimrejesha kutoka uhamishoni kwa vile alikuwa mjomba wake.

Sasa ikiwa mshauri wa karibu ni mtu wa aina hii, ni kitu gani kinachotarajiwa kutokea, ikiwa si uharibifu na ufisadi katika ardhi, na haya ndiyo yaliyotokea mpaka yakasababisha kifo cha Khalifa, kwa vile alikataa kata kata kumwajibisha pale Waislamu walipomuomba Khalifa amuwajibishe.

Mtu mwengine wa karibu ambaye ilipelekea Khalifa Uthman alaumiwe ni kumpa ugavana mtu ambaye Qur'ani imemueleza bayana kwamba ni fasiki, inasema:

---

[97] Muhammad Abdalla Riday, Masahaba kumi waliobashiriwa Pepo, Uk.37.
[98] Al-Halabiy, *As-Siratul Halabiyyah*, Jz. 1, Uk. 509.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنْ جَاءَكُمْ فَاسِقٌ بِنَبَإٍ فَتَبَيَّنُوا أَنْ تُصِيبُوا قَوْمًا بِجَهَالَةٍ فَتُصْبِحُوا عَلَى مَا فَعَلْتُمْ نَادِمِينَ وَاعْلَمُوا أَنَّ فِيكُمْ رَسُولَ اللَّهِ لَوْ يُطِيعُكُمْ فِي كَثِيرٍ مِنَ الْأَمْرِ لَعَنِتُّمْ وَلَٰكِنَّ اللَّهَ حَبَّبَ إِلَيْكُمُ الْإِيمَانَ وَزَيَّنَهُ فِي قُلُوبِكُمْ وَكَرَّهَ إِلَيْكُمُ الْكُفْرَ وَالْفُسُوقَ وَالْعِصْيَانَ أُولَٰئِكَ هُمُ الرَّاشِدُونَ فَضْلًا مِنَ اللَّهِ وَنِعْمَةً وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ

> "Enyi ambao mmeamini! Akiwajia fasiki na habari yoyote, ichunguzeni, msije mkawasibu watu kwa kutojua, na mkawa wenye kujuta kwa mliyoyatenda. Na jueni kuwa yuko kati yenu Mtume wa Mwenyezi Mungu. Lau angeliwatii katika mambo mengi, bila ya shaka mngelitaabika. Lakini Mwenyezi Mungu amewapendezea Imani, na akaipamba katika nyoyo zenu, na akauchukiza kwenu ukafiri, na upotovu, na uasi. Hao ndio walioongoka. Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu na neema Zake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye hikima." (Qur'ani 49:6-8)

Aya hii ilitosha kwa mtu huyo kutokupewa nafasi yoyote katika Dola ya Kiislamu, lakini kwa vile alikuwa mtu wa karibu wa Khalifa Uthman alimpa ugavana, na kwa vile alikuwa fasiki alikumbwa na kashfa ya ulevi, kiasi ambacho siku moja aliwaswalisha watu Swala ya asubuhi akiwa amelewa, badala ya kuswali rakaa mbili aliswali rakaa nne na kisha kuwageukia maamuma wake na kuwauliza: "Je, niwaongeze?"[99]

Ama kuhusiana na Muawiya, ambaye aliteuliwa kuwa gavana tangu katika zama za Khalifa wa pili na kuendelea kubakizwa katika

[99] *Usudul Ghabah*: Jz. 5,Uk. 91.

nafasi hiyo na Khalifa wa tatu, ni mtu ambaye pia alikuwa hastahiki kabisa kupewa nafasi hiyo kutokana na maneno ya Mtume (s.a.w.w.) pale aliposema:

"إذا رأيتم معاوية على منبري فقتلوه."

> "Pindi mutakapomuona Muawiya katika mimbari yangu, basi muuweni."[100]

Muawiya ndiye yule ambaye Mtume (s.a.w.w.) alimtuma mtu akamwite, alipofika alikuwa anakula chakula, Muawiya akamwambia yule mjumbe kwamba anakula, mjumbe akapeleka habari kwa Mtume, kwamba Muawiya anasema anakula, Mtume (s.a.w.w.) akamtaka mjumbe arudi tena kwa Muawiya, jawabu lake likawa ni kama lile la mwanzo, hapo Mtume (s.a.w.w.) alikasirika na kusema: "Katu Mwenyezi Mungu hatolishibisha tumbo lake."Wanahistoria wanaeleza kwamba Muawiya alikuwa akila mpaka akichoka kutafuna, kwani alikuwa hashibi.[101] Lakusikitisha kwa wapenzi wa Muawiya, wanaona laana hii ya Mtume (s.a.w.w.) kwa Muawiya kuwa ni fadhila kubwa kwake, kwa madai kwamba Mtume (s.a.w.w.) alimuomba Mola wake kwamba kila laana anayoitoa aigeuze kuwa ni kheri na baraka kwa huyo anayelaaniwa! Na wakati huo huo wamenakili riwaya inayosema kwamba siku moja Mtume (s.a.w.w.) alimkuta mtu anakula kwa mkono wa kushoto, akamuuliza kwa nini unakula kwa mkono wa kushoto? Yule mtu akajibu: "kwa sababu siwezi kula kwa mkono wa kulia." Mtume akamwambia: "Katu hutoweza." Basi ule mkono wake wa kulia ukapooza.

---

[100] Dhahabiy, *Mizanul-i'dital*, Jz. 2, Uk. 382.
[101] At-Tabariy, *Tarikh Tabariy*, Jz. 8, Uk. 186.

# MGAWANYIKO WA WAISLAMU

Wanasema:

> "Kifo cha Mtume kiliwagawa Waislamu makundi matatu. Ukoo wa Mtume (AhlulBayt), Muhajirina na Ansaar. Pamoja na kuwekwa sawa hali wapo waliondeleza vikundi vyao moyoni na pale upinzani ulipochukua umbo la kuonesha makosa serikalini. Bado lilikuwepo tatizo la mtu binafsi. Wapo Waislamu walioji-ingiza katika upinzani kwa maslahi yao binafsi. Mfano mzuri ni Muhammad bin Abu Bakar na Muhammad Hudhaifa."[102]

Mtume (s.a.w.w.) alitambua vyema kwamba baada yake kutatokea mgawanyiko kati ya Maswahaba wake, na mgawanyiko huo kufikia kiwango cha kuuwana wenyewe kwa wenyewe kama ilivyotokea katika historia ya Kiislamu, kwa hivyo alipangilia vyema mambo ya Waislamu ili pasitokee mgawanyiko na mtafaruku kati yao, ndio maana akawataka Maswahaba wampelekee wino na kalamu ili awaandikie usia ambao hawatopotea baada yake, lakini hawakukubaliana na amri hii ya Mtume (s.a.w.w.) na wakawa wanazozana kati yao, kwani kulikuwepo wale waliotaka apelekewe hicho alichoagiza na wengine wakakataa, hatimaye Mtume wa Mwenyezi Mungu akawafukuza kutoka katika hadhara yake tukufu!

Ama kuhusiana na tuhuma hii aliyotuhumiwa Muhammad ibn Abi Bakar, waandishi hao wamemtuhumu kwa sababu tu alikuwa ni kipenzi na mfuasi mtiifu wa Imamu Ali (a.s.), kwani hata yeye mwenyewe Imamu Ali (a.s.) hakusalimika na tuhuma zao, wamesema kwamba uteuzi wake haukuwa katika mfumo unaokubalika, kachaguliwa na wauwaji, vita alivyolazimishwa kupigana vilikuwa kwa ajili ya maslahi yake binafsi… Pia ni kwasababu Muhammad ibn Abi Bakar alikuwa mpinzani mkubwa wa siasa za Khalifa wa tatu, hasira zake dhidi ya Khalifa zilizidi pale watu wa Misri

[102] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk. 360.

walipokwenda Madina na kumueleza matatizo aliyonayo gavana wake wa huko, aliyekuwa akijulikana kwa jina la Sa'd ibn Abi Sarhi ambaye naye pia alikuwa ni katika watu wa ukoo wa Khalifa, na kumwambia kwamba hawamtaki na badala yake wanamtaka Muhammad ibn Abi Bakar, Khalifa aliwakubalia ombi lao, na wakati Muhammad alipokuwa safarini pamoja na ujumbe wake, njiani walimkuta mtumishi wa Khalifa Uthman akiwa amepanda farasi wa Khalifa, walimpekua na kumkuta na barua iliyoandikwa kupelekewa Sa'd ibn Abi Sarhi, ikimtaka awauwe watu hao na wengine wasulubiwe na wengine wakatwe mikono na miguu, barua hiyo ilikuwa na muhuri wa Khalifa Uthman.[103]

Baadhi ya waandishi wanasema kwamba barua hiyo, licha ya kuwa na muhuri wa Khalifa na kubebwa na mtumishi wake aliyekuwa akiitwa Abu Awar Assalamiy akiwa amepanda ngamia wa Khalifa, haikuandikwa na Khalifa, bali aliyeiandika ni Marwan ibn al-Hakam! Ikiwa ni hivyo, basi ni kwanini Khalifa hakumwajibisha Marwan? Huenda aliathirika zaidi na ile kauli isemayo: Damu ni nzito kuliko maji." Kwani Marwan alikuwa anatokana na ukoo wa Bani Umayya, alikuwa mtoto wa mjomba wake Uthman (Al-Hakamu aliyetimuliwa kutoka katika mji wa Madina, lakini Khalifa Uthman alimrudisha), na zaidi ya hayo alikuwa mkwe wake, kwani Uthman alimuozesha binti yake.

Hivi ndivyo historia ya Kiislamu ilivyochafuliwa, ule umoja na mapenzi yaliokuwepo katika zama za Mtume (s.a.w.w.) yalitoweka, ukabila, dhulma, na mauwaji yakutisha yakashika nafasi! *Innaa lillahi wainnaa ilayhi rajiuun!*[104]

---

[103] Masahaba Kumi Waliobashiriwa Pepo, Uk. 41

[104] Kwa nyongeza tu nakuomba ufuatilie kionjo hiki: Je unajua ni kwanini Waswahili walisema "Mungu si Athman?"
Na ni wakati gani husemwa kauli hii? Kawaulize Waswahili waliitoa wapi kauli hii na kwanini huitumia katika mazingira hayo – Mhariri.

# UPINZANI WAKATI WA UKHALIFA WA ALI

Katika mada hii wamesema yafuatayo:

"Kipindi cha Ukhalifa wa Ali hakukuwa na upinzani kutoka nje ya Dola ya Kiislamu. Na inaweza kusemwa kuwa hakukuwa na upinzani kwa sababu hapakuwa na kiongozi aliyechaguliwa kwa utaratibu unaokubalika na kwa sababu hii inakuwa vigumu kusema kulikuwa na upinzani ila kulikuwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe. Ni vigumu kusema kuwa Ali alikuwa ameteuliwa kwa utaratibu wa Uislamu kuwa khalifa. Wahaini wale baada ya kumuua Khalifa Uthman, mji wa Madina na serikali yake ilikuwa chini yao kwa muda wa siku sita na swala ya Ijumaa waliendesha wao."[105]

Waislamu wa madhehebu mbalimbali wanatambua utukufu wa Imamu Ali ibn Abi Talib (a.s.) na wengi wao wanaitakidi kwamba ni mmoja kati Makhalifa waongofu, na hata wale waliosimamia utayarishaji wa Kitabu hicho kijulikanacho kwa jila la ' Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha Nne.' Wasimamizi hao ni Bakwata na Wizara ya Elimu Zanzibar. Waislamu wanaofanya kazi katika vitengo hivi viwili ni wafuasi wazuri wa Madhehebu ya Imamu Shafi, tumeona ni namna gani Imamu Shafi alivyokuwa akiwasifu na kuwaheshimu Ahlul-Bayt wa Mtume (s.a.w.w.) akiwemo Imamu Ali (a.s.). Imamu Shafi alikuwa mmoja wa watu waliopelekwa Iraqi kutoka Yemen wakati wa utawala wa Harun Rashid, huku wakiwa wametiwa minyororo shingoni mwao na miguuni mwao kwa tuhuma kwamba wao ni Mashia, baada ya kufika huko kila mmoja alitakiwa aingie sehemu aliyokuwa amekaa Harun Rashid,

[105] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk. 367.

kila aliyeingia huko alikatwa kichwa chake, na Imamu Shafi ndiye mtu pekee aliyesalimika na kifo hicho cha kidhulma na kinyama.[106]

Sidhani kwamba wasimamizi hao wanakubaliana na maandiko haya. Ikiwa Imamu Ali (a.s.) hakuchaguliwa kwa njia inayofaa, ni maandiko gani matakatifu yanayotoa ruhusa kumpiga vita na kusababisha mauwaji ya maelfu ya Waislamu katika vita vya Ngamia chini ya uongozi wa Bibi Aisha na vita vya Siffin chini ya uongozi wa Muawiya?!

Wanaendelea kusema:

> "Siku ya sita Ali alitangazwa kuwa khalifa na wauwaji. Aisha, Talha na Zubeir ni vigumu kusema kuwa waliupinga Uislamu walipopigana na Ali katika vita vya ngamia, na vile vile ni vigumu na haiwezekani Muawiya alipokataa kumtii Ali alikuwa amekosea hivyo alipinga Uislamu alipopigana na Ali katika vita vya Sifin. Tunachoweza kusema wakati wa Ali kulikuwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe. Katika vita hivyo, nani alipigania Uislamu, nani alipigania kundi lake au ukoo wake au udugu au kabila lake n.k. ni maoni ya kila mwanahistoria baada ya kujua mkondo wa matukio ya historia."[107]

Tumeshaeleza huko nyuma, namna Sheikh Muhammad Kasim Mazrui alivyosema jinsi makundi ya Maswahaba wa Mtume walivyomkimbilia Imamu Ali (a.s.) na kumtaka ashike nafasi ya Ukhalifa, na pale alipokataa kutokana na hali ilivyokuwa imeharibiwa na watawala waliopita alikataa katakata, lakini walimlazimisha, na hatimaye akakubali.

Lakini kwa faida zaidi, yasome haya aliyoyaandika At-Tabariy katika kitabu chake: "Na Ahmad ibn Hanbal amepokea kwa sanadi

[106] *Kitabul Ummi*. Imamu Shafi: Jz. 1, Uk. 9.
[107] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk. 367.

yake kutoka kwa Muhammad ibn Hanafiyya, amesema: "Nilikuwa pamoja na Ali wakati Uthman alipokuwa amezingirwa, mtu mmoja alimuendea na kusema: Kiongozi wa Waumini (Uthman) ameuwawa. Ali alikwenda nyumbani kwake na akaingia ndani na akafunga mlango, mara watu wakamuendea na wakahodisha na kisha kuingia, kisha wakamwambia: Mtu huyu (Uthman) amekwishauwawa, na hakuna budi kwa watu isipokuwa wawe na Khalifa, na hatujamuona yeyote anayestahiki zaidi kuliko wewe. Ali aliwaambia: Hapana musinichague mimi, kwa kweli mimi kuwa waziri wenu ni bora zaidi kuliko kuwa amiri (Khalifa).Walisema: Hapana, kwa jina la Mwenyezi Mungu! Hakuna yeyote anayestahiki zaidi kuliko wewe. Akasema: Ikiwa mutanikatalia, basi viapo vyenu vya utiifu kwangu visiwe kwa siri, bali nitatoka niende msikitini, na atakaye kunipa kiapo cha utiifu atanipa. Basi alitoka na kwenda msikitini na watu wakampa viapo vyao vya utiifu.''[108]

Riwaya hii inajulisha mambo yafuatayo:

1. Imamu Ali (a.s.) hakuwa na tamaa ya kutaka uongozi, kwani alijiweka nyumbani kwake, mpaka pale Maswahaba walipomuendea wakimtaka awe Khalifa wao.

2. Maanswari na Muhajirina pamoja na watu wote kwa ujumla, ndio waliomuendea Imamu Ali na kumtaka akubali kuchukua viapo vyao vya utiifu wa kuwa Khalifa wao, walimsisitiza sana mpaka akakubali.

3. Kwa mujibu wa mitazamo ya Maswahaba ni kwamba zama hizo mtu aliyestahiki zaidi kuwa Khalifa ni Imamu Ali (a.s.), hii inatokana na msisitizo wao kwake ili akubali kuchukua viapo vya utiifu kutoka kwao, na pia kutoka na kauli yao

[108] *Fadhailu Swahaba*: Jz. 2, Uk. 573, *Tarikh Tabariy*: Jz. 4, Uk. 427.

kwamba: Hawamuoni yeyote anayestahiki zaidi kuwa Khalifa kuliko yeye.

4. Kupatikana makubaliano ya Muhajirina na Maanswari juu ya Ukhalifa wa Imamu Ali (a.s.), na ni watu wa Sham tu ndio ambao walimkataa, na jambo hili halidhuru baada ya makubaliano ya watu wa Madina.[109]

Na hiki kilichoelezwa na waandishi hawa wawili ni kwa misingi ya kwamba ukhalifa hupatikana kwa njia ya uchaguzi, na hili ndilo ambalo Imamu Ali (a.s.) hakulipenda, kwa hivyo alisema:

"Kwa hakika mimi kuwa waziri wenu ni bora kuliko kuwa amiri (Khalifa)."

Ama kwa mujibu wa misingi iliyo sahihi, ni kwamba Ukhalifa hupatikana kwa uteuzi kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na si juu ya Imamu kuukataa, lakini kutokana na watu kulikataa hili tangu mwanzoni kabisa, na wakawa wanaendelea kuchaguana, Imamu Ali hakupenda kuutwaa Ukhalifa kwa mujibu wa matakwa yao, ili isionekane kwamba ni wao waliomchagua kama walivyochaguliwa watangulizi wake kwenye nafasi hiyo, mpaka walipokiri wenyewe kwamba hawamuoni anayestahiki zaidi yake yeye.

Pamoja na ushahidi huu ulio wazi, kwa mujibu wa misingi ya watu (kiongozi huchaguliwa), ushahidi ulioko katika riwaya ya Ahmad ibn Hanbal, ambayo ni sahihi na wapokezi wake ni madhubuti, wapokezi waliopokea katika riwaya za Bukhari na Muslim, je kutakuwa na shaka yoyote juu bai'a ya Muhajirina na Maanswari kwa Imamu Ali (a.s.)?

---

[109] *Bai'atu Ali ibn Abi Talib fii Dhaw'I Riwayat Aswahiiha Liummi Malik al-Khalidiy wa Hasan Farhaniy al-Malikiy*:
Uk. 104-105.

Na je, ni haki kwa mtu mwadilifu kuyakubali maneno yao, ya kwamba Imamu Ali (a.s.) alichaguliwa na wauwaji, kwa hivyo uteuzi wake haumo katika utaratibu wa Kiislamu katika kumpata kiongozi?! Sijui hao Muhajirina na Maanswari ndio wauwaji wanaowakusudia au kuna wengine?!

Pia si sahihi kwa watu walioishi pamoja na Mtume (s.a.w.w.) kuachiwa wanahistoria waamue ni nani alikuwa katika haki na yupi alikuwa katika batili kutokana na yale yaliyojiri kati yao. Kwani Mtume (s.a.w.w.) aliyaeleza yote yatakayojiri kati yao na kubainisha ni nani yuko sahihi na ni nani hayuko sahihi, ni vyema katika hili turudi katika maandiko matakatifu yatuamulie, ili ukweli ujulikane, badala ya kuwaachia tu wanahistoria kuamua kwa mujibu wa utashi wao.

Bila ya shaka, Mtume (s.a.w.w.) alibainisha yale yaliotokea kati ya Maswaha kabla ya kutokea kwake, na kuweka bayana ni nani yuko katika haki. Kila aliyepitia maelezo yetu huko nyuma atagundua hilo, na zaidi ya hayo tutayabainisha zaidi huko mbeleni.

Wameeleza kwamba vita hivyo vilikuwa ni vita vya wenyewe kwa wenyewe, ni kweli vita hivyo vilikuwa tofauti na vile vita vilivyopiganwa katika uhai wa Mtume (s.a.w.w.), kwani ilikuwa ni dhidi ya Makafiri, lakini haina maana kwamba vita vya Waislamu wenyewe kwa wenye pande zote zinakuwa ziko kwenye haki au kwenye batili, bali Mwenyezi Mungu ameliweka wazi jambo hili katika Kitabu Chake, kama anavyosema:

وَإِنْ طَائِفَتَانِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ اقْتَتَلُوا فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُما فَإِنْ بَغَتْ إِحْداهُما عَلَى الأُخْرى فَقاتِلُوا الَّتِي تَبْغِي حَتَّى تَفِيءَ إِلى أَمْرِ اللهِ...

> "Na ikiwa makundi mawili katika waumini yanapigana, basi yapatanisheni. Na likiwa moja la hayo linadhulumu jingine, basi lipigeni linalodhulumu mpaka lirejee kwenye amri ya Mwenyezi Mungu.…" (Qur'ani, 49:9).

Hivi kweli anayedhulumu na anayedhulumiwa wote wako katika haki? Na kama wote wako kwenye haki kwa nini basi Allah aseme: **'basi lipigeni linalodhulumu mpaka lirejee kwenye amri ya Mwenyezi Mungu.'** Au kwao waandishi hawa kwenda kinyume na Aya ya Mwenyezi Mungu si kukosea? Au kwao wao watu wanapokuwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe basi wote wenye kupigana wako katika haki, na inaruhusiwa yeyote kumuuwa mwingine maadamu tu ni vita vya wenyewe kwa wenyewe, au ndio kusema Uislamu unaruhusu vita vya wenyewe kwa wenyewe? Akili gani hii? Mnapelekwa wapi na upofu wa moyo? Au wamejisahaulisha kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo:

وَمَنْ يَقْتُلْ مُؤْمِنًا مُتَعَمِّدًا فَجَزَاؤُهُ جَهَنَّمُ خَالِدًا فِيهَا وَغَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَلَعَنَهُ وَأَعَدَّ لَهُ عَذَابًا عَظِيمًا

> "Na mwenye kumuua muumini kwa kukusudia, basi malipo yake ni Jahannam, ni mwenye kudumu humo; na Mwenyezi Mungu amemughadhibikia na amemlaani na amemwandalia adhabu kubwa." (Qur'ani 4: 93).

Au ndio kusema vita vya watu wa familia moja, au dini moja au taifa moja havihusiki na Aya hizi hata kama vimeteketeza nafsi za Waumini, vimeleta uharibifu ndani ya jamii, vimezalisha wajane na mayatima? Au mkosefu na haini ni yule tu aliyeandaa na kushawishi mauaji ya Khalifa Uthmani, yule nyota wa mchezo waliyembuni kwa

jina la Ibn Saba? Ama yule kiumbe halisi na mhusika halisi aliyeandaa, kuratibu na kushawishi mauwaji ya maelfu ya Waislamu katika vita vya Ngamia na Suffin, huyo ni mtu safi, hana makosa na wala haipasi kulaumiwa!Ni wazi kwamba vita hivyo vilivyotokea kati ya makundi mawili ya Waislamu, mojawapo lilikuwa katika haki, na haya ameyabainisha wazi Mtume (s.a.w.w.) kama utakavyoona.

Wanaendelea kusema:

> "Jambo la kusikitisha ni kuwa kipindi cha Khalifa Ali kilitawaliwa na mapigano baina ya wenyewe kwa wenyewe baina ya Khalifa na Aisha, Talha na Zubeir, Khalifa na Khawarij na Khalifa na Muawiya Gavana wa Syria."[110]

Ni kweli ni jambo la kusikitisha kwa Maswahaba wakubwa na wazito, kuanzisha vita dhidi ya Khalifa na Imamu wao, hasa kwa wale waliokuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha Imamu Ali (a.s.) anashika Ukhalifa, watu hao ni Talha na Zubeir, lakini kumbe walikuwa na ajenda zao, ambapo walitarajia kuwa iwapo Imamu Ali atakabidhiwa mamlaka ya kuwaongoza Waislamu, basi wao watapata Ugavana, Zubeir katika jimbo la Kufah, na Talha katika jimbo la Basra, walipoukosa ndipo walipoanzisha uasi dhidi yake, ni kweli inasikitisha hasa tukiyaangalia na kuyatia akilini maandiko haya matakatifu kutoka kwenye kinywa cha Mtume Mtukufu (s.a.w.w.) pale aliposema:

> "Mwenye kufa katika hali yakuwa ni mwenye kuwafarakisha watu, basi mtu huyo atakufa kifo cha kijahili."[111]

Na pia ndugu msomaji yasome maneno haya ya Mtume (s.a.w.w.) kwa makini pale alipomuambia Imamu Ali:

---

[110] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk. 367.
[111] *Musnad Imami Ahmad*: Jz. 2, Uk. 133.

> "Kwa hakika, hakupendi wewe isipokuwa Muumini na hakuchukii isipokuwa mnafiki."[112]

Baada ya hapo wanaelezea namna hali ilivyokuwa, wanasema:

> "Baada ya kuuawa kwa Khalifa Uthman na kutawazwa kwa Ali baadhi ya jamaa wa Khalifa walikwenda Makka kueleza tukio lilivyokuwa, mama wa waumini Bi Aisha alistushwa sana na tukio hili, lakini lililotisha zaidi ni hatua ya Khalifa ya kuahirisha adhabu ya waliomuuwa Khalifa Uthman kwa hoja kuwa kwanza arudishe amani nchini kisha ndipo awaadhibu wauwaji. Hoja hii ilikuwa ni ngumu kueleweka hasa ukizingatia mambo matatu. Kwanza mwanzilishi wa ghasia na hatimaye kufikia kifo cha Khalifa Uthman alifundisha imani ya wasii wa Ali. Pili hilo ndilo lililomuweka Ali madarakani na tatu, wauwaji hawa pamoja na kuambiwa waondoke Madina siku ya tatu ya Ukhalifa wa Ali kundi la Saba lilikhalifu amri ya Khalifa na kuendelea kubaki madina kwa kisingizio cha urafiki. [113] Mama wa waumini ambaye alikuwa anarudi Madina kutoka kwenye Hija Makka alirudi Makka na kuwaomba watu kwenda kulipiza kifo cha Khalifa. Maswahaba maarufu Talha na Zubeir walimuunga mkono na wakawa naye. Wapiganaji 2000 walipatikana. Lakini walipokuwa wanakwenda Madina wakapata wazo la kupita Basra kupata watu wengi walipokuwa njiani kuelekea Basra alikuwa na watu 3000 chini ya Bendera yake."[114]

Ni kweli mama wa Waumini, Bibi Aisha alistushwa sana, lakini lililomstusha si kifo cha Khalifa Uthman, kwani yeye ndiye aliyewaamrisha watu wamuuwe baada ya kukasirishwa kutokana na siasa zake, Bibi Aisha alisema: "Muuweni mpumbavu, kwani amekufuru."[115]Bali

---

[112] *Musnad Ahmad*: Jz.1,Uk. 138. *Sunan Tirmidhiy*: Jz. 5, Uk. 343. *Sahihi Muslim*: Jz. 1, Uk. 86.

[113] Dr. M.A. Khan: The pious caliphs, uk. 186

[114] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk. 367.

[115] *Tarikh Tabariy*, Jz. 4, Uk. 407. *Tarikh ibn al-Athir*, Jz. 3, Uk. 206, *Lisanul al-Arabi*, Jz. 14, Uk. 193, *Taj al-Arus*, Jz. 8, Uk. 141.

lililomstusha na kumkasirisha sana ni pale alipopewa habari kwamba baada ya kifo cha Khalifa, aliyechaguliwa kuwa Khalifa ni Ali ibn Abi Talib (a.s.), ndio maana akaandaa jeshi kubwa akishirikiana na Talha na Zubeir dhidi ya Khalifa wa Waislamu!

Kuhusiana na sababu ya kifo cha Khalifa, tumebainisha namna Sheikh Muhammad Kasim Mazrui alivyosema kwamba Marwan ndiye aliyemsababishia kifo. Na tumeeleza namna watu wa majimbo mbalimbali walivyopeleka malalamiko yao dhidi ya magavana walioteuliwa na Khalifa Uthman, ambao wengi wao walikuwa ni katika jamaa zake ambao hawakuwa watu wema, kwani wengine Mwenyezi Mungu amewaeleza kuwa ni mafasiki, wengine wamelaaniwa… Badala ya watu kuelezwa ukweli, kilichofanyika ni kuambiwa kwamba, mwanzilishi wa ghasia na hatimaye kufikia kifo cha Khalifa Uthman alifundisha imani ya wasii wa Ali.

Ikiwa Khalifa Ali aliwaambia watu wafanye subira mpaka hali itakapotulia, ndipo awachukulie hatua wale waliomuuwa Khalifa Uthman, je Khalifa hakuwa na haki ya kutoa maamuzi na raia kuwa na haki ya kumtii Khalifa? Je Imamu Ali (a.s.) hakuwa miongoni mwa watu walio na mamlaka miongoni mwa Waumini ambao ni wajibu kutiiwa kama Mwenyezi Mungu alivyoagiza katika Kitabu Chake pale aliposema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ أَطِيعُواْ اللَّهَ وَأَطِيعُواْ الرَّسُولَ وَأُوْلِي الأَمْرِ مِنكُمْ فَإِن تَنَازَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللّهِ وَالرَّسُولِ إِن كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللّهِ وَالْيَوْمِ الآخِرِ ذَلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلاً

"Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume na wenye madaraka katika nyinyi. Na mkizozana katika jambo basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, ikiwa mna-

> muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Hayo ndiyo bora zaidi na ndiyo yenye mwisho mwema." (Qur›ani 4:59).

Kama kuna mtu yeyote alifundisha imani ya uwasii wa Imamu Ali (a.s.), itakuwa amefanya yale yanayomridhisha Mwenyezi Mungu, kwani Hadithi Sahihi mbalimbali tulizozibainisha zinaonesha kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliusia kwamba haki ya Ukhalifa ni ya Ahlul-Bayt kwa kuanzia Imamu Ali (a.s.), kwa hivyo hilo si kosa na wala si uzushi, kwani huo ndio mwenendo wa Mwenyezi Mungu, bali ni katika mambo yanayomkurubisha mja karibu na rehema za Mwenyezi Mungu. Mtu wa aina hiyo atakuwa amemfahamu vyema Mtume (s.a.w.w.) pale aliposema:

إنّي تاركم فيكم الثقلين كتاب الله وعترتي وإنّهما لم يفترقا حتى يردا عليّ الحوض.

> "Hakika mimi ninawaachieni vizito viwili, Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Kizazi changu, na viwili hivyo havitaachana mpaka vitakapo nifika katika Hodhi.[116]

Pia Mtume (s.a.w.w.) alisema kwa kukariri mara tatu juu ya kushikamana na Ahlulbayt wake, hiyo inamaanisha namna alivyokuwa akisisitiza juu ya jambo hilo:

أذكركم الله في أهل بيتي أذكركم الله في أهل بيتي أذكركم الله في أهل بيتي...

[116] Tafsir Ibnu Kathir Jz. 4, Uk. 122

> "…nakukumbusheni Mwenyezi Mungu kuhusu watu wa nyumba yangu, nakukumbusheni Mwenyezi Mungu kuhusu watu wa nyumba yangu…"[117]

Na pale baadhi ya watu walipokwenda kutia chokochoko dhidi ya Imamu Ali (a.s.), Mtume (s.a.w.w.) aliwakasirikia na kusema kama Imamu Ahmad ibn Hanbal anavyosimulia:

"Ametusimulia Abdu Razzaq, ametusimulia Ja'far ibn Sulayman, amenisimulia Yazid Arrishki, kutoka kwa Mitraf ibn Abdillah, kutoka kwa Imran ibn Huswein, amesema: Mtume (s.a.w.w.) alipeleka kikosi cha wapiganaji, na akamfanya Ali kuwa kiongozi wao, katika safari yake Ali alifanya jambo fulani, watu wanne miongoni mwa Maswahaba wa Mtume (s.a.w.w.) waliazimia kulifikisha jambo hilo kwa Mtume (s.a.w.w.).

Imran akasema: Ilikuwa pale tunaporudi kutoka katika safari, kwanza tukifikia kwa Mtume (s.a.w.w.), na kumsalimia. Akasema: Waliingia, na mtu mmoja miongoni mwao alisimama na kusema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Hakika Ali amefanya jambo hili na lile. Mtume (s.a.w.w.) aliwageuzia uso. Kisha akasimama mtu wa pili, naye akasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Hakika Ali amefanya jambo hili na lile. Mtume (s.a.w.w.) aliwageuziauso. Kisha alisimama mtu wa tatu, naye akasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Hakika Ali amefanya jambo hili na lile. Kisha alisimama mtu wa nne, naye akasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Hakika Ali amefanya jambo hili na lile.Akasema: Mtume (s.a.w.w.) alimuelekea mtu wanne na huku uso wake ukiwa umebadilika rangi, akasema: Mwacheni Ali, mwacheni Ali, mwacheni Ali, kwani Ali anatokana na mimi, na mimi natokana na yeye, na yeye ni Kiongozi wa kila Muumini baada yangu."[118]

---

[117] *Sahihi Muslim* Jz. 7, Uk. 123

[118] *Sunan Tirmidhiy*: Jz. 5, Uk. 296.

Na pia Hadithi hii ameisimulia Abu Ya'laa al-Muswiliy, kutoka kwa Ubeydullah ibn Umar al-Qawaririy, kutoka kwa Ja'far ibn Suleyman, kwa sanadi iliyotangulia. [119] Na ibn Abi Shayba [120] ameisimulia, na pia Habban katika *Sahihi* yake [121], Abu Naim al-Asfahaniy katika '*Hilyatul- Awliyai'*[122] na Muhibbu Diyn Tabariy, [123] Al-Baghwiy, [124] ibn Kathir katika kitabu chake cha historia, [125] As-Suyutiy, [126] na al-Muttaqiy. [127]

Na kuna wapokezi wengine wa hadithi waliopokea ya kwamba Mtume (s.a.w.w.) alisema:

"Mnataka nini kwa Ali? Mnataka nini kwa Ali? Mnataka nini kwa Ali? Hakika Ali anatokana na mimi na mimi natokana na Ali, na yeye ni Kiongozi wa kila Muumini baada yangu." Walioipokea kwa maneno haya ni: Tirmidhiy, amesema: Hadithi hii ni nzuri iliyo ngeni, [128] An-Nasaiy, [129] Muhibbu Diyn, [130] na ibn Hajar, [131] wamesema: Sanadi yake ni yenye nguvu. Na pia kuna sanadi nyingine ya hadithi hii, nayo ni: Amesimulia Abu Daud Tayalasiy, kutoka kwa Abi Awana, kutoka kwa Abi Balji, kutoka kwa Amru ibn Maymun, kutoka kwa ibn Abbas, Mtume (s.a.w.w.) amesema kumuambia Ali: "Wewe ni Kiongozi wa Kila Muumini baada yangu."[132] Na sanadi yake ni sahihi na wapokezi wake wote ni madhubuti.

[119] Musnad Abi Ya'laa: Jz. 1, Uk. 203.
[120] Al-Muswanif: Jz. 12, Uk. 180.
[121] Sahihi ibn Habban: Jz. 5, Uk. 374.
[122] *Hilyatul-Awliyai*: Jz. 6, Uk. 294.
[123] Riyadhun Nadhira: Jz. 3, Uk. 116.
[124] Maswabihu Sunna: Jz. 4, Uk. 172.
[125] Albidaya wannihaya: Jz. 7, Uk. 381.
[126] Jamiul Hadith, Jz. 4, Uk. 352.
[127] Kanzul-Ummal: Jz. 11, Uk. 608, Hadith Na. 32940, 23941.
[128] Sunan Tirmidhiy: Jz. 5, Uk. 590.
[129] Khaswaiswu Amiril Muuminina, Uk. 92.
[130] Riyadhun Nadhra: Jz. 3, Uk. 115
[131] Al-iswaba: Jz. 2, Uk. 509.
[132] *Mustadrak Abi Daud Tayalasiy*: Uk, 360, Hadithi Na.2752.

Hayo ndiyo maandiko sahihi yanayothibitisha kwa wazi kwamba Imamu Ali (a.s.) ndiye aliyestahiki kushika mamlaka ya uongozi wa Waislamu mara tu baada ya kufariki Mtume (s.a.w.w.), kwa hivyo bila shaka yeyote mwenye kuyafundisha haya atakuwa na malipo makubwa mbele ya Mwenyezi Mungu.

Ama kule kudaiwa kwamba mfundishaji wa haya alikuwa ni myahudi aliyejulikana kwa jina la Abdullah ibn Sabaa, haya tumeyaeleza katika kurasa za mbele.

Kwa kweli ni masikitiko mengine makubwa kwa Mama wa Waumini kuwahamasisha watu wengine ili wapambane dhidi ya watoto wake wengine, na yeye kuongoza mapambano hayo akiwa katikati ya wanaume, badala ya kuwa msuluhishi, licha ya kwamba Mwenyezi Mungu amewataka mama zetu hao wakae majumbani mwao, kama anavyosema:

وَقَرْنَ فِي بُيُوتِكُنَّ وَلا تَبَرَّجْنَ تَبَرُّجَ الْجاهِلِيَّةِ الأُولى وَأَقِمْنَ الصَّلاةَ وَآتِينَ الزَّكاةَ وَأَطِعْنَ اللهَ وَرَسُولَهُ...

> "Na kaeni majumbani mwenu, wala msioneshe mapambo yenu kama walivyokuwa wakionesha mapambo yao wanawake wa zama za ujahili (ujinga na ukafiri), na simamisheni Swala na toeni Zaka, na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake…" (Qur'ani, 33:33).

Lau kama mama wa Waumini angejilazimisha na mafunzo haya matakatifu, basi hayo mapambano yake dhidi ya Khalifa Ali (a.s.) yasingetokea na damu ya watoto wake pamoja na roho zao zingesalimika.

Wanaendelea kusema kuhusiana na tukio hili la kuhuzunisha:

> "Gavana wa Basra Uthman bin Hanif alituma watu ili kujua lengo la ziara ya Bibi Aisha Basra. Wajumbe wa Gavana walifahamishwa kuwa yeye mama Aisha na (uk.367) Waislamu wengine walitaka kuwakumbusha Waislamu juu ya wajibu wao kwa Khalifa aliyeuwawa. Na dhima yao ni kuwaadhibu wauwaji. Kusikia hivi Gavana alizuia msafara usiingie Basra. Kwa hiyo akaita mkutano na kuwaamuru watu wake wawapige Mama Aisha na wenzake baada ya kupata maelekezo kwa Khalifa Ali. Watu wake waligawanyika, kuna waliomuunga mkono yeye na wapo waliomuunga mkono Gavana. Mama Aisha alitoa Hotuba ambayo iliwezesha kuwateka nusu ya watu ambao mwanzoni walimuunga mkono Khalifa. Kuona hivi mama Aisha alitaka suluhu lakini upande wa gavana kulikuwa na watu wa Saba ambao suluhu hawakuitaka, Hakim bin Hublan akiwa kiranja wa kundi hili lisilotaka suluhu alivamia jeshi la Mama Aisha r.a. hata kabla ya ruhusa ya gavana wake na uchokozi huu vita vikaanza, gavana akatekwa, Hublan na wenzake wengi wapatao 600 wakauwawa na Basra ikatekwa na kuwa chini ya Bibi Aisha, Talha na Zubeir."[133]

Hivi ndivyo hali ilivyokuwa huko Basra, lakini si sawa kwamba kulikuwa nawatu wa Saba (Abdullah ibn Saba) ambao walikataa suluhu. Ni kwamba kulikuwa hakuna mtu huyo, na pia safari ya Bibi Aisha ilikuwa na lengo moja tu, ambalo ni kupambana na Khalifa wake. Ikiwa Hakim bin Hublan alivamia jeshi la Mama Aisha hata kabla ya ruhusa ya gavana wake na uchokozi huu vita vikaanza, kama walivyoandika, basi ni kwamba hata huyo kamanda wa vita aliyetoka Madina akielekea Basra akiwa amekhalifu amri ya Mola wake, kwani Mwenyezi Mungu amemuamrisha yeye pamoja na wake wenzake wa Mtume (s.a.w.w.) kubakia katika majumba yao. Na pia Hadithi mbalimbali za Mtume (s.a.w.w.) zinazoashiria waji-

[133] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk. 367-368.

bu wa kuwapenda Ahlul-Bayt wa Mtume (s.a.w.w.) na zaidi tutaona Hadithi za Mtume (s.a.w.w.) zinazobainisha ni nani alikuwa sahihi katika vita hivi.

Waislamu waelewe kwamba huyo Gavana aliyetekwa na jeshi la mama wa Waumini ni Uthman ibn Hunayf, ambaye alikuwa ni Swahaba mwema wa Mtume (s.a.w.w.), baada ya kumteka waliingia katika nyumba ya kuihifadhia mali za Waislamu (Hazina ) na kuzigawa kwa wanajeshi wa jeshi la Bibi Aisha, na huyo Gavana wakamnyonyoa ndevu zake zote! Baada ya Imamu Ali (a.s.) kuwasili Basra, Gavana huyo alimwambia Imamu Ali a.s: “Ewe Amirul-Muuminina, umenipeleka Basra nikiwa na ndevu, na leo nakujia uso mtupu hauna hata unywele mmoja kama kijana kibarobaro tu.” Sayyidna Ali akamjibu: “Umepata kheri na thawabu.”[134]

Wanaendelea kusema:

“Khabari za kutekwa Basra zilimchukua kwa mshangao mkubwa Khalifa Ali ambaye alikuwa aende Syria kumrudi Muawiya alilazimika kwenda Basra kwanza kutuliza hali ya kule.

Alipofika Dhi-Qar’a mahali karibu na Basra alituma ujumbe kwa Aisha, Talha na Zubeir wafanye mazungumzo ya amani. Nafasi ilipatikana mazungumzo yakafanywa na wakati karibu kukubaliana baada ya Ali kuahidi kuwa atawaadhibu wauwaji wa Uthman Dola itakapokuwa na amani. Lakini mpango wa amani haukuwa na maslahi kwa lile kundi la Ibn Saba ambalo lilifanya sehemu ya jeshi la Ali. Walinong’onezana kuwa Ali anataka kufanya makubaliano ya amani na ameahidi kuwaadhibu waliomuua Uthman. Kundi hili lililokuwa ndilo lililomuua Khalifa Uthman halikupendezwa na mpango huu wakaunda hila iliyochochea kutokea vita. Mbinu mbili walizitumia. Kwanza walipeleka umbea Basra kuwa Ali akiingia Basra atawa-

[134] Masahaba Kumi waliobashiriwa Pepo, Uk. 68

fanya watumwa wakazi wote na atawaua vijana wote. Kwa sababu hii watu wa Basra lazima wapigane. Ibn Saba na wachochezi wake usiku usiku walivamia jeshi la mama Aisha ambaye aliarifiwa na kwa namna hii vita vikaanza. Vita hivi vinajulikana kwa jina la vita vya ngamia.

Vita vilikuwa vikali kwa vile ukubwa wa jeshi ulilingana. Hata hivyo baada ya mapigano makali na kuuwawa Waislamu wapatao elfu kumi. Hata hivyo ushindi ulikuwa wa Ali. Talha alikufa, Zubeir aliacha kupigana na akawa anaelekea Madina ndipo akauliwa njiani, Talha aliuliwa vitani. Wakati wote wa vita mama Aisha alikuwa katika sehemu ya uwanja wa vita akiwa amepanda ngamia, kuwepo kwake kulifanya mapigano yaende kwa kasi kubwa, bila kukoma, ndipo Ali alipoamuru ngamia wake akatwe miguu ya nyuma. Ngamia alianguka miguu yake ya mbele na kwa heshima zote akatolewa ndani ya kikalio cha ngamia na vita vikaisha, ushindi ukawa upande wa Khalifa Ali. Mama Aisha akasindikizwa Madina na kaka yake Muhammad bin Abi Bakr.

Baada ya vita alizungumza na Waislamu katika msikiti wa Basra na Waislamu wakampa mkono wa utii. Alipoondoka alimuacha Abdallah bin Abbas kuwa Gavana wa Basra. Yasemekana roho za Waislamu elfu kumi zilipotea."[135]

Hapa wameeleza tena kwamba kundi la Sabaa (Abdullah ibn Sabai), halikupendezewa na suluhu, kwa vile wao ndio waliomuuwa Khalifa Uthman. Tumeeleza huko nyuma kwamba, Khalifa alikosa watu wa kumtetea kwani hata baada ya kifo chake mwili wake ulibakia siku tatu, na baada ya hapo ukazikwa katika makaburi ya mayahudi, baada ya Waislamu kukataa usizikwe kwenye makaburi ya Waislamu, tena bila ya kuoshwa na kuvishwa sanda na walioshiriki maziko yake hawazidi watu kumi. Basi hao wapenzi wa Khalifa

[135] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk. 378.

Uthman waliokusanya jeshi kubwa walikuwa wapi? Na pia miongoni mwa watu waliotoa amri ya kuuwawa ni mama wa Waumini, na wale walioshiriki katika mzingiro wa Khalifa Uthman, na kumuwekea vikwazo mbalimbali ili kutoa shinikizo la kujiuzulu alikuwemo Talha na Zubeir.

Pengine dhana hii ya kwamba Bibi Aisha aliwaamrisha watu wamuuwe Khalifa Uthman kama ilivyonakiliwa na At-Tabariy katika *Tarikh* yake, itakuwa nzito katika baadhi ya masikio ya watu, basi ikumbukwe kwamba ni Bibi Aisha huyo huyo ndiye aliyekusanya jeshi kubwa kwa ajili ya kumuua kiongozi wa Waumini Imamu Ali (a.s.), kwani mlengwa mkubwa katika mapambano yoyote ni kiongozi wao. Bila ya shaka yoyote wangekuwa na uwezo wa kumfikia wangemuua.

Haya ndiyo waliyoyaandika kuhusiana na vita hivi vya Ngamia chini ya jemedari mkuu Bibi Aisha binti Abi Bakar dhidi ya Khalifa Ali (a.s.).

Katika kuweka wazi zaidi ili kujua wale waliokuwa sahihi katika vita hivyo, basi tumsikilize Sheikh Muhammad Kasim Mazrui anavyosema katika maudhui aliyoyaita 'Mwana Aisha na mbwa wa Haw'ab':

"Likatoka jeshi la watu 3000 kwenda Basra, na Mw. Aisha pamoja nao, amepandishwa ngamia. Kufika mahala paitwapo Haw'ab ambapo palikuwa na mbwa wengi, walipoona jeshi la watu wa ngamia, wale mbwa wakalia na kufanya ghasia. Mw. Aisha akashituka na kuuliza: "Ni mahali gani hapa?" Akaambiwa ni Haw'ab. Kusikia vile mara alipiga ukelele wa kilio na huku akisema: "Wele wangu! Niregezani! Niregezani! (Nirudisheni) Nilimsikia Mtume (s.a.w.w.) siku moja akiwambia wakeze: Nani katika nyinyi atakayeliliwa na mbwa wa Haw'ab." Siku hiyo sote tulistaajabu, tukaona itakuwa-

je hata mke waMtume afike mahali hapo? Leo nimejijua kuwa ni mimi! Sitaki tena kwenda Basra. Niregezeni! Niregezeni!! Akisema hivi na huku alimketisha ngamia, hataki tena kwenda mbele. Jamaa wakajaribu kumbembeleza na kusema nae, lakini asiwakubalie kabisa, akawashikilia kuwa lazima arudi. Walipokosa budi, ndipo walipomtisha, wakamwambia: "Jeshi la Ali karibu litakutana, na yeye ashapata khabari kuwa wewe ndiye adui mkubwa, basi usipokwenda tutakuata (tutakuacha) hapa, twende zetu."Hapo Mw. Aisha akafanya khofu akawa hana budi kuwafuata.Akenda bila ya furaha, mpaka wakafika Basra.''[136]

Huu ndio ukweli ulio wazi kama Sheikh Muhammad Mazrui alivyoubainisha, kwani watu walidiriki kumdanganya na kumtisha Bibi Aisha ili aelekee vitani baada ya kubainikiwa na haki kwamba vita vyake hivyo ni batili, kwa vile tayari Mtume (s.a.w.w.) alikwisha mtahadharisha navyo, ukweli alitambua baada ya kubwekewa na majibwa ya Haw-ab, na Mtume (s.a.w.w.) aliisikitikia hali hiyo itakayomtokea mmoja kati ya wake zake, na aliyekinywa kikombe hicho ni Bibi Aisha.

Vita hivyo vinabainisha wazi kwamba Imamu Ali (a.s.) alikuwa na haki kupambana nao kwa vile ni amri ya Mtume (s.a.w.w.), kwani imesihi kutoka kwake kwamba alimkataza Bibi Aisha juu ya kutoka dhidi ya Imamu Ali (a.s.), Ahmad ibn Hanbal amepokea katika Musnadi yake kwa sanadi yake kutoka kwa Qays ibn Ab Hazim, amesema: Wakati alipotoka Aisha na kufika mahala penye maji ya bani Amir wakati wa usiku, mbwa walibweka, Aisha akasema: Haya ni maji gani? Wakasema: Ni maji ya Haw-ab, Aisha akasema: Si mwenye kudhani, isipokuwa mimi ni mwenye kurudi. Baadhi ya watu waliokuwa pamoja naye walisema: Bali ni vyema lau kama utakwenda ili Waislamu wakuone, huenda Mwenyezi Mungu akaleta su-

[136] Maisha ya al-Imam Aly: uk. 37-38.

luhu kati yao. Aisha alisema: Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu alisema siku moja: Itakuwaje kwa mmoja wenu (kati ya wakeze Mtume (s.a.w.w.)) atakapobwekewa na mbwa wa Haw-ab!"[137]

Na katika riwaya ya Bazzar, amesema(s.a.w.w): "Hali itakuwaje! Ni nani kati yenu atakayekuwa mpanda ngamia mwenye manyoya mengi, atatoka na kubwekewa na mbwa wa Haw-ab,watauwawa watu wengi wa kuliani mwake na kushotoni mwake, kisha ataokoka baada ya kukaribia (kuuwawa).''[138]

Na pia katika maudhui haya tunataja yale aliyoyapokea Hakim kutoka kwa Abi Said, amesema:

"Tulikuwa tumekaa tukimsubiri Mtume (s.a.w.w.), alitujia akitokea katika moja ya nyumba za wake zake, tulisimama pamoja naye, mara kiatu chake kikakatika, akampa Ali ili akishone, Mtume (s.a.w.w.) akawa anatembea, nasi tukawa tunatembea pamoja naye, kisha akawa anamsubiri Ali, na tulisubiri pamoja naye, kisha akasema: "Hakika miongoni mwenu kuna yule ambaye atapambana katika kuieleza hii Qur'ani kama mimi nilivyopambana katika kushuka kwake." Tulijitukuza kwa kupata nafasi hiyo, na miongoni mwetu alikuwemo Abu Bakar na Umar, Mtume (s.a.w.w.) akasema: Hapana, lakini (nafasi hiyo ni ya) mshona viatu." Tulimuendea Ali kwa ajili ya kumpa hongera, akasema: Kama vile alikuwa amesikia."[139]

Ni kwamba Imamu Ali (a.s.) hakuanza kumpiga vita yoyote, bali maadui zake ndio walioongoza jeshi dhidi yake, kwa mfano, jeshi la watu waliovunja ahadi zao (jeshi la bibi Aisha), walikusanya mali nyingi sana kwa ajili ya vita na wakaingia Basra, gavana wa Imamu

[137] *Musnad Ahmad*: Jz. 6, Uk. 97

[138] Haythamiy amesema katika '*Majmau Zawaidiy* : Jz. 7, Uk. 234.: Imepokewa na Bazzar na wapokezi wake ni wakutegemewa, pia amesema ibn Hajar katika *Fat-hul Baariy*: Jz. 13, Uk. 55.

[139] *Mustadrakul Hakim*: Jz .3, Uk. 123.

Ali wa zama hizo alikuwa Uthman ibn Huneyf, Uthman alimzuia Aisha na aliyekuwa pamoja naye kuingia, walisema: Sisi hatukuja kupigana, bali tumekuja kufanya suluhu. Basi wakaandikiana kati yao mkataba wa suluhu kwamba, pasifanyike lolote mpaka atakapowasili Imamu Ali (a.s.), na kila kundi litakuwa katika hali ya usalama, kisha kila kundi likatawanyika, na Uthman ibn Huneyf akaweka silaha zake chini, askari wa Aisha walimnyofua ndevu zake na masharubu yake na kope zake na nyusi zake, na wakenda kwenye nyumba ya hazina ya mali, na wakachukua kila kilichokuwemo humo…[140]

Ikiwa hivi ndivyo watu walivyomtendea gavana wa Imamu Ali (a.s.), je, inafaa kwa Imamu Ali (a.s.) awaache hivi hivi bila ya kuwachukulia hatua stahiki?!

Vipi Imamu Ali (a.s.) awaache, na ilhali wametoka Makka wakiwa na jeshi kubwa. Ibn Wadhih al-Akhbariy anasema: "Aisha alitoka akiwa pamoja na Talha na Zubeir katika jeshi kubwa sana, na Ya'laa ibn Muniya alikuja kutoka Yemen akiwa na mali za Yemen, inayokisiwa kufikia dinari laki nne, Talha na Zubeir waliichukua mali hiyo na kuitumia katika maandalizi ya vita, na kisha wakaelekea Basra."

Na dalili ya wazi kwamba Imamu Ali (a.s.) hakuanza vita ni kauli yake kwa Maswahaba wake:

"Musiwapige mpaka watakapoanza kuwapiga, kwani kwa baraka za Mwenyezi Mungu nyinyi muna hoja (dalili), na kuwaacha mpaka wakuanzeni kukupigeni ni hoja yenu nyingine dhidi yao." Kisha Imamu Ali (a.s.) alichukua msahafu na kusema: "Na mwenye kuuchukua msahafu huu, na kuwalingania, basi malipo yake yatakuwa ni Pepo."

Kijana mmoja aliyekuwa akiitwa Muslim, alisimama na kuishika Qur'ani kwa mkono wake wa kulia na kuanza kuwalingania watu,

[140] *Tarikhul Ya'qoubiy*: Jz. 2, Uk. 181, *Tarikh Tabariy*: Jz. 3, Uk. 485 na 486

mara watu wa jeshi la Aisha wakamkata mkono wake wa kulia, kisha akaishika kwa mkoni wake wa kushoto, na kuwalingania, pia nao wakaukata, kisha wakampiga mapanga mpaka wakamuuwa."[141]

Kisha majeshi ya Aisha yakawa yanawarushia mishale kwa mfululizo askari wa Imamu Ali (a.s.), ambapo watu watatu waliuwawa au zaidi ya watatu, askari wake walinyanyua sauti zao na kusema: Mishale yao imetuchoma, na hawa hapa watu waliouwawa wako mbele yako, baada ya hapo Imamu Ali (a.s.) alisema: "Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na hakika sisi tutarejea Kwake. Ewe Mola Wangu shuhudia." Baada ya hapo akavaa nguo za kivita zilizokuwa za Mtume (s.a.w.w.) na akachukua upanga wake maarufu ujulikanao kwa 'Dhulfiqar' kisha akampa bendera nyeusi mtoto wake; Muhammad ibn Hanafiyya, na akawambia Hasan na Husein: Kwa hakika nimempa bendera mdogo wenu kuwaacha nyinyi kutokana na nafasi yenu kwa Mtume (s.a.w.w.)"[142]

Kwa hivyo uongo ulitumika katika kumdanganya Bibi Aisha, ili aendelee na vita, na si hivyo tu pale ukweli ulipombainikia yakwamba safari yake hiyo ni batili, aliamua kurudi, lakini walimlazimisha mke huyo wa Mtume na kuendelea na safari ya kwenda vitani, huku watu hao wakiwaacha wake zao majumbani mwao wakijitia hina na kujifukizia udi!

Jambo hili la mke huyo wa Mtume (s.a.w.w.) kutoka katika nyumba yake, baada ya Mwenyezi Mungu kuwataka wakae katika nyumba zao kama ilivyokuja katika Aya ya 33 ya Sura ya 33, lilibakia katika nafsi yake, na kila alipokuwa akiisoma Aya hiyo alikuwa akilia sana mpaka machozi yakawa yanaulowesha mtandio wake, kutokana na kukumbuka mauwaji aliyoyasababisha, huku akisema:

---

[141] *Usudul Ghaba*: Jz. 3, Uk. 308. *Al-Aghaniy*: Jz. 10, Uk. 203.
[142] *Sharhu Nahjul Balaghah*: Jz. 9, Uk. 111.

"Laiti ningekuwa mtu niliyesahauliwa."[143] Lakini wapi! Mke huyo wa Mtume atakumbukwa daima kutokana na ushiriki wake wa vita hivyo dhidi ya mtu mtukufu zaidi baada ya Mtume (s.a.w.w.).

Lakini Bibi Aisha haikuwa mara ya kwanza kumuudhi mtu mtukufu kama Imamu Ali (a.s.) ambaye hakuwahi kusujudia masanamu katu katika maisha yake, na ambaye ni mbora wa watu baada ya Mtume (s.a.w.w.), bali alianza kumuudhi Mtume Mtukufu na mbora wa viumbe vyote, kama ambavyo Sheikh Abdullah Saleh al-Farsy anavyotusimulia katika tafsiri yake kwa kusema:

"Wanawake ni wanawake tu. Mtume akisema katika Hadithi zake Sahihi kuwa hakutokea mwanamke aliyekamilika katika kila kitu, tangu ulimwengu ulipoanza, mpaka utamalizika, isipokuwa wanawake WANNE tu- Bibi Fatmah na Bibi Khadija na Bibi Maryam na Bibi Asiyah. Basi hata hao wake wa Mtume walikuwa mara nyingi wakimtaabisha, hasa mabibi wawili hawa- Bibi Aysha na Bibi Hafsa…"[144]

Sasa na huku kumuudhi kwake Mtume (s.a.w.w.) wasomi hao wa I.P.C. hawajui ni nani aliyekuwa katika haki, ikiwa watasema kwamba Mtume (s.a.w.w.) ndiye aliyekuwa katika haki, basi pia waelewe kwamba katika vita vya Ngamia Imamu alikuwa katika haki, kwani Mtume (s.a.w.w.) amesema wazi kwamba: "Yeyote mwenye kumuudhi Ali atakuwa ameniudhi mimi."[145]

Bila ya shaka maneno haya ya Mtume (s.a.w.w.) yatawatoa katika shaka juu ya nani alikuwa katika haki katika mapambano hayo yaliyochukua roho za Maswahaba maelfu kwa maelfu. Ama kuhusiana na ushiriki wa Zubeir katika vita hivyo, ni wazi kwamba kama ilivyokuwa kwa Bibi Aisha, ambapo hakuwa na haki yoyote ya

[143] *Tarikh Baghdadi*: Jz. 9, Uk. 183.
[144] Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy, Tafsiri ya Qur'ani Tukufu: Uk.709.
[145] *Musnad imami Ahmad*: Jz. 3, Uk. 483.

kisheria iliyomtaka kuingia katika vita hivyo dhidi ya Imamu Ali (a.s.), hali ni hivyo kwa wawili hao, hasa ikizingatiwa kwamba wao ndio waliokuwa mstari wa mbele kuhakikisha Ali ibn Abi Talib (a.s.) anakuwa Khalifa wa Waislamu.

Ama kuhusiana na ile kauli yao kwamba Talha na Zubeir walilazimishwa kutoa kiapo chao cha utii ni jambo lisilo sahihi, kama anavyosema Muhammad Abdalalla Riday: "Sayyidna Ali alikwenda msikitini, akapanda mimbari, akapewa kiapo cha utii na watu wote, ilikuwa ni Jumamosi, tarehe 19 ya mfungo Tatu mwaka 35 A.H. Lakini yasemekana kwamba Twalha na Zubair walimpa viapo vyao vya utii walipotakiwa na Sayyidna Ali wampe kiapo cha utii, nao wakamuomba Sayyidna Ali awafanye wawe ma-amir wa Basra na Kufah, lakini Sayyidna Ali akawaambia kuwa nyinyi mtakuwa pamoja nami mkinipumbaza."[146] Kwa hivyo, wawili hawa kuanzisha vita hivyo, haitokani na mapenzi waliyokuwa nayo juu ya Khalifa Uthman, bali kwa sababu tu ya kukosa madaraka waliyotarajia kuyapata kutoka kwa Imamu Ali (a.s.)

Wakati Imamu Ali (a.s.) alipokabiliana na Talha na Zubeira, aliwasemesha, aliaanza na Talha:

"Ewe Talha umemleta mke wa Mtume vitani ukipigana kwa jina lake, na mke wako umemficha nyumbani!" Ama kuhusiana na Zubeir alimkumbusha maneno aliyoambiwa na Mtume (s.a.w.w.), alisema: "Wakumbuka Mtume alikwambia: Utapigana na Ali na hali ya kuwa wewe ndiye dhalimu?" Zubeir alisema: "Kweli nakumbuka, lakini nilikuwa nimesahau." Zubeir alikula kiapo na kusema: "Sitapigana na wewe tena."[147]

Baada ya ushuhuda huo, Zubeir aliondoka katika uwanja wamapambano, lakini kwa masikitiko, hakuliamrisha jeshi lake kuacha

[146] Masahaba kumi waliobashiriwa Pepo, Uk. 58-59
[147] Kitabu kilichotangulia, Uk. 71

vita dhidi ya Khalifa wao, alishindwa hata kumnasihi mtoto wake, Abdallah ibn Zubeir kuacha vita, hatima yake ni maisha ya maelfu ya watu yakapotea! Kwa ushuhuda huu ni dalili ya wazi kwamba jeshi lililokuwa likiongozwa na Bibi Aisha lilikuwa limeshikamana na batili na jeshi la Imamu Ali (a.s.) ndilo lililokuwa la haki, na kwa nini lisiwe na haki, wakati Mtume (s.a.w.w.) amesema:

"Ali yupamoja na haki na haki ipamoja na Ali, haki inatembea naye popote anapotembea."

Ama kuhusiana vita vya Siffin vilivyokuwa vikiongozwa na Muawiya ibn Abi Sufiyan dhidi ya Imamu Ali (a.s.), uhalali wa Imamu Ali katika vita hivyo uko wazi, kama vile ambavyo batili ya Muawiya ilivyokuwa wazi, kama ambavyo Sheikh Muhammad Kasim anavyosema:

Sheikh Muhammad Kasim Mazrui ameandika yafuatayo katika maudhui aliyoyaita 'Haki na Batili':

"Siku hiyo aliuliwa Sahaba mmoja mashuhuri ambae alikuwa upande wa Sydna Aly k.w.  Nae alikuwa ni Bw. Ammar bin Yasir. Kuuliwa kwa Bwana huyu kulikuwa ni ushahidi mkubwa wa kuthibitisha kuwa Sydna Aly yu katika haki na Muawiya yu katika batili, kama utakavyoona katika kisa kifuatacho:

Alipouliwa Ammar alitoka Abdullah bin Amr bin Al-Aas akamwendea babaake na khofu kubwa akamwambia: "Baba! Mwajua kwamba mumemwua Ammar bin Yasir?" Abdullah akamwambia: "Hukusikia maneno aliyoyasema Mtume s.a.w. kwa habari ya mtu huyu?"  Akasema: "Sikumbuki." Akamwambia: "Kwani hukupata habari kwamba wakati Waislamu walipokuwa wakijenga Msikiti, ikawa watu watukua [wachukua] jiwe moja moja na tofali moja moja, Ammar akawa atukuwa mawili mawili, hata akachoka akaanguka tini [chini]. Akaja Mtume s.a.w. akawa humfuta mtanga

[mchanga] usoni mwake na huku akimwambia: "Una nini Ammar? Watu watukua jiwe moja moja na tofali moja moja na wewe watukua mawili mawili kwa kutaka thawabu nyingi; na juu ya hayo utauliwa na TAPO LA WAASI!Kwa hivyo tumekuwa WAASI ni sisi."Kusikia hivyo Amr akageuza farasi wake, akamwendea Muawiya akampa khabari. Muawiyah kwa kuchelea mambo yasije yakamharibikia, akapindua tafsiri ya maneno ya Mtume s.a.w. akasema: "Aliyemwua Ammar ni Aly, maana ndiye aliyemleta vitani. Kwa hivyo yeye na watu wake ndio waasi." Sydna Aly aliposikia maneno aliyoyasema Muawiyah, akasema: "Ikiwa ni hivyo, basi na Mtume ndiye aliyemwua Hamza, maana ndiye aliyempeleka vitani akauliwa." Ama Abdullah bin Amr, hakukubali tafsiri ya Muawiya, wala hakupigana tena mpaka kumalizika vita."[148]

Huu ndio ukweli ulivyokuwa katika masiku hayo ya vita vya kidhalimu dhidi ya Khalifa wa Waislamu. Bila ya shaka wanafunzi wanaosomeshwa kitabu hicho, kwa kutumia akili zao za kisomi watakuwa na masuala mengi ya kuwauliza walimu wao hukusiana na matukio haya ya kihistoria yenye kuhuzunisha. Bila shaka watakuwa wamejua ni nani aliyekuwa mkosa katika sakata hilo, na kukataa yale wanayotakiwa wayajue hata kama si sahihi. Baada ya hapo wanarudia kauli yao kwamba muasisi wa fitina hii ni Abdulla ibn Sabai, wanasema:

"Pamoja na makundi mengi haya, kiongozi wa udhia wote huu ni Myahudi aliekuwa mkazi wa Yemen aliyejulikana kwa jina la Abdulla bin Saba. Saba hakuwa anataka Uislamu, na alipanga mpango wa kuudhuru Uislamu mbinu aliyotumia ni kuingia katika Uislamu na kuupiga vita Uislamu kutoka ndani.

Kwa kutumia hali ya mazingira ya wakati ule alitunga na kuhubiri imani zisizokuwemo katika Uislamu, ambazo ni kila Mtume aliacha

[148] Maisha ya al- Imam Aly: uk. 52-53

‘’Wasii’’ (administrator) mtawala (mrithi wake katika ujumbe wake) na wasii wake alikuwa ndugu yake, kwa mfano Mtume Musa alimfanya Haruna kuwa “Wasii” na Mtume wasii wake ni ndugu yake Ali. Na Ali alikuwa mtu pekee aliye halali kupewa Ukhalifa.’’[149]

Hapa na pia mahali pengi mnaeleza kwamba kundi la Ibn Saba ndio linalotetea usia juu ya Ali (a.s.) na nukuu ya hapo juu mnaeleza kwamba kundi la Saba ndio lililounda mbinu za kuanza vita baada ya kuona Ali anatengeneza Amani na wapinzani wake! Mkanganyiko huu unaashiria nini? Ni kwamba mnang’ang’ania dhana na dhamira ya kuficha ukweli kwa kumchukia tu Amirul-Mu’mini Ali (a.s.). Na unapotaja kumrudi mtu ni maana kwamba mtu huyo ni mkosaji, hivyo kukubali kwamba yeye alidhamiria kwenda kumrudi Muawiya ni maana kwamba huyo Muawiya alikuwa ni mkosaji!

Vita vikubwa viliyotokea baada ya Mtume (s.a.w.w.) kufariki dunia na kupelekea mauwaji makubwa ya Waislamu wenyewe kwa wenyewe, ni jambo lililoitia doa kubwa historia ya Kiislamu, badala ya Waislamu kuyasoma hayo yaliyopita na kutafakari na kujua sababu iliyopelekea hayo na kuwajua waliosababisha hayo, kilichofanyika ni kutengenezwa mtu wa kutupiwa makosa yote yaliyofanywa na Maswahaba na kumbebesha msalaba wao!

Sidhani kwamba bibi Aisha alishawishiwa na Abdalla ibn Sabai ili atowe amri ya kuuliwa Uthman, au huko kutoka kwake dhidi ya Imamu Ali (a.s.), na wala sidhani kwamba kundi lote hilo la Maswahaba waliweza kughilibiwa na mtu huyo! Wameeleza wazi kwamba huyo Abdallah ibn Sabai alikuwa katika wanajeshi wa Imamu Ali (a.s.), basi ni Myahudi gani aliyemshawishi Bibi Aisha kuendelea na safari yake baada ya kubwekewa na mbwa wa Haw-ab na kutaka kurudi Madina?!

[149] Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari, Kitabu cha 4: Uk. 360-361.

Jambo ambalo ni zito kwa Waislamu wengi katika ndimi zao ni kusema kwamba baadhi ya Maswahaba walikosea, ni nadra sana kuiona ibara hii katika vitabu, lakini waandishi wa Kitabu hicho wamediriki kusema wazi wazi juu ya mambo ambayo wao wanaona ni makosa yaliotendwa na Imamu Ali (a.s.), na kupelekea Ukhalifa wake kutokuwa sahihi!

Ni vyema kila mtu abebeshwe mzigo wake mwenyewe na huku kutafuta watu wa kuwabebesha mizigo ya wengine hakuwasaidii chochote siku ya Kiyama, na ni bora kila mmoja alaumiwe kwa yale aliyoyatenda, na lau kama watu wenyewe walikubali fikra zisizo sahihi na kusababisha mauwaji makubwa, basi Mwenyezi Mungu atawahukumu kwa kule kukubali kumtii mtu huyo, kwani Mtume (s.a.w.w.) anasema: "Haifai kumtii kiumbe katika kumuasi Muumba." Na pia Mwenyezi Mungu amewataka Waumini wamtii Yeye pamoja na Mtume wake na wale waliona mamlaka miongoni mwao.

Qur'ani imetuelezea namna Siku ya Kiyama watu watakavyombebesha ibilisi lawama nzito kutokana na makosa yao, lakini atawaambia: "Msinilaumu mimi, bali zilaumuni nafsi zenu."Basi kama Waislamu hao walioishi pamoja na Mtume (s.a.w.w.) na kushuhudia miujiza mbalimbali, na kupata mafunzo sahihi kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) huku wengi wao wakiwa ni wenye kuhifadhi Qur'ani, kisha wakaingia katika mtego wa Myahudi,wao ndio wa mwanzo wanaostahiki kubeba mzigo wa lawama.

Katika kitabu chetu hiki tumenakili baadhi ya mandiko sahihi yanayoweka wazi kwamba Mtume (s.a.w.w.) alimuusia Ukhalifa Imamu Ali (a.s.), na hakuna hata riwaya moja iliyopokelewa na huyo mtu aliyebuniwa na Seif ibn Umar al-Tamimiy.

Kwa maelezo zaidi kwa kuhusiana na mtu huyo anayedaiwa kwamba ndiye muenezaji wa nadharia ya usia, soma kitabu kiit-

wacho 'Abdallah ibn Sabai na Ngano Nyingine' cha Allamah al-Askariy, huko utafahamu kwa kina kwamba huyo si mtu aliyepata kuumbwa na Mwenyezi Mungu katika ardhi hii, bali ni katika watu waliobuniwa na huyo Seif ibn Umar ambaye ni mashuhuri kwa kuzusha na kupachika habari za uongo, na pia unaweza kusoma kitabu kiitwacho *'al-Fitnatul Kubra'* cha Twaha Husein, na ukitaka soma kitabu kiitwacho *'Aswilatu Bayna Taswawwuf Watasshayyu'i'* cha Dakta Mustafa Kamil, ili ufahamu kwamba huyo Abdallah ibn Sabai asemwaye si mwengine bali ni Ammar ibn Yasir r.a.[150]

[150] Tijani Samawi, Ili Niwe Pamoja na Waongofu, Uk. 83.

# HITIMISHO

Haya ndio tuliyoweza kuwakusanyia katika kitabu hiki, tukiwa na lengo la kubainisha ukweli, na ikiwa kuna pahala popote pale pamemgusa mtu yeyote, basi hilo sio kusudio letu, basi itakuwa ni vyema turudi katika marejeo ya vitabu tulivyoviainisha ili tujue asili ya maneno hayo. Ni vyema kwa kila Mwislamu anayefanya utafiti juu ya historia ya yale yaliojiri baada ya kutawafu Mtume (s.a.w.w.) aifanye kwa kuzingatia misingi madhubuti ya kielimu na sio kwa misingi ya kimazoea, asitangulize dhana ya kulitukuza jambo kwa sababu tu aliyelifanya jambo hilo ni fulani hata kama halina usahihi wowote.

Katika kitabu chao hicho *'Elimu ya Dini ya Kiislamu'* kilivyobariki namna ya makhalifa watatu wa mwanzo walivyochaguliwa kwa namna tofauti, ikiwemo njia ya wasia, lakini panaposemwa kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliusia juu ya mtu anayestahiki kuwa Khalifa, huonekana ni mawazo butu na yalio kinyume na Uislamu![151]

Jambo la kushangaza ni kwamba waandishi hao wamediriki kupinga yale yaliyonakiliwa na Bukhariy na Muslim katika sahihi zao, kwa sababu hayaendani na utashi wa mawazo yao na itikadi zao. Kwani wanaelewa wazi hiyo ni hoja ya wazi dhidi ya anayekanusha Usia wa Mtume (s.a.w.w.) kwa Imamu Ali (a.s.) wa kuwa Khalifa baada yake.

Wakati umefika kwa Waislamu kuacha kurithishana habari zisizo sahihi, kama vile tulivyorithishwa uongo wa namna samaki ajulikanaye kwa jina la nguva, eti samaki huyo ana maumbile kama ya

[151] Masahaba wote waliofanya makosa makubwa na madogo mnayatetea, bali mko tayari kumtia Mtukufu Mtume na Wasii wake Ali (Amani juu yao wote) makosani kama ilivyojionyesha kwenye kitabu chenu hicho! Subuhanallah!

mwanadamu kuanzia kiunoni kadi kichwani! Huo ni uongo unaoendelea kuenezwa na kurithishwa kizazi hadi kizazi chengine.

Mfumo huu wa uandishi wa historia kwa lengo la kupotosha ukweli ni urithi uliorithiwa kutoka kwa Bani Umayya ambao ni mashuhuri katika kuwapinga Bani Hashim, chuki zao zilidhihiri pale Mtume (s.a.w.w.) alipotangaza kwamba yeye ni Mtume aliyetumwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu, walizua propaganda mbalimbali dhidi yake, waliposhindwa walipambana naye kijeshi, na pia baada ya kushindwa katika njia hii waliamua kujiingiza katika Uislamu kwa lengo la kuuharibu.

Bani Ummaya walidiriki hata kuyageuza maneno ya Mtume (s.a.w.w.), kwa sababu tu yanamnyanyua daraja Imamu Ali (a.s.), kwa mfano katika Hadithi hii: "Ewe Ali nafasi yako kwangu ni kama nafasi ya Harun kwa Musa, isipokuwa hakuna utume baada yangu."[152]

Kutokana na hali hii Hadithi zilizosahihi zinaonekana mpya katika masikio ya Waislamu wengi, kwa mfano Hadithi isemayo kwamba Mtume (s.a.w.w.) ametuachia vizito viwili: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Ahlul-Bayt. Ama ile ile iliyodhaifu, inayosema Mtume katuachia Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ndiyo iliyomashuhuri kwa Waislamu! Haya yote yamepangwa kwa lengo la kuuficha ukweli.

Mwisho kabisa, kwa heshina na taadhima, tunawaomba viongozi wa BAKWATA pamoja na Wizara ya Elimu Zanzibar, ambao tunaamini kwamba wao ni wafuasi wa Imamu Shafi, wavipitie kwa kina vitabu hivi, ili kurekebisha kasoro zilizomo. Na katika kulifanya hili wawashirikishe Waislamu wa madhehebu mbalimbali wakiwemo Mashia ili na wao watoe mchango wao. Kwa kufanya hivi tutakuwa na vitabu vya Dini vyenye kubeba ujumbe ulio sahihi.

[152] *Tah-dhib Tah-dhib*: Jz.2, Uk. 209.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuoneshe haki kwamba ni haki na atuwezeshe kuifuata.

Waswallahu Alaa Muhammad Waali Muhammad.

# VITABU VYA MAREJEO


1. Qur'ani Tukufu
2. Addurul Manthur, Assuyutiy.
3. Al-Aghaniy, Al-Asfahaniy.
4. Al-Bidayatu Wannihaya, Ibn Kathir.
5. Al-Iswaba, Ibn Hajar.
6. Al-Muswanif, Abdur Razaq.
7. Asadul Ghaba, ibn Athir.
8. Aswahiiha Liummi Malik al-Khalidiy wa Hasan Farhaniy al-Malikiy
9. Bai'atu Ali ibn Abi Talib fii Dhaw'i Riwayat
10. Elimu ya Dini ya Kiislamu, Shule za Sekondari Kitabu cha 2, I.P.C.
11. Fadhaailu Swahaba, Annasai.
12. Fat-hul Baariy, Ibn Hajar.
13. Fiqhu Sunna, Sayyid Sabiq.
14. Hilyatul- Awliyai, Abu Naim.
15. Ili Niwe Pamoja na Wakweli, Tijan Samawi.
16. Imama Wassiyasa, Ibn Qutayba.
17. Jamiul Hadith, Sayyid al-Burujurdiy.
18. Kanzul-Ummal,Al-Muttaqiy al-Hindiy.

19. Khaswaiswu Amiril Muuminina
20. Khulafau Rasul, Khalid Muhammad Khalid,
21. Kitabul Ummi. Imamu Shafi
22. Lisanul al-Arabi, Ibn Mandhur.
23. Maisha ya al-Imam Aly, Sheikh Kasim Mazrui.
24. Maisha ya Nabii Muhammad (s.a.w.w.), Sheikh Abdalla Saleh Farsiy.
25. Maisha ya Sayyidna Husein, Sheikh Abdalla Saleh Farsiy.
26. Maisha ya Sayyina Hasan, Sheikh Abdalla Saleh Farsiy.
27. Majmauz Zawaid, Al-Haythamiy
28. Masahaba Kumi Waliobashiriwa Pepo, Muhammad Abdalla Riday.
29. Maswabihu Sunna,Ali ibn Abdul Azizi al-Baghwiy.
30. Mizanul- i'dital, Dhahabiy.
31. Mughnil Labib, Ibn Hisham al-Answariy.
32. Muruju Dhahabiy, Dhahabiy.
33. Musnad Abi Ya'laa, Abu Ya'laa.
34. Musnad Ahmad, Imamu Ahmad.
35. Mustadrak Abi Daud Tayalasiy
36. Mustadrakul Hakim, Hakim Nisaburiy.
37. Riyadhun Nadhira, Majdud Din Tabariy.
38. Sahihu ibn Habban, Ibn Habban
39. Sahihu Muslim, Muslim Nisaburiy.

40. Sahihul Bukhariy,Muhammad ibn Ismail al-Bukhariy.
41. Sharhu Muslim,Annawawiy.
42. Sharhu Nahjul Balagha, Ibnul Hadidi
43. Siratul Halabiya, Ali ibn Burhanud Din al-Halabiy Ashafiy.
44. Siyaru A'lami Annubalai, Dhahabiy.
45. Sunan Tirmidhiy, Tirmidhiy
46. Sunanu ibn Majah, Ibn Majah
47. Tafsir Ibnu Kathir, Ibn Kathir
48. Tafsiri ya Qur'ani Tukufu, Sheikh Abdullah Saleh al-Farsy.
49. Tafsiru Ibn Arabiy, Ibn Arabiy.
50. Tafsiru Raziy,Raziy
51. Tafsirul-Aalusiy Al-Aalusiy
52. Tahdhibul kamali, Jamalud Din al-Mazziy.
53. Taj al-Arus, Azzubeydiy.
54. Tarikh ibn al-Athir,Ibn Athir
55. Tarikh ibn Khaldun, inb Khaldun.
56. Tarikh Madinatu Dimishqi, Ibn Asakir.
57. Tarikhu Baghdad, Al-Khatib Baghdad
58. Tarikhul Kabir, Bukhariy.
59. Tarikhul Ya'qubiy, Al-Ya'qubiy,
60. Usudul Ghaba, Ibn Athir
61. Yanaabihul Mawaddati, Al-Qanduziy

# ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo  Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo  Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia

18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu

40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)

61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)

82. Urejeo (al-Raja’a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Ngano ya kwamba Qur’ani imebadilishwa
100. Idil Ghadiri
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu

104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kumsalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Maarifa ya Kiislamu
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi

126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)

147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia

169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi naBidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana naMatarajio ya Baadaye
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake

190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Mwonekano wa Upotoshaji katika Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina (‘as) na Makhalifa
197. Uongozi na Utawala katika Mwenendo wa Imam ‘Ali (‘a)
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni wa Kisunni na Mwanachuoni wa Kishia (Al-
204. Muraja’aat)
205. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
206. Upotoshaji dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
207. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
208. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
209. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
210. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii

211. Maadili ya Ashura
212. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
213. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza
214. Imam Ali na Mambo ya Umma
215. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
216. Kuvunja Hoja Iliyotumika Kutetea Uimamu wa Abu Bakr
217. Mfumo wa Wilaya
218. Ndoa ya Mutaa
219. Vipi Tutaishinda Hofu?

# KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA

## KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba’Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n’amavuko by’ubushiya
4. Shiya na Hadithi

# ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA

## AL-ITRAH FOUNDATION KWA LUGHA YA KIFARANSA

1. Livre Islamique